# Nipashe

Jumamosi Agosti 31, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580011

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




## Udhibiti ugonjwa wa Ebola kwenye mipaka waimarishwa

UKURASA 4




UKURASA 13

# DED matatani kwa upotevu wa bil. 5/-


• **Wamo** pia watumishi 52, wadaiwa kujilipa mamilioni kwa vituo hewa vya uchaguzi, Ofisi ya Rais yasema... *Endelea ukurasa 2*



Madaktari Bingwa wa magonjwa ya moyo wa Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI), Yona Gandye na Khuzeima Khanbai wakimwekea mgonjwa mwenye umri wa miaka 101, kifaa maalum cha kurekebisha mapigo ya moyo ili yawe sawa (Pace-maker) katika taasisi hiyo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JKCI**

## Kabendera adaiwa kuugua gerezani

UKURASA 2



## JKCI yaweka rekodi mpya upasuaji moyo

• **Ni** ya babu wa miaka 101, awekewa kifaa maalum... *Endelea ukurasa 3*

**MICHEZO** **MAVUGO AMFUATA MSUVA EL JADIDA** UK.31 **MAONI, KATUNI** UK.6

HABARI KITAIFA

# Mwandishi Kabendera augua gerezani

**Na Hellen Mwango**

UPANDE wa utetezi katika kesi ya uhujumu uchumi ikiwamo kuongoza genge la uhalifu na kutakatisha fedha zaidi ya Sh. milioni 100, inayomkabili mwandishi wa habari za uchunguzi, Erick Kabendera, umeiomba mahakama kuliamuru Jeshi la Magereza kumpeleka mshtakiwa hospitali yoyote ya serikali kupimwa afya.

Wakili wa Utetezi, Jebra Kambole, alidai jana mahakamani kuwa mshtakiwa anasumbuliwa na maradhi yasiyojulikana na amekuwa kupoteza nguvu mwilini, kushindwa kupumua vizuri wakati wa usiku na kupoteza fahamu mara kwa mara.

Kambole alitoa madai hayo jana katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu jijini Dar es Salaam mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi Janeth Mtega, baada ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Augustine Rwizile, aliyepangiwa, kuwa na kazi nyingine.

Awali, Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simon, alidai kesi hiyo ilipangwa kwa ajili ya kutajwa, lakini kuna maeneo bado wanaendelea na uchunguzi, hivyo upelelezi wake bado haujakamilika.

Wakili wa utetezi, Kambole aliomba Jamhuri kuharakisha upelelezi kwa sababu mshtakiwa anakabiliwa na tuhuma ambazo hazina dhamana.

Alidai jambo la pili, mshtakiwa ana matatizo ya afya na kwamba tangu usiku wa kuamkia Agosti 21, mwaka huu, akiwa gerezani, alianza kuumwa na mpaka jana, hali yake ilikuwa haijaimarika na anapata shida kupumua nyakati za usiku.

"Mheshimiwa, mimi mwenyewe nilikwenda kumwona mshtakiwa, anashindwa kutembea, anaishiwa nguvu na wakati mwingine anapoteza fahamu, mpaka sasa ndugu zake hawafahamu kinachomsumbua ni nini," wakili huyo alidai.

"Tunaomba mahakama itoe amri kwa Jeshi la Magereza kumpeleka mshtakiwa hospitali yoyote ya serikali ikiwamo Muhimbili kwa ajili ya kupata vipimo vinavyostahili ili apate matibabu na ijulikane anaumwa nini, mshtakiwa ana haki ya kupata huduma bora."

Akijibu hoja za utetezi, Wankyo alidai kuwa atafikisha taarifa mahali husika kuhusu kuharakisha upelelezi.

Kuhusu matibabu, wakili huyo alidai Jeshi la Magereza lina utaratibu wake wa kutoa huduma za matibabu kwa watuhumiwa.

"Si sahihi mahakama hii kutoa amri kulielekeza jeshi hilo kwamba apelekwe hospitali gani kwa sababu hajasema kama amekosa huduma hiyo gerezani.

"Tuhuma zinazomkabili mshtakiwa zinasikilizwa na Mahakama Kuu, kwa hiyo, mahakama hii haina mamlaka ya kusikiliza hoja na kutoa uamuzi," Wankyo alidai.

Akifafanua zaidi, Wankyo alidai kama utetezi wana hoja, wawasilishe mbele ya hakimu aliyepangiwa kesi hiyo.

Hakimu Mtega alisema amesikiliza hoja za pande zote mbili lakini anazihifadhi mpaka hakimu anayehusika na jalada hilo atakaporudi.

Mshtakiwa alirudishwa mahabusu mpaka Septemba 2, mwaka huu, kesi hiyo itakapotajwa tena.

Katika kesi ya msingi, Kabendera anadaiwa kuwa katika siku tofauti kati ya Januari 2015 na Julai 2019, katika maeneo tofauti jijini Dar es Salaam, alitoa msaada katika genge la uhalifu kwa nia ya kujipatia faida.

Pia anadaiwa bila kuwa na sababu za msingi kisheria, alishindwa kulipa kodi ya Sh. 173,247,047.02 ambayo ilitakiwa ilipwe kwa Mamlaka ya Mapato (TRA).

Katika shtaka la tatu, inadaiwa mshtakiwa alijipatia Sh. milioni 173.2 wakati akijua kuwa fedha hizo ni za kutakatisha na zao la makosa tangulizi ya kukwepa kodi na kujihusisha na genge la uhalifu.

Wakati akisomewa mashtaka hayo, mshtakiwa hakutakiwa kujibu chochote kwa kuwa mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza kesi hiyo.



Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Ramadhan Mwinyi (kushoto), na Balozi wa Saudi Arabia hapa nchini, Mohamed Almalik (kulia), wakiwa wamewabeba watoto mapacha waliokuwa wameungana na kutenganishwa nchini Saudi Arabia, baada ya kuwasili wakiwa salama, katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere, jijini Dar es Salaam jana. Katikati ni mama yao, Jonehsia Jovitus. **PICHA; MIRAJI MSALA**

# DED matatani kwa upotevu wa mabilioni

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

BUNGE limewaweka katika wakati mgumu aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Hanang, Felix Mabula na watumishi 52 baada ya kuagiza washughulikiwe kutokana na kuisababishia serikali hasara ya Sh. bilioni 5.03 zikiwamo Sh. milioni 77.7 za Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015.

Agizo hilo lilitolewa jana na Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC), Abdallah Chikota, wakati akisoma maazimio ya kamati hiyo baada ya kupitia ripoti ya ukaguzi maalum wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa halmashauri hiyo.

Baada ya kubaini hasara hiyo, kamati hiyo iliagiza hatua zichukuliwe dhidi yao kutokana na kuwapo na ubadhirifu katika maeneo mbalimbali.

Alisema kwa sababu msimamizi mkuu wa halmashauri ni Mkurugenzi Mtendaji, mwaka 2013/14 hadi 2015/2016 alikuwa Felix Mabula, achukuliwe hatua stahiki kwa kusababisha hasara hiyo.

Alisema kuna watumishi wengine 52 wameorodheshwa kwenye taarifa ya CAG ambao wanaonekana wamehusika kwa njia moja ama nyingine kwenye hasara hiyo, nao wachukuliwe hatua.

"Kamati inaagiza mamlaka husika kuwachukulia hatua za kiutumishi na sheria watumishi wa Hanang waliotajwa katika kipindi cha ukaguzi kuhusu usimamizi usioridhisha wa halmashauri ikiwa ni pamoja na kurejesha fedha ambazo zimetumika nje ya taratibu," alisema.

Akifafanua zaidi kuhusu ubadhirifu huo, Chikota alisema kuna ubadhirifu wa Sh. milioni 77.7 katika fedha za Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015.

"Hapa tumeona ubadhirifu wa malipo kwa vituo hewa ambavyo havikuwa na wapigaji kura na magari ambayo hayakutumika katika shughuli za uchaguzi," alisema.

Aliongeza kuwa kuna matumizi ya halmashauri yasiyozingatia sheria na mfumo dhaifu wa udhibiti wa ndani ambayo yamesababisha hasara ya Sh. milioni 879.4.

"Eneo lingine ni mianya katika mfumo wa ukusanyaji wa mapato ya ndani uliosababisha ubadhirifu wa Sh. bilioni 3.4," alisema.

Chikota pia alisema kuna upotevu wa fedha za fidia ya ardhi Sh. milioni 48.4 na malipo yenye ubadhirifu katika programu ya maendeleo ya sekta ya maji Sh. milioni 395.3.

Vilevile, alisema kuna ubadhirifu katika ukusanyaji wa tozo na kodi za ardhi takribani Sh. milioni 174.8 na kuna kampuni na wazabuni ambao wakati CAG anafanya kazi katika halmashauri hiyo, aliwaita ili wapeleke vielelezo mbalimbali lakini hawakufanya hivyo.

Aliagiza Halmashauri ya Wilaya ya Hanang itoe taarifa kwa Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP), PPRA na Brela kuhusu kampuni nane zilizoshindwa kuwasilisha taarifa muhimu kikiwamo cheti cha mlipa kodi na usajili wa kampuni ili wachukuliwe hatua zinazostahili.

"Hizi kampuni zilihusika kwa namna moja na ubadhirifu wa fedha katika halmashauri, wanatakiwa kupeleka nyaraka lakini hadi mkaguzi anaondoka, hawakupeleka taarifa hizo,"alisema.

Akizungumza mara baada ya kupewa maagizo hayo, Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mitaa na Serikali ya Mitaa (Tamisemi), Josephat Kandege, alisema wamepokea maelekezo yao kama yalivyoelekezwa na Ofisi ya CAG na watahakikisha wanasimamia utekelezaji wake.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA,
Tarehe 30/08/2019.

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya JUMAMOSI tarehe **31/08/2019** kampuni ya **SINO-SHINE OVERSEARS CONSTRUCTION & INVESTMENT** itapita bila mizigo kutoka KABANGA kuelekea SUMBAWANGA gari yenye namba za usajili:

   **T349 BNT/T 646 BCJ.**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
   Urefu-mita 20.0
   Upana –mita 3.0
   Kimo – mita 2.90

3. Njia itakayotumika **KABANGA hadi SUMBAWANGA kupitia MPANDA** gari litasafiri muda wa mchana tu. **(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)**

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**

115397402

SHABIKI MKUU WA TAIFA STARS




# Mzee wa miaka 101 apasuliwa moyo

**Na Joseph Mwendapole**

KWA mara ya kwanza madaktari bingwa wa magonjwa ya moyo wa Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI) wamemwekea mgonjwa mwenye umri wa miaka 101 kifaa maalum cha kurekebisha mapigo ya moyo ili yawe sawa (Pacemaker).

Kifaa hicho kisaidizi cha moyo huwekwa kwa wagonjwa ambao mapigo yao ya moyo yako chini ya asilimia 30 kwa dakika.

Akizungumza baada ya kumfanyia upasuaji mdogo na kumwekea mgonjwa huyo kifaa hicho, Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Moyo wa JKCI, Dk. Yona Gandye, alisema mara nyingi wanawawekea kifaa hicho wagonjwa wenye umri wa miaka 80 kushuka chini, lakini jana iliandikwa rekodi mpya kwa taasisi hiyo kumwekea mgonjwa wa umri wa miaka 101.

"Kabla ya kufanya upasuaji, tulimfanyia mgonjwa uchunguzi wa kina na kugundua mfumo wake wa umeme wa moyo unahitilafu na mapigo ya moyo yapo chini ya asilimia 20, hivyo tumemwekea kifaa ambacho kitausaidia moyo kuongeza mapigo yake na mara baada ya kumwekea kifaa hiki mapigo yake ya moyo yako vizuri kati ya asilimia 60 na 100 kwa dakika," Dk. Gandye alisema.

Akizungumza kwa furaha mara baada ya baba yake kuwekewa kifaa hicho, Saimoni Maina, alisema matatizo ya baba yake yalianza mwaka mmoja uliopita na kutibiwa katika hospitali mbalimbali mkoani Manyara na Arusha.

Alisema hospitali za mikoa hiyo ziligundua kuwa mapigo yake ya moyo yako chini, hivyo kumpa rufaa kwa ajili ya kutibiwa JKCI.

"Baba alikuwa akianguka na kupoteza fahamu mara kwa mara ndipo tukaamua kumpeleka hospitalini kwa ajili ya matibabu ili kufahamu anasumbuliwa na tatizo gani.

"Tunashukuru sana uwapo wa taasisi hii kwani baba yetu amefanyiwa upasuaji na hali yake inaendelea vizuri kama mnavyomwona," Maina alisema.

Kwa upande wake, Mzee Maina alisema kabla ya kufanyiwa upasuaji huo, alikuwa akipata maumivu makali sehemu za moyo, kuanguka, kupoteza fahamu na kushindwa kutembea, lakini baada ya kufanyiwa upasuaji huo, hali yake imebadilika na maumivu yamepungua.



Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, akizungumza na wananchi wa Kijiji cha Mayomboni kilichopo Wilaya ya Mkinga mkoani Tanga, alipokwenda kutangaza uamuzi wa serikali kufuta Mashamba matatu ya Mkomazi Plantantions Co Ltd maarufu kama MOA, jana. Wa kwanza kushoto ni Mbunge wa Jimbo la Mkinga mkoani Tanga, Dustan Kitandula. **PICHA: WIZARA YA ARDHI**

# Polisi waua wanne tuhuma ujambazi

**Na Jovin Lamwel**

JESHI la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam limewaua watu wanne kwa tuhuma za ujambazi jijini.

Limeeleza kuwa mmoja wa watuhumiwa hao alifariki dunia wakati akiendelea na matibabu Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) alikopelekwa baada ya kuzidiwa wakati likimhoji. Kamanda wa kanda hiyo, Lazaro Mambosasa, alidai majambazi hao waliuawa katika matukio tofauti yaliyotokea jijini.

Alidai katika tukio la kwanza, mtuhumiwa Elia Kituli (55), mkazi wa Kivule wilayani Ilala aliyekuwa anatafutwa, alikamatwa baada ya kukimbia kwenye tukio la ujambazi lililotokea mwanzoni mwa mwezi uliopita.

Katika tukio hilo, Kamanda Mambosasa alidai majambazi wawili waliuawa na kukutwa na silaha mbili aina ya bastola huko Kitunda Machimbo.

"Kituli alikimbia lakini tulimkamata akiwa na silaha moja aina ya Rifle yenye namba MK3-90893 ikiwa na risasi tatu ndani ya kasha na vifaa mbalimbali vilivyoporwa maeneo tofauti," alidai.

Mambosasa alidai mtuhumiwa huyo alikutwa na Ipad mbili aina ya Samsung na Apple, simu janja nane aina ya Infinx, Samsung, Nokia, Huawei, Techno na Iphone.

"Alikutwa na saa moja ya mkononi aina ya Seiko 5 rangi ya dhahabu, kisu, kamera ya kidigitali moja aina ya Sony, kompyuta mpakato moja aina ya Toshiba, kisikiliza sauti 'earphone' moja na chaja mbalimbali za simu," alidai.

Kamanda Mambosasa alidai mtuhumiwa huyo baada ya kukamatwa wakati akiendelea kuhojiwa Kituo cha Polisi, aliugua ghafla na kupelekwa Muhimbili na baadaye alifariki dunia.

Katika tukio lingine, Kamanda Mambosasa alisema lilitokea Jumapili iliyopita usiku maeneo ya Pugu, ambapo Jeshi la Polisi liliwaua majambazi watatu na kukamata silaha mbili aina ya Shortgun na bastola.

Alisema walimkamata Omary Athuman (39), mkazi wa Mkuranga ambaye alikuwa anatafutwa kwa kujihusisha na matukio ya unyang'anyi wa kutumia silaha.

Pia alisema katika mahojiano, mtuhumiwa alikiri kujihusisha na matukio mbalimbali na amewahi kufungwa miaka 30 jela na alitoka kwa rufaa na kujiunga na kundi lingine la ujambazi.

"Katika mahojioano, alikiri kushirikiana na wenzake watatu ambao walipanga kwa pamoja kwenda kupora fedha duka la M-Pesa lililoko maeneo ya Pugu shuleni na alikuwa tayari kuwapeleka askari eneo la tukio ili kuweka mtego," alisema.

Kwa mujibu wa Kamanda, wakati askari wakiwa eneo la Pugu wakiwa wameweka mtego ili kuwakamata washirika wa mtuhumiwa huyo wa ujambazi, ghafla majambazi hao waliwarushia risasi askari ndipo walipojibu mapigo na kuwajeruhi watatu ambao ni Omary Athuman, Fullsaba na Babu Shobo ambao baadaye walifariki dunia Hospitali ya Muhimbili.

Alidai watuhumiwa hao wa ujambazi walikutwa na silaha mbili namba YA- 1547 aina ya Shortgun iliyokuwa imekatwa kitako, mtutu wenye risasi tatu, ganda moja la risasi na bastola moja iliyokuwa imefutwa namba ikiwa na risasi mbili na maganda mawili ya risasi.

Kamanda Mambosasa alidai silaha hiyo aina ya Shortgun ilibainika kuwa iliporwa Aprili 13, mwaka huu na kesi yake ya unyang'anyi ilifunguliwa Kituo cha Polisi Ukonga na kampuni ya ulinzi ya Alarms Security.

Alidai silaha hiyo ilitumika kupora Sh. milioni sita pamoja na simu tano za aina mbalimbali maeneo ya Markaz Gongo la Mboto kwa mfanyabiashara Justine Chaula.

**KUDAI NDEGE**

Katika tukio lingine, kamanda Mambosasa alidai viongozi watatu waliodaiwa kuwa waratibu wa maandamano yaliyofanyika Jumatatu kwenda Ubalozi wa Afrika Kusini nchini kushinikiza kuachiwa ndege ya serikali, wameachiwa kwa dhamana.

"Upelelezi wa tukio hili bado unaendelea na kama utapatikana, ushaidi wa kutosha basi watapelekwa mahakamani," alisema.

SHABIKI MKUU WA TAIFA STARS




TAIFA STARS vs BURUNDI
SEPTEMBA 8, 2019 • UWANJA WA TAIFA

HAIUZWI KWA WALIO NA UMRI CHINI YA MIAKA 18. TAFADHALI KUNYWA KISTAARABU.



Raia wa kigeni wanaoingia mpaka wa Rusumo wakinawa mikono ikiwa njia mojawapo ya kukabiliana na Ebola. **PICHA: AUGUSTA NJOJI.**

# UDHIBITI MKALI EBOLA MIPAKANI

## Magari yatoa taarifa kilomita 20 kabla ya kufika mpakani, abiria wapimwa na kunawa mikono....

**Na Augusta Njoji, KAGERA**

KUTOKANA na kuwapo kwa tishio la Ebola kwa nchi za maziwa makuu ikiwamo Tanzania, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto imechukua tahadhari kubwa kwenye mipaka yake ili kudhibiti ugonjwa huo kuingia nchini.

Miongoni wa tahadhari hizo ni pamoja na madereva na makondakta wa magari kutoa taarifa umbali wa kilomita 20 kabla ya kufika mpaka husika kama kuna mtu anahisiwa kuwa na ugonjwa huo, kunawa mikono kwa maji yenye dawa, vifaa vya kupima joto ili kubaini mgonjwa na eneo maalum la kumweka mgonjwa anayehisiwa.

Nipashe ilishuhudia kuwapo kwa tahadhari hiyo katika mpaka wa Mtukula ambao Tanzania inapakana na Uganda na Rusumo ambao inapakana na Rwanda ambayo iko mkoani Kagera.

Katika ziara ya waandishi kuangalia uimarishwaji wa huduma za afya mipakani, Ofisa Afya Mfawidhi wa Kituo cha Afya Mtukula, Mathew Godfrey, alisema juzi kuwa serikali imetoa vitendea kazi ili kukabiliana na ugonjwa huo na kwamba imejipanga vya kutosha kuhakikisha hauingii nchini.

"Tunafanya 'sensation' kwa abiria, madereva na watu wote wanaohusika kwenye magari yanayopita kwenye mpaka wetu na pia jamii inayotuzunguka wakiwamo madereva wa bodaboda. Tumeweleza wakiona au kumhisi mtu mwenye dalili za kuwa na joto kali, kutapika, viungo kuuma na kutokwa na damu sehemu za mwili, watoe taarifa kwenye ofisi iliyoko mpakani, "alisema.

Godfrey alisema waendesha pikipiki wamepewa elimu ya utoaji taarifa wanapomhisi mgonjwa mwenye dalili hizo na ugonjwa huo unasambaa kwa kushikana.

"Kutokana na kusambaa pia kwa kushikana, tunatoa huduma hapa mpakani ya kunawa mikono ili kuchukua tahadhari kama wanapokuwa safarini wameshikana na mgonjwa wa Ebola. Ikitokea tumempata mhisiwa wa ugonjwa wa Ebola, kuna eneo maalum tunamhifadhi na kutoa taarifa kwa hospitali ya wilaya. Wanamchukua na kumpeleka sehemu husika," alisema.

Aidha, Godfrey alisema makondakta au madereva wamekuwa wakitoa taarifa kabla ya kufika kilometa 20 mpakani kama gari liko salama, hakuna mgonjwa au kama kuna mgonjwa wanayemhisi.

"Baada ya taarifa hiyo wanapofika mpakani tunakagua abiria mmoja mmoja kwa kupima joto na kuthibitisha kama kilichosemwa na abiria au dereva kipo salama. Joto la mtu mwenye dalili au anayehisiwa akikutwa na nyuzi joto 38 au zaidi, tunapima mmoja mmoja kwa kutumia 'hand scanner' ambayo tumeletewa na wizara," alisema.

Naye Ofisa Afya Mpaka wa Rusumo, Osward Kimasi, alisema wamejipanga kwa kiwango kikubwa kudhibiti ugonjwa huo kuingia nchini na pale inapotokea abiria anashukiwa kuwa na dalili za Ebola, wanachukua taarifa zake na kupelekwa hospitali ya wilaya na inapothibitika kuwa si Ebola , anaruhusiwa kuendelea na safari.

"Pia tuna vikaratasi maalum tunavitoa kwa mtu ambaye tayari tumemfanyia 'scanning', hivyo anapokwenda kwa ofisa uhamiaji au TRA (Mamlaka ya Mapato Tanzania), anaonyesha kikaratasi hicho ndipo anaendelea kupewa huduma na kama hatapita kukaguliwa hapa kule akienda lazima arudishwe hapa kupimwa," alisema.

Alisema ushirikiano uliopo ni wa kila siku kwa maofisa wote wa TRA, Uhamiaji, Polisi, walinzi na madereva wa pikipiki na magari.

"Watu wanaotoka Congo tumewawekea fomu maalum ili kuonyesha atafikia wapi akiwa Tanzania na siku atakazokaa na kurejea nchini kwake ili kufuatilia kwa karibu kudhibiti ugonjwa huo," alisema.

Ushauri watolewa

Ofisa Mfawidhi Mamlaka ya Mapato (TRA) kwenye mpaka wa Mtukula, William Mkenda, alisema kutokana na kuwapo mwingiliano wa watu kwenye masoko ya mipaka ya kuingilia Tanzania, ni vyema elimu ya kutosha kwa wananchi wanaozunguka mipaka hiyo ikatolewa ili kukabiliana na ugonjwa huo.

Alisema elimu hiyo itolewe pia kwa viongozi wa serikali za mitaa wa maeneo hayo kwa kuwa ni rahisi kubaini kabla ya kuingia eneo la mpaka.

"Mtu anavyoambiwa mpakani anaweza kufikiri mpaka unatenganishwa na ukuta au kizuizi watu wa jamii moja na wengine wasionane lakini si hivyo. Ukiona uhalisia wa mpaka ni watu wanaoweza kuingiliana kwa namna fulani kubwa sana,"alisema.

Aliongeza kuwa: "Hapa ndani kwenye mpaka tumejipanga vizuri lakini inatakiwa elimu itolewe kwa hawa viongozi wa serikali za mitaa kwa kuwa kuna watu wanatoka sokoni upande mmoja kwenda mwingine ni rahisi wao kumuona mtu hatua za awali na kutoa taarifa kabila ya kukutana na mtu mwingine."

Alisema maofisa wa idara mbalimbali katika mpaka huo wameshapewa elimu mwaka jana mara baada ya ebola kuibuka nchini Congo hivyo kila mmoja anashiriki kuhakikisha ugonjwa huo hauingii nchini.

"Pia hivi karibuni nchini Uganda ambapo kuna watu walishukiwa kuwa na maambukizi ya Ebola kulikuwa na utayari hapa mpakani iliendeshwa na watu wa idara ya afya juu ya kumtambua mtu mwenye ugonjwa huo na kutoa taarifa na kukabiliana na ugonjwa huo," alisema.

MADEREVA WAFUNGUKA

Naye dereva wa lori kutoka Congo, Ally Mpame, alisema nchini kwao wamejipanga kwa kiwango kikubwa kudhibiti ugonjwa huo na kuwataka watu wasipende kushikana mikono.

"Nawashauri madereva wenzangu ambao tunaenda kwenye nchi hizo kuhakikisha kila tunapoingia na kutoka tunaangaliwa afya zetu ili tusiingize Ebola nchini Tanzania," alisema.

Mwendesha pikipiki kutoka Rwanda, Damasent Twisent, alishauri katika mpaka wa Rusumo waendesha vyombo hivyo wanaobeba abiria, nao kupimwa kila wanapobeba abiria badala ya abiria pekee kupimwa.



Ofisa Afya wa mpaka wa Rusumo, Osward Kimasi, akizungumza na waandishi wa habari kuhusu ugonjwa wa Ebola.



Wafanyakazi wa kampuni ya Gasco, wakitandaza mabomba kwaajili ya usambazaji wa gesi ya matumizi ya nyumbani katika nyumba 85 zikiwamo za mawaziri, katika eneo la Mikocheni, jijini Dar es Salaam mapema wiki hii. **PICHA: JOHN BADI**

# Serikali yafuta miliki mashamba ya vigogo

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imefuta miliki ya mashamba matatu ya Mkomazi Plantantions, maarufu MOA, yaliyoko Wilaya ya Mkinga mkoani Tanga kutokana na kukiuka masharti ya uendelezaji.

Imeelezwa kuwa moja ya masharti yaliyokiukwa ni mashamba hayo kutoendelezwa na hayajalipiwa kodi ya pango la ardhi.

Uamuzi huo ulitangazwa jana na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, alipozungumza na wananchi wa Mayomboni wilayani Mkinga alipokwenda kutatua mgogoro wa muda mrefu katika eneo hilo.

Mashamba yaliyofutiwa ni yenye hati Na. 9780 na ukubwa wa ekari 14,688, shamba Na. 4268 lenye ekari 804 na shamba lenye hati Na. 9781 lenye ekari 246.

Kutokana na uamuzi huo, jumla ya vijiji 10 vyenye kaya 3,236 zenye wakazi 16,450 zitanufaika na uamuzi wa serikali kutokana na wananchi wake kuvamia mashamba hayo na kufanya maendelezo ya kujenga makazi, shule na kuendesha shughuli za kilimo cha mazao ya kudumu na ya muda mfupi.



Vijiji vilivyonufaika na uamuzi wa serikali ni Kilulu-Dunga, Zingibari, Mwaboza, Mwakikoya, Mhandakini, Nkanyeni, Sigaya, Mayomboni, Ndumbani na Moa.

Akizugumza wakati wa kutangaza uamuzi huo, Waziri Lukuvi alisema uamuzi wa kufuta mashamba hayo matatu unafuatia maombi yaliyotumwa kwa Rais John Pombe Magufuli ya kutaka kufutwa mashamba hayo kutokana na kutoendelezwa na wamiliki wake kwa muda mrefu.

Alisema Rais ameridhia maombi hayo kwa kuwa serikali imekuwa ikisisitiza utekelezwaji wa Sheria ya Ardhi Na. 4 ya Mwaka 1999 inayotaka uendelezaji wa mashamba ambayo yamemilikishwa katika maeneo mbalimbali nchini.

Waziri huyo pia aliagiza kufanyika upimaji katika vijiji vyote 10 na kuainishwa mipaka ya vijiji hivyo na kupatiwa hati ili wananchi wanaoishi kwenye vijiji hivyo wasibughudhiwe.

Lukuvi (pichani) pia alitaka maeneo yaliyopangwa kwa ajili ya uwekezaji katika shamba yaliyofutwa kuachwa kwa ajili ya shughuli hiyo ikiwamo mwekezaji wa Katani, Azka International Tanzania mwenye ekari 500 pamoja na maeneo ya viwanda.

Katika hatua nyingine, Waziri Lukuvi aliagiza kufanyika uhakiki wa mashamba mengine ya Kwa Mtili Estates Co. Ltd yaliyoko Mkinga mkoani Tanga ambayo alibaini ekari 58 pekee ndiyo zilizoombwa kufutwa kwa Rais kutokana na kutoendelezwa huku mmiliki wake ikidaiwa kumiliki ekari 2,841.

Hatua hiyo inatokana na Mkuu wa Idara ya Ardhi na Maliasili katika Halmashauri ya Wilaya ya Mkinga, Obed Katonge, kueleza kuwa Kwa Mtili Estates Co Ltd inalo shamba lenye ukubwa wa ekari 2,841 tofauti na inavyoonekana katika kumbukumbu za ofisi ya Msajili wa Hati Kanda ya Kaskazini ambazo ni 58.

Lukuvi aliagiza wataalamu wa ardhi kutoka Kanda ya Kaskazini kufanya uhakiki huo katika kipindi cha mwezi mmoja na kumpa taarifa ya uhakiki huo mwisho wa mwezi ujao na pale itakapothibitika kuna ujanja uliofanyika wa kumwongeza mmiliki wa shamba hilo, hatua kali zitachukuliwa dhidi ya wahusika.

Mbunge wa Mkinga, Dustan Kitandula, aliishukuru serikali kwa kusikiliza kilio cha muda mrefu cha wananchi wanaoishi eneo la shamba lililofutwa la kutaka kurejeshewa ardhi yao waliyokuwa wakiitumia kwa shughuli mbalimbali.

Alisema mgogoro wa ardhi baina ya wananchi wa Mkinga na wamiliki wa mashamba ya Mkomazi Plantantions Co. Ltd ni wa muda mrefu na anaamini uamuzi wa serikali umepeleka furaha jimboni kwake.

# Tanzania, UNHCR kutatua changamoto za wakimbizi

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imesema itaendelea kushirikiana na Shirika la Kuhudumia Wakimbizi la Umoja wa Mataifa (UNHCR) kutatua changamoto zinazotokana na uwapo wa wakimbizi nchini.

Katika kutatua changamoto hizo, serikali imesema miongoni mwa mambo ya kushughulikiwa ni pamoja na kutafuta suluhu ya kudumu kwenye nchi zao ili wakimbizi hao warejee kwao kuendelea na shughuli za maendeleo.

Waziri Mkuu Kassim Majaliwa (pichani) alisema hayo jana katika mazungumzo yake na Kamishna Mkuu wa UNHCR, Filippo Grandi, kwenye Kituo cha Maonyesho cha Yokohama nchini Japan baada ya kuhitimishwa kwa Mkutano wa Saba wa Kimataifa wa Tokyo kuhusu Maendeleo ya Afrika (TICAD 7).

Katika mazungumzo hayo, Waziri Mkuu alisisitiza umuhimu wa UNHCR kuisaidia mikoa inayokaliwa na wakimbizi kutokana na kuharibiwa kwa mazingira.

"Hata hivyo, serikali ya Tanzania itaendelea kushirikiana na UNHCR kuimarisha ulinzi wa maeneo ya wakimbizi ili wananchi wa maeneo hayo waendelee kuishi kwa amani na utulivu," alisema.

Kwa upande wake, Grandi alisema amefurahishwa na utayari wa serikali ya Tanzania katika kupokea wakimbizi na usikivu wa Rais John Magufuli katika kushughulikia changamoto za wakimbizi.

Waziri Mkuu yuko nchini Japan akimwakilisha Rais Magufuli kwenye Mkutano wa TICAD 7 uliomalizika jana.

Katika mkutano huo, Waziri Mkuu ameambatana na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika ya Mashariki, Prof. Palamagamba Kabudi na viongozi mbalimbali kutoka Serikali ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.






## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# *Yanga, Zahera ushirikiano unahitajika kuitoa Zesco*

**HATIMAYE** Tanzania Bara imebakiwa na timu mbili tu kwenye michuano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa na Kombe la Shirikisho barani Afrika baada ya wawakilishi wawili, Simba na KMC FC kutolewa kwenye raundi ya awali.

Kwa sasa macho na masikio yote kwa Watanzania yameelekezwa kwa Yanga inayoiwakilisha nchi kwenye Ligi ya Mabingwa na Azam FC inayopeperusha bendera ya Tanzania katika michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Simba ambayo msimu uliopita ilifika robo fainali ya Ligi ya Mabingwa kwenye michuano hiyo inayoandaliwa na Shirikisho la Soka barani Afrika (Caf), imeyaaga mashindano hayo baada ya kutolewa kwa faida ya bao la ugenini na UD Songo ya Msumbiji kufuatia sare ya bao 1-1 ikiwa ni baada ya awali kutoka suluhu.

Kwa upande wa KMC FC ambayo hii ilikuwa ni mara ya kwanza kupanda Ligi Kuu Bara msimu uliopita na kufanikiwa kuipeperusha bendera ya Tanzania kwenye Kombe la Shirikisho Afrika, yenyewe imetolewa na AS Kigali ya Rwanda kwa jumla ya mabao 2-1 baada ya mechi ya awali ugenini kutoka suluhu.

Aidha, Yanga ambayo imeitoa Township Rollers ya Botswana kwa jumla ya mabao 2-1 kufuatia sare ya bao 1-1 Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam kabla ya kwenda kushinda kwa bao 1-0 ugenini, sasa itakabiliana na Zesco ya Zambia katika raundi ya kwanza ya michuano hiyo.

Hivyo, Yanga inahitaji maandalizi makubwa ili kuweza kuitoa Zesco ambayo iliitoa Green Mamba FC ya Eswatini kwa jumla ya mabao 3-0, wakati pia Azam FC iliyoitoa Fasil Kenema ya Ethiopia kwa mabao 3-2, inapaswa kufanya kazi ya ziada kuitupa nje Triangle FC ya Zimbabwe iliyoiondosha Rukinzo FC ya Burundi kwa jumla ya mabao 5-0.

Hakika haitakuwa kazi rahisi kwa wawakilishi wetu hao waliosalia kwenye michuano hiyo, ambayo tunatamani kuwaona wakisonga mbele ili kuweza kuiongezea pointi Tanzania na kufanikiwa kuingiza tena timu nne kwenye michuano hiyo ya Caf msimu ujao.

Na wakati huu timu hizo zikijiandaa kuelekea mechi hizo, tungependa kuona viongozi wa klabu hizo wakizingatia zaidi progamu ya mazoezi ya makocha ili kuondoa lawama pindi timu zinapofanya vibaya.

Tumelazimika kukumbusha suala hilo, kutokana na ukweli kwamba, kabla ya Yanga kuelekea Botswana kwenye mechi ya marudiano dhidi ya Township Rollers, iliweka kambi mikoa ya Kaskazini, Kilimanjaro na baadaye Arusha na kisha kucheza mechi mbili za kirafiki dhidi ya Polisi Tanzania na AFC Leopards ya Kenya. Hata hivyo, Kocha Mkuu wa Yanga, Mwinyi Zahera alilalamikia kambi hiyo akidai kwamba haikuwa na maslahi ya kuwasaidia wachezaji na badala yake uongozi ulilenga kujiingizia kipato zaidi badala ya kumulika kuiandaa timu kutokana na mechi ya Ligi ya Mabingwa dhidi ya Township Rollers iliyokuwa ikiwakabili.

Zahera alienda mbali zaidi kwa kueleza kuwa alishindwa kuwachezesha wachezaji wake muhimu katika mechi hizo za kirafiki kutokana na viwanja vibovu jambo ambalo alihofia wanaweza kuumia na kumgharimu kuelekea mechi hiyo ya marudiano.

Ni wazi kabisa, kama Yanga ingepoteza mchezo huo Zahera tayari alishapata sababu ya kujitetea, jambo ambalo hata hivyo liliepukika kutokana na timu hiyo kushinda na kufanikiwa kusonga mbele. Septemba 13, mwaka huu siku ambayo mechi ya kwanza kati ya Yanga na Zesco itapigwa Uwanja wa Taifa, si mbali, hivyo maandalizi ya kina yanahitajika na umoja kati ya uongozi wa klabu hiyo na benchi la ufundi.

Hatutarajii tena kusikia kukiwapo na kutupiana lawama kati ya benchi la ufundi na uongozi wa Yanga, kwani lengo letu ni kuona Yanga na Azam zikifika mbali katika michuano hiyo ili Tanzania iweze kuingiza tena timu nne kwenye michuano hiyo msimu ujao.

Na hilo litawezekana tu kama kwa wiki hizi mbili maandalizi ya kina kwa kila timu yatafanyika na kwa upande wa Yanga ikimulika zaidi safu yake ya ushambuliaji ambayo imekuwa ikikosa mabao mengi katika mechi za kimashindano na za kirafiki ilizocheza hadi sasa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# *Yanga: Hakuna kapa isiyokuwa na usubi*

Na Barnabas Maro

**'USUBI'** ni wadudu wadogo wanaofanana na mbu. 'Kapa' ni sehemu ya pwani inayoota mikoko na ambayo huwa na tope na haikosi usubi. Maana yake hakuna msitu wa mikoko usiokuwa na usubi.

Methali hii yatufunza kuwa hakuna kitu kisichokuwa na kasoro au hitilafu zake. Kila kitu kina faida na hasara zake.

Tangu Yusuf Manji alipojiuzulu Uenyekiti wa Yanga, klabu hiyo kongwe ni kama ilifiwa na mlezi wake kwani aliiacha katika ufukara mkubwa. Hali hiyo iliiweka Yanga kwenye matatizo makubwa ya fedha hata kushindwa kulipa mishahara ya wachezaji na stahiki zao, kadhalika watumishi wengine wa klabu.

Wanachama na mashabiki wa Yanga hawakukubaliana na Manji kujitoa kwenye uongozi lakini yeye alisimama kidete kutetea msimamo wake. Jambo hilo lilisababisha klabu ya Yanga ishindwe kujiendesha yenyewe hata kuitwa 'ombaomba' (hali duni inayohitaji msaada kutoka kwa wengine).

Watani zetu (Simba) wakawa wanawatania kwa kuwaita 'Yanga bakuli' yaani wanaopita na bakuli mitaani na viwanjani kuomba msaada. Hata Yanga ilipokuwa inapambana na timu zingine, wapiga picha za runinga hawakukosa kuonesha picha za watu waliokuwa wakichangisha fedha kwa ajili ya Yanga.

Ilikuwa fedheha ya aina yake kwa klabu kongwe kuomba msaada viwanjani. Ni jambo lililokera wengi, lakini hakukuwa na jinsi ila kukubaliana na hali halisi.

Hata hivyo, wahenga walisema: "Hakuna kubwa lisilo ukomo." Maana yake kila jambo lina mwisho wake kwani hata maisha ya binadamu hufikia kikomo chake. Methali hii hutumiwa kumliwaza mtu anayepambana na hali ngumu au matatizo kuwa ajitahidi kuvumilia hatimaye yatafikia mwisho wake.

Hivi karibu, wanachama wa Yanga walifanya uchaguzi na kumchagua Dk. Mshindo Msolla kuwa Mwenyekiti wao kwa kumpa kura 1,276 huku mgombea mwenzake wa nafasi hiyo, Dk. Jonas Tiboroha aliyepata kuwa Katibu Mkuu wa Yanga enzi za Mwenyekiti Yusuf Manji, akipata kura 60 tu.

Hata hivyo, ingawa Dk. Jonas Tiboroha alishindwa, alikubali matokeo ya uchaguzi huo na kumtaka Mwenyekiti mpya (Dk. Msolla) avunje makundi kama alivyoahidi wakati akijinadi. Akasema kwa roho nyeupe amekubaliana na matokeo na kutoa rai kuwa kambi zote zivunjwe ili Yanga iwe moja chini ya Mwenyekiti Dk. Mshindo Msolla.

Aliyeshinda nafasi ya Makamu Mwenyekiti ni Fredrick Mwakalebela aliyewashinda wagombea wengine watano kwa kupata kura 1,206. Mwakalebela alipata kuwa Katibu Mkuu wa TFF zamani. Walioshinda nafasi za ujumbe ni: Frank Kamugisha, Arafat Haji, Salum Rupia, Bahati Mwaseba, Saad Kimji, Rodgers Gumbo, Ahmad Islam na Dominic Kata.

Viongozi hawa wameitwaa Yanga ikiwa na matatizo mengi yanayohitaji hekima, maarifa na juhudi kubwa kuirejesha pale ilipokuwa zamani. Kama kuna kiongozi aliyechaguliwa kwa lengo la kujinufaisha badala ya kuinufaisha Yanga, ni vema ajiondoe mapema na kuwaachia wenye uchungu na Yanga, wenye lengo la kuitoa kwenye umasikini uliokithiri.

Viongozi wapya wanapaswa kuzingatia mambo makubwa manne. Wahakikishe wanapata hatimiliki (waraka wa kisheria unaompa mhusika haki ya kumiliki ardhi au mali nyingine) iliyo mikononi mwa mtu asiyetaka kuipa klabu. Kama atakataa kuitoa kwa viongozi, ashitakiwe mahakamani ili haki itendeke ili hatimiliki irejeshwe klabuni.

Hatimiliki hiyo itumiwe na viongozi kama dhamana ya kupata mkopo wa Benki itakayokubali kujenga ile nyumba iliyokuwa makao makuu ya Yanga zamani kwenye makutano ya mitaa ya Mafia/Nyamwezi jijini Dar es Salaam. Jengo hilo laweza kuwa la ghorofa 10 au zaidi, maalum kwa biashara kama hoteli na maduka, likiwamo duka la klabu litakalouza jezi, skafu, vikombe vya chai, glasi na vifaa mbalimbali vya michezo vyenye nembo ya Yanga.

Pili lile ghorofa linalotumika sasa kule Jangwani, lifanyiwe ukarabati mkubwa ili liwe maalum kwa ofisi za viongozi wa klabu na pia malazi ya wachezaji wanapokuwa kambini badala ya kukodi hoteli za watu binafsi kama ilivyozoeleka.

Ghorofa ya chini iwe mahsusi kwa wachezaji kupata chakula, vinywaji baridi na eneo maalum la kuwapa wachezaji mafunzo ya nadharia (maelezo ya kanuni na namna ya kufanya jambo fulani) kwa muktadha huu, kandanda.

Tatu, viongozi wapya wafute kabisa mpango wa ujenzi wa uwanja wa mpira pale Jangwani kwani ni eneo linalofurika maji wakati wa mvua za masika na vuli. Ni eneo ambalo chini yake kuna bomba kubwa la maji yanayokwenda kwenye Hospitali Kuu ya Rufani Muhimbili. Kwa ufupi wakubaliane na maelezo ya serikali kuwa eneo lile halifai kujengwa uwanja wa mpira.

Kwa kuwa wakati wa mvua ndio mujarabu kujua eneo zuri la kujenga viwanja vya mpira, viongozi watembelee maeneo mbalimbali ya jiji la Dar es Salaam na viunga vyake ili kujua maeneo yanayofaa kwa ujenzi wa viwanja vya michezo kwani hayatakuwa yamejaa au kuzungukwa na maji ya mvua.

*marobarnabas@yahoo.com*
*0784 334 096*

# Vijana wataka matatizo yageuzwe kuwa fursa

**Na Beatrice Moses**

BAADHI ya vijana waliokutana jijini Dar es Salaam kuhamasishana kuhusu uwekezaji, wamekubaliana kuyageuza matatizo yanayoikabili jamii kuwa fursa.

Wameyataja baadhi ya matatizo hayo kuwa ni upungufu wa damu kwa wajawazito, ukosefu wa maji safi na salama, uchafu wa mazingira na ukatili wa kijinsia.

Makubaliano ya kuzigeuza changamoto hizo kuwa fursa za ajira kwa vijana, yalifikiwa jana jijini Dar es Salaam baada ya vijana hao kupata semina elekezi ya wiki moja kuhusu ujasiriamali na hamasa katika uwekezaji iliyotolewa na Shirika la Action Aid, Global Platform.

George Bundi, mmoja wa washiriki wa semina hiyo, alisema wamebaini tabia ya kuchagua kazi za kufanya inawanyima fursa za kujipatia kipato, hivyo wamejipanga kuhakikisha matatizo yanayoikabili jamii wanayatumia kujiajiri.

"Mfano uzoaji wa taka, baadhi ya vijana tumekuwa tukiona kama vile kazi ya ovyo, lakini ni nzuri kwani licha ya kuweka mazingira yetu kuwa safi, pia kuna malipo ya fedha, hivyo tutapata kipato," Bundi alisema.

Shauri Yombayomba, akizungumzia changamoto ya upungufu wa ukosefu wa damu ambayo imekuwa ikiwakumba baadhi ya wajawazito na kuhatarisha maisha yao, alisema inaweza kugeuzwa kuwa fursa ya ajira kwa vijana.

"Nilishuhudia tatizo hilo kwa dada yangu, ilishuka hadi kufikia tano na alishauriwa kunywa maji ya matunda fulani, ndani ya wiki moja tu akafikisha kiwango cha damu kilichotakiwa, naamini vijana tunaweza kulima zao hilo kwa wingi maana nimebaini kuwa mahitaji ni makubwa," alisema.

Meneja wa Programu wa shirika lisilokuwa la kiserikali la Youth Partnership Countrywide (YPC) la Kibaha lililoandaa semina hiyo, Janeth Mulungi, alisema imewasaidia vijana walioshiriki kubadili fikra zao na kuona fursa za uwekezaji kwenye matatizo yanayoikabili jamii.

"Kumekuwa na changamoto kadhaa zinazosumbua kwenye jamii, vijana wamefuzwa kuzitambua na kuzitumia kama fursa za ajira kwa kutokusubiri kuajiriwa au kushinda wakilalamika," alisema.

Mwezeshaji Teresiah Warui wa Action Aid kutoka Kenya, alisema vijana wakibadili fikra, wanaweza kunufaika kupitia ujasiriamali na kujitegenezea kipato chenye uhakika.

"Wanapaswa kukaa pamoja na kuangalia ufumbuzi wa matatizo yanayowakabili na jinsi gani wanaweza kuyatatua na kujipatia kipato na kusaidia jamii husika," alisema.



Meneja wa Benki ya Biashara ya Mkombozi tawi la Kariakoo, Bonphace Mahenge (kushoto), akimwangalia Fatuma Rashid (katikati), mke wa Salim Rashid (hayupo pichani), wakati akisaini fomu ili kufungua akaunti ya pamoja (Joint Akaunti), jijini Dar es Salaam juzi, baada ya benki hiyo kutoa msaada wa sh. milioni moja kwa mume wake anayesumbuliwa na saratani ili taasisi mbalimbali ziweze kumsaidia kwa matibabu yake. **NA MPIGAPICHA WETU**

## Askari polisi wapata ajali

**Na Steven William,** MUHEZA

ASKARI wawili wa kituo kikuu cha Polisi wilayani Muheza, mkoani Tanga, wamepata ajali mbaya baada ya kugongwa na gari ndogo na kulazwa hospitalini.

Tukio hilo lilitokea juzi jioni katika eneo la Kwavangirisasi wilayani hapa baada ya pikipiki waliyokuwa wamepanda kugongwa na gari hilo.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tanga, Edward Bukombe, alisema askari hao, Konstebo Faraji na Konstabo Jafari, walikuwa katika pikipiki hiyo katika barabara kuu ya lami ya kutoka Muheza mjini kwenda Tanga mjini.

Alisema askari hao waligongwa na gari hilo na kuumia vibaya na kupoteza fahamu. Alisema kwa sasa askari hao wamelazwa katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa ya Bombo kwa matibabu na kwamba hali zao zinaendelea vizuri.

Bukombe alisema uchunguzi wa awali umebaini kuwa askari hao wameumia sehemu mbalimbali za mwili ikiwamo kuvunjika mifupa na kwamba dereva wa gari lililosababisha ajali hiyo amekamatwa na yuko chini ya ulinzi wa jeshi hilo.

Kutokana na hali hiyo, Mkuu wa Polisi wa Wilaya ya Muheza, Cosmas Maziwa, Mkuu wa Upelelezi Wilaya ya Muheza, Jonas Sira, na Mkuu wa Upelelezi Wilaya ya Tanga, Oscar Joshua, walifika kwenye eneo la tukio na kusimamia kuhakikisha Faraji na Jafari wanafikishwa hospitalini kwa huduma za matibabu.

## Mzee baraza anusurika kifungo kupokea rushwa

**Na Paul William,** MOSHI

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Mkoani Kilimanjaro imemhukumu kifungo cha miaka mitatu jela au kulipa faini ya Sh. Milioni moja aliyekuwa mzee mshauri wa mahakama ya Mwanzo Marangu, Godfrey Nyaki, baada ya kupatikana na hatia ya kuomba na kupokea rushwa ya Sh. 120,000.

Kesi hiyo iliyokuwa ikisikilizwa mbele ya Hakimu Mfawidhi Benezitha Maziku, mshtakiwa alidaiwa kuomba na kupokea rushwa kinyume na kifungu cha 15 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na. 11 ya mwaka 2007.

Mshitakiwa huyo alikana makosa yake na mahakama ilipanga kesi hiyo kutajwa juzi na mshitakiwa aliomba kukumbushiwa mashtaka yanayomkabili, ndipo Mwendesha Mashitaka wa Takukuru, Samuel Gabriel, alipofanya hivyo.

Baada ya kukumbushwa makosa yake, mshtakiwa huyo alikiri kuomba na kupokea rushwa hiyo ili kumsaidia mshtakiwa wa kesi ya jinai iliyokuwa ikisikilizwa katika mahakama ya Mwanzo Marangu.

Baada ya kukiri kosa hilo, Hakimu Maziku alimhukumu kutumikia kifungo cha miaka mitatu jela au kulipa faini ya Sh. 500,000 kwa kila kosa na hatimaye kulipa faini hiyo, hivyo kuepuka kwenda jela.

# Walia ujenzi wa zahanati kusuasua

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WANANCHI wa Kijiji cha Manyada, wilayani Shinyanga, wamelalamika kutokamilika ujenzi wa zahanati kwa miaka saba sasa, hivyo kukosa huduma ya afya kuwa karibu.

Hatua hiyo wameeleza imechangia watu kutumia muda mwingi kufuata matibabu umbali mrefu na hata kupoteza maisha hasa kwa wajawazito.

Wananchi walipaza kilio hicho juzi mbele ya Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko, kwenye mkutano wa hadhara wa kusikiliza kero za wananchi na kuzitatua huku wakiomba ujenzi wa zahanati hiyo ukamilishwe na kuanza kufanya kazi ili kuokoa vifo hasa vitokanavyo na uzazi.

Kwa mujibu wa wananchi hao, walijenga zahanati hiyo kwa nguvu zao tangu Mwaka 2012 na kufikisha hatua ya linta, hivyo kuiomba serikali kukamilisha boma hilo hadi kuanza kutoa huduma.

Mmoja wa wananchi hao, Theresia Bundala, ambaye pia ni muuguzi wa afya ngazi ya jamii, alisema kutokana na kukosa huduma ya afya kuwa karibu, kumesababisha wajawazito kupoteza maisha wakati wa kujifungua kutokana na baadhi kujifungulia njiani na kumwaga damu nyingi.

"Tunaomba serikali itusaidie kukamilisha ujenzi wa zahanati yetu hii hapa kijijini ili itusaidie kuondokana na changamoto ya kufuata matibabu umbali mrefu takribani kilomita tano pamoja na kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi," alisema.

Kutokana na malalamiko hayo, Mboneko aliiagiza halmashauri hiyo ipange utaratibu wa kila robo ya mwaka iwe inatenga fedha kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa maboma ya zahanati, ambayo yamejengwa kwa nguvu za wananchi ili kuwaondolea adha hiyo.

Kaimu Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, Dk. Joseph Ngowi, alisema ili kukamilika kwa ujenzi wa zahanati hiyo kunahitajika Sh. milioni 40 ambazo si rahisi kupatikana lakini akaahidi kujenga vyumba vichache vya msingi ili ianze kufanya kazi.

# Serikali yaandaa mkakati haki jinai

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

SERIKALI imesema inaandaa mkakati wa miaka mitano utakaotekelezwa na Wizara ya Katiba na Sheria na taasisi mbalimbali katika maeneo yanayohitaji mfumo wa kuboresha haki jinai.

Waziri wa Katiba na Sheria, Balozi Dk. Augustine Mahiga, alisema hayo jana wakati akifungua kikao cha mawaziri, makatibu wakuu wa wizara na wakuu wa taasisi zinazounda jukwaa la haki jinai.

Mkutano huo unafanyika kujadili hitimisho la mchakato wa sekta ndogo ya mfumo wa haki za jinai, ulioanza Julai, mwaka huu.

Balozi Mahiga alisema mara ya mwisho kupitia mfumo huo na kufanyia uboreshaji ni takribani miaka 20 iliyopita, hivyo ni muhimu kupitia ili kuendana na wakati uliopo sasa.

Alisema baada ya mapitio ya mfumo huo, yatapitishwa na kujadili maeneo yaliyopendekezwa kuboreshwa ili kufanya mfumo huo kuwa rafiki kwa wadau wote wa haki jinai.

"Katika kipindi cha miezi miwili sasa wataalamu kutoka wizara na taasisi za serikali na asasi za kiraia wamekuwa wakichambua na kujadili masuala mbalimbali katika mfumo wa haki jinai ambayo wamekuwa kikwazo katika kushughulikia na kusimamia masuala ya jinai nchini," alisema Dk. Mahiga.

Alisema mfumo huo unahusisha mnyororo wa hatua mbalimbali zinazotolewa wakati wa kushughulikia uhalifu wa kuanzia katika ngazi ya kuzuia uhalifu, kutambua unapotokea ikiwamo kukamata wale wanaofanya uhalifu kutekeleza vitendo vya kihalifu, kushtakiwa mahakamani, kutoa adhabu kurekebisha tabia za wahalifu na kufuatilia mienendo wanapomaliza kutumikia adhabu.

Katika mnyonyoro huo, alisema mambo mbalimbali yamewekwa kisheria ya namna ya kushughulika na wahalifu na vyombo au taasisi mbalimbali za jukwaa la haki jinai, hivyo ni lazima kuboreshwa.

Naye Katibu wa Wizara ya Katiba na Sheria, Prof. Sifuni Mchome, alisema kikao hicho ni muhimu kwa sababu kina lenga kufanya majadiliano ya hitimisho la mchakato wa kuboresha sekta ndogo za mfumo wa haki jinai.

Kutokana na hali hiyo, alisema ni vyema wataalamu waliopo wakatumia nafasi hiyo kujadili mabadiliko hayo ili yalete tija na jamii kwa ujumla.

Ooo

# Mapacha walioungana watenganishwa

**Na Mary Geofrey**

WATOTO mapacha Asnisia na Melnes Benard, waliokuwa wameunga maeneo ya kifuani hadi kwenye nyonga, wamefanikiwa kutenganishwa Saudi Arabia na kurejea nchini salama.

Watoto hao waliorejea nchini jana, walifanyiwa upasuaji wa kuwatenganisha kwa saa 14, ukihusisha madaktari bingwa 35 katika Hospitali ya King Abdallah, Saudi Arabia.

Daktari Bingwa wa Upasuaji aliyesafiri na watoto hao, Dk. Zainab Bokhary, akizungumza na waandishi wa habari muda mfupi baada ya kutua katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere jijini Dar es Salaam, alisema walienda Saudi Arabia Julai 8, mwaka jana.

Alisema watoto hao ambao walizaliwa Bukoba, walianza kufanyiwa vipimo na uchunguzi na madaktari bingwa wa mifupa, plastiki na kibofu kwa sababu walikuwa wanatumia njia moja ya mkojo.

Alisema upasuaji wao ulifanyika kwa mafanikio makubwa na wanaendelea vizuri wakati wakisubiri kurudi tena Saudi Arabia kwa ajili ya uchunguzi zaidi.

Katibu Mkuu Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano Afrika Mashariki, Balozi Ramadhani Mwinyi, alisema mafanikio ya matibabu ya watoto hao yanatokana na ushirikiano uliopo baina ya Tanzania na Saudi Arabia.

"Saudi Arabia imekuwa ikishirikiana kwa karibu na Hospitali ya Taifa Muhimbili kwani wamekuwa wakitupa msaada wa mambo mbalimbali kuhusiana na matibabu hasa vifaa vya tiba," Balozi Mwinyi alisema.

Balozi wa Saudi Arabia nchini, Mohammed Almalik, alisema wamefurahi kuona watoto hao wametibiwa na kuwa na afya njema.

"Sisi kwa upande wetu tunashukuru kuona watoto wamerudi na afya njema kwa sababu inatia matumaini na uaminifu," Almalika alisema.

Watoto hao pia walipokewa na Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Elias Kwesi.



Kamishna Jenerali wa Magereza nchini, Phaustine Kasike, akiteta jambo na Kamishna Jenerali Mstaafu wa Magereza, John Casmir Minja, baada ya gwaride maalum la kuwaaga Makamishna wastaafu wa Jeshi hilo ambao wamestaafu utumishi wao jeshini kwa mujibu wa sheria, katika hafla iliyofanyika katika Viwanja vya Chuo cha Taaluma ya Urekebishaji Tanzania, Ukonga jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MAGEREZA**


## TANGAZO

1. Kampuni ya **MM integrated Steel Wills Ltd** inawatangazia wananchi kuwa siku ya Jumapili tarehe **01/09/2019** itapitisha gari lenye vipimo tofauti kutoka **Dar es Salaam kwenda Mboga (Lugoba)**, gari lenye namba za usajili **T 265 BQW/ T997 BSV.**
2. Gari lina vipimo vifuatavyo
   Urefu -16.0
   Upana -2.5
   Kimo -4.8
3. Njia itakayotumika ni barabara ya Bagamoyo hadi Msata-Mboga.

**Tunaomba radhi kwa usumbufu wowote utakaojitokeza.**


# Malaria yaitesa Kigoma

**Na Magreth Magosso Kigoma**

KIGOMA imetajwa kuwa miongoni mwa mikoa vinara kwa maambukizo ya malaria nchini, asilimia 24.4 ya watoto walio katika umri wa chini ya miaka mitano wakiwa ni waathirika wa ugonjwa huo.

Imeelezwa kuwa hali hiyo inatokana na elimu duni ya matumizi ya chandarua na dhana potofu ya kuishiwa nguvu za kiume kwa wanaotumia vyandarua vyenye dawa za kuua mbu.

Mratibu wa Malaria katika Hospitali ya Rufaa ya Maweni Kigoma, Dk. Godfrey Smart, alisema sehemu kubwa ya jamii inaugua ugonjwa huo mkoani humo.

Alibainisha kuwa 2017/18, kupitia huduma ya upimaji shuleni, ilibainika kuwa asilimia 38.14 ya wanafunzi, walikuwa na maambukizo ya malaria.

"Elimu inatolewa lakini maralia Kigoma ni shida. Kati ya watu 1,000, watu 260 huugua ugonjwa wa malaria na asilimia 30 ni wagonjwa kutoka katika kambi mtambuka tatu za kuhifadhi wakimbizi.

"Katika kipindi cha Januari hadi Machi mwaka huu, jumla ya watu 238,828 walikutwa na maambukizo na watu 72,850 ni wagonjwa kutoka kambi za wakimbizi," mratibu huyo alibainisha.

Alisema serikali kwa kushirikiana na wadau, ina mkakati wa kuangamiza mazalia ya mbu katika kambi za wakimbizi kwa nyumba zenye sifa ya kupuliziwa viuatilifu vya kuua mazalia ya mbu na zaidi ya kaya 200,000 zinatarajiwa kupuliziwa.

Alisema tayari wameanza kuandaa mazingira ya upuliziaji katika wilaya hatarishi za Kasulu, Kibondo na Kakonko na ugawaji wa vyandarua unafanyika kupitia shule za msingi na vituo vya kutolea huduma kwa wajawazito.

Alisema kila halmashauri itazindua upuliziaji ifikapo Oktoba mwaka huu ili kupunguza vifo vitokanavyo na ugonjwa huo.

Hata hivyo, alisema idadi ya vifo vitokanavyo na maambukizo ya malaria imeshuka, akibainisha kuwa mwaka 2016 vilikuwa 432, mwaka 2017 vifo 388, mwaka 2018 vifo 189 na katika kipindi cha Januari hadi Machi mwaka huu, kulikuwa na vifo 110 mkoani Kigoma.

# Wajipanga kukusanya bil. 6/- sekta ya madini

**Na Cynthia Mwilolezi,** MANYARA

MKOA wa kimadini Simanjiro umelenga kukusanya kodi ya serikali Sh. bilioni sita kupitia mrabaha wa madini mbalimbali yanayochimbwa kwenye eneo hilo kwa mwaka huu wa fedha.

Kaimu Ofisa Madini Mkazi wa Mkoa huo, Castro Maduwa, aliyasema jana katika mji mdogo wa Orkesumet wakati wa ufunguzi wa soko la madini ya vito uliofanywa na Mkuu wa Wilaya ya Simanjiro, Zephania Chaula.

Maduwa alisema kuwa baada ya serikali kuwapangia kukusanya kiasi hicho, wamejipanga ipasavyo kuhakikisha wanafanikisha hilo kupitia madini ya Tanzanite, rubi, green momarine, green gainet na mengineyo.

Alisema kwa mwaka wa fedha wa 2019/2020, watafanikisha kupatikana kwa kiasi hicho kupitia masoko mawili ya madini ya Orkesumet lililofunguliwa na la Mirerani linalotarajiwa kufunguliwa hivi karibuni.

**Kwa mwaka jana, walipangiwa kukusanya Sh. bilioni 1.5, lakini walivuka lengo kwa kukusanya Sh. bilioni 2.8.**

Alisema kwa mwaka jana, walipangiwa kukusanya Sh. bilioni 1.5, lakini walivuka lengo kwa kukusanya Sh. bilioni 2.8.

"Tunaendelea kuwapa elimu wananchi kuwa kodi ya mrabaha siyo nyingi, ni asilimia saba ya madini uliyonayo, mfano Sh. 100,000 unalipa Sh. 7,000, hiyo Sh. 93,000 iliyobaki ni yako," Maduwa alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Simanjiro (Chaula), akizungumza wakati akizindua soko hilo, aliwataka wafanyabiashara na wachimbaji wa madini kutumia soko hilo kuuza madini na kulipa kodi ya serikali.

"Hauwezi kuulizwa umeyatoa wapi madini uliyonayo kwa kuwa unafanyiwa tathmini na kukadiriwa bei kisha unauza na kulipa kodi ya serikali bila tatizo lolote na kufanya maendeleo yako binafsi," Chaula alisema.

Mwenyekiti wa Chama cha Wachimbaji Madini Mkoa wa Manyara (Marema), Justin Nyari, alimpongeza mkuu huyo wa wilaya na ofisi ya madini kwa kuhakikisha soko hilo linaanzishwa.

"Hongera sana kiongozi kwani umefanikiwa kutekeleza maagizo ya Rais John Magufuli ya kujenga masoko ya madini kila mahali ambako kunapatikana madini, mpe salamu zetu Mkuu wa Mkoa, Alexander Mnyeti na Rais Magufuli kwa kujali sekta ya madini," Nyari alisema.

Mchimbaji wa madini ya ruby kwenye machimbo ya Kitwai, Raphael Mollel, alisema wanashukuru kwa kupata soko hilo.

"Tunatamani mazingira mazuri huku Simanjiro kwa wanunuzi kwani wengi wao wana ofisi jijini Arusha na pia wanaofanya tathmini wawe wengi ili kupunguza muda wa siku saba wa kusubiri tathmini ifanyike," Mollel alisema.



Mkuu wa Wilaya ya Simanjiro, mkoani Manyara, Mhandisi Zephania Chaula, akizungumza na wadau wa maendeleo wa wilayani humo, juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

## Wakoshwa uwekezaji katika sekta ya utalii

**Na Cynthia Mwilolezi,** MANYARA

MIRADI yenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 100 imetekelezwa katika Kijiji cha Vilima Vitatu wilayani Babati mkoani Manyara kutokana na mchango wa sekta ya utalii.

Kijiji hicho ambacho kiko katika eneo la Hifadhi ya Jamii ya Wanyamapori ya Burunge, kimenufaika na misaada toka mwekezaji wa Kampuni ya Chemchem ambayo imewekeza katika utalii wa picha na hoteli.

Mwenyekiti wa kijiji hicho, Erasto Balela na Ofisa Mtendaji wa Serikali ya kijiji hicho, Husna Shaban, alisema misaada ambayo wameipata, imesaidia sekta ya elimu, afya, ajira na mikopo kwa vikundi vya wajasiriamali.

Balela alisema mwekezaji huyo na jumuiya wamesaidia ukarabati na ujenzi Shule ya Msingi Vilima Vitatu na Shule ya Msingi Mdori uliogharimu zaidi ya Sh. milioni 60.

"Mwekezaji amekuwa na mchango mkubwa katika maendeleo ya jamii ya vilima vitatu," alisema.

Ofisa Mtendaji wa kijiji hicho (Husna) alisema mwaka huu, jumuiya hiyo pia ametoa fedha kwa vikundi vitano vya kina mama.

"Mbali na misaada yote hiyo, pia wametoa basi kwa ajili ya kubeba wanafunzi wa sekondari ambao walikuwa wakitembea zaidi ya kilomita 10 kwenda shule," alisema.

Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Chemchem, Walter Pallangyo, alisema mwekezaji huyo pia ametoa madawati 100 kwa shule za msingi na sekondari.

Pallangyo alisema pia wanaendelea na mpango wa kuwasomesha wanafunzi kutoka kaya maskini katika vijiji 10.

**Mbali na misaada yote hiyo, pia wametoa basi kwa ajili ya kubeba wanafunzi wa sekondari ambao walikuwa wakitembea zaidi ya kilomita 10 kwenda shule.**

## Waitaka serikali kupeleka watumishi sekta ya afya

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WAKAZI wa kata za Mbulu, Karatu na Endabash wilayani Karatu mkoani Arusha wameiomba serikali kuongeza jitihada za kuajiri watumishi wa afya wakiwamo madaktari na wauguzi ili vituo vya afya vilivyokamilika vitoe huduma kwa ufanisi.

Ombi hilo lilitolewa jana wilayani Karatu na wananchi hao katika ziara ya siku tano ya Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Mrisho Gambo, anayekagua miradi ya sekta ya afya, miundombinu na umeme.

Mmoja kati ya wananchi hao, Lucas John, alisema vituo vipya vya afya na vingine vikipata wataalamu wa afya, vitaweza kutoa huduma bora za afya na kuleta ufanisi zaidi.

Alisema hivi sasa, serikali imesogeza huduma bora za afya kwao, lakini ni muhimu vifaa na upatikanaji wa dawa ukaimarika zaidi.

Mganga Mkuu wa Mkoa, Dk. Wedson Sichalwe, alisema kwa sasa, Mkoa wa Arusha umeshaanza kuchukua hatua za kukabiliana na upungufu wa wataalamu wa afya ili kutoa huduma bora za afya kwa wananchi kwenye maeneo mbalimbali.

Awali, Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Gambo, alibaini uwapo wa vifaa vingi vipya ambavyo bado havijaanza kutumika kutokana na kutokamilika kwa mifumo yake na kuagiza Bohari ya Dawa (MSD) kuhakikisha mifumo hiyo inaanza kufanya kazi mapema ili wananchi wapate huduma bora.

Mkuu wa Wilaya ya Karatu, Theresia Mahongo, alisema bado kuna mahitaji ya fedha kuendeleza ujenzi wa vituo hivyo vya afya.

Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, Prof. Abiud Kaswamila, alisema kwa mwaka huu, mamlaka hiyo imetenga Sh. milioni 100 kwa ajili kuboresha sekta ya afya.

"Lengo letu ni kuona wananchi wa maeneo haya wanapata huduma bora za afya na jirani na maeneo yao wanaoishi ili kuepuka matumizi makubwa ya nauli kufuata huduma hizo mbali na wanakoishi," alisema.

## Mawenzi kutoa elimu ya afya

**Na Paul William,** MOSHI

HOSPITALI ya Rufani ya Mkoa wa Kilimanjaro, Mawenzi, iko katika mpango wa kuwaelimisha wananchi kuruhusu pindi wanapofiwa na ndugu zao, marehemu hao watolewe baadhi ya viungo ili kuwekewa wagonjwa wenye uhitaji.

Hayo yalibainishwa na Mganga Mfawidhi wa Hospitali hiyo, Dk. Japhet Boniface, wakati wa ziara ya Kamati ya Siasa ya Chama Cha Mapindizi (CCM) ilipotembelea hospitali hiyo kukagua ujenzi wa jengo la mama na mtoto ikiwa ni utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi.

Dk. Boniface alisema mpango huo utakapoanza, utasaidia wananchi kuepuka kwenda nje ya nchi kuwekewa baadhi ya viungo kama figo kwa kuwa zitakuwa zikiwekwa katika hospitali nchini.

"Tunataka kuanzisha mpango maalum wa kuwaelimisha wananchi kuruhusu pindi ndugu zao wanapofariki dunia, tutoe baadhi ya viungo kwa ajili ya kuwawekea watu wengine wenye uhitaji wa viungo hivyo," alisema Dk. Boniface.

Akizungumzia suala la ujenzi wa jengo hilo la mama na mtoto, Dk. Boniface alisema jengo hilo la ghorofa tatu linatarajiwa kuigharimu serikali Sh. bilioni 12 hadi kukamilika pamoja na vifaa vyake.

Alisema mpaka sasa Sh. bilioni 4.7 zimeshatumika katika ujenzi na kwamba fedha hizo ni ruzuku ya serikali huku pia akibainisha kuwa hospitali hiyo ambayo ni pekee Kanda ya Kaskazini inayohudumia wagonjwa wa akili, inakabiliwa na ukosefu wa daktari bingwa wa magonjwa hayo.

Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Kilimanjaro, Patrick Boisafi, alishangazwa na kitendo cha kusimamishwa kwa ujenzi wa jengo hilo la mama na mtoto huku fedha za kuendelea na kazi hiyo zikiwa zimeshatolewa na serikali.

"Tukiwa wasimamizi wa ilani, haturidhishwi kuona fedha za kuendeleza ujenzi huu zimeshatolewa na serikali lakini ujenzi umesimama hivyo niiombe Wizara ya Afya kwa kushirikiana na mkandarasi wa ujenzi huu ambaye na Wakala wa Majengo (TBA) kuhakikisha ujenzi huu unaendelea ili kuwanufaisha wananchi" alisema Boisafi.

Mwenyekiti huyo alisema kukamilika kwa jengo hilo kutapunguza idadi ya wagonjwa wanaopelekwa katika Hospitali ya Rufani ya Kanda ya KCMC kutokana na baadhi ya huduma muhimu za mama na mtoto kutolewa katika hospitali ya Mawenzi.

Aidha Boisafi aliutaka uongozi wa hospitali hiyo kubuni michoro ya kujenga majengo yake kwenda juu kutokana na eneo la hospitali hiyo kuwa dogo na kuwataka kuanza na jengo la dharura ambapo serikali imeshatoa fedha kwa ajili ya jengo hilo.

# Operesheni TRA yaibua madudu

**Mary Mosha na Paul William,** ROMBO

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA) Mkoa wa Kilimanjaro, imefanya operesheni maalum ya siku sita katika eneo la Tarakea wilayani Rombo kwa lengo la kuwatembelea walipakodi kwenye maeneo yao ya biashara na kusikiliza changamoto zao katika ulipaji kodi.

Meneja wa TRA Mkoa wa Kilimanjaro, Gabriel Mwangosi, alisema hayo alipozungumza na waandishi wa habari ofisini kwake kwamba operesheni hiyo maalum iliyopewa jina la 'mtaa kwa mtaa', ilikuwa na lengo la kutoa elimu kwa walipakodi.

Mwangosi alisema operesheni hiyo ilianza kwa kuwakusanya wafanyabiashara wote wilayani Rombo na kutoa semina na kisha kufuatiwa na ziara katika maeneo ya wafanyabiashara.

Alisema maofisa hao wa TRA walitembelea maduka ya jumla na rejareja, hoteli, viwanda vya kupasua mbao na baa na kubaini uwapo wa pombe zinazouzwa ambazo hazina stika ya TRA.

"Vipo baadhi ya vinywaji ambavyo ni pombe zimekuwa zikiuzwa kwa wateja lakini hazina stika ya TRA. Tumevikamata na tunaendelea kuwasiliana na TRA Mkoa wa Ilala ili msambazaji na mmiliki wa vinywaji hivyo achukuliwe hatua za kisheria kutokana na kusambaza vinywaji visivyo na stika," alisema Mwangosi.

Meneja huyo alisema changamoto nyingine waliyoibaini ni walipakodi kutumia udanganyifu katika matumizi ya risiti za mashine (EFD) na wale wote waliobainika kufanya hivyo walichukuliwa hatua ikiwamo kulipa faini.

Katika operesheni hiyo, pia alisema walibaini uwapo wa wateja waliojisajili katika kodi ongezeko la thamani (VAT) lakini wamekuwa hawalipi na kwamba baada ya kuwabaini wanaendelea kukokotoa ili wateja hao walipe kodi halali.

Pia alisema waliwabaini wateja wapya na kuwasajili katika VAT na kudai kuwa operesheni hiyo itakuwa na mwendelezo ili kuhakikisha wafanyabiashara wote wanalipa kodi stahiki ya serikali bila kuonewa.

Mmoja wa wafanyabiashara katika wilaya ya Rombo, Elisante Mrema, alisema uwapo wa operesheni hiyo utasaidia kubaini baadhi ya wafanyabiashara wasio waadilifu ambao wanakwepa kodi.

"Tunaomba opereshani hii iwe endelevu na ipite mtaa kwa mtaa kwani wako wanaokwepa kodi kwa makusudi na baadhi yao hawana elimu ya kutosha juu ya ulipaji wa kodi na viwango wanavyopaswa kulipa kwa kila mtu kulingana na mtaji wake," alisema Mrema.

Erieti Kimario, kwa upande wake, aliwataka maofisa kutoka TRA kupita mtaa kwa mtaa kutoa elimu juu ya namna ambavyo wafanyabiashara wanapaswa kulipa mapato kwa hiari na kueleza umuhimu wa ulipaji huo kwa wakati kwa manufaa yao na taifa.



Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kilimanjaro, Hamisi Issah, akionyesha juzi, moja ya magari ya wizi yaliyoibwa nchini Kenya na kukamatwa mkoani humo. Jeshi hilo limekamata magari 20 ya aina tofauti yaliyoibwa kutoka nchini Kenya na kuingizwa nchini katika kipindi cha mwaka 2018/19, katika maeneo ya mpakani hasa mpaka wa Tarakea wilayani Rombo na kuwekwa namba bandia za usajili. **PICHA: JAMES LANKA**

# Wataka wataalamu kilimo ili kuongeza tija

**Na Mary Mosha,** HAI

WAKULIMA wa skimu ya Mtamba, wilayani Hai, wameiomba serikali kupeleka wataalamu wa udongo ili kuwawezesha kulima kwa tija badala ya kuendelea kufanya shughuli hiyo kwa mazoea.

Kufahamu udongo huo kunaweza kusaidia kufahamu ni aina gani ya chakula wanayoweza kuipanda na kutumia mbolea kiasi gani na aina gani ili kuzalisha mazao yenye tija.


Wakizungunza na Nipashe kwa nyakati tofauti, wananchi wa vijiji vitatu vilivyoko ndani ya skimu hiyo, Noel Mwalimu na Fatma Ali, walisema licha ya kuwapo kwa vyanzo vya maji vya kutosha, bado wakulima hawawezi kulima kwa tija kutokana na kutojua udongo tunaoufanyia kazi unahitaji rutuba gani.

"Kwa sasa tunalima kwa mazoea bila kufahamu ni mbolea gani iweko na badala yake tunaongeza mazao mbolea bila utaalamu wowote. Lakini ikiwa tutapewa elimu ya aina ya udongo na virutubisho ambavyo tunaweza kutumia, upatikanaji wa bidhaa unaweza kuongezeka na kuleta faida kwa mkulima mmoja mmoja na taifa kwa ujumla," alisema Fatma.

Naye Ofisa Kilimo na Umwagiliaji, John Chuwa, alisema halmashauri watalichukuwa na kushirikiana na mamlaka zingine za serikali katika kuhakikisha udongo huo umepimwa na wakulima wameshauriwa kitaalamu.

Kutokana na ombi hilo, Mhandisi Umwagiliaji Kanda ya Kilimanjaro, Saidi Ibrahim, alisema ni jukumu la umwagiliaji kufanya utafiti wa udongo katika skimu mbalimbali ili kuwasaidia wakulima wanaofanya kilimo maeneo hao.

"Tumepokea kilio chao, Tume ya Umwagiliaji Kanda ya Kilimanjaro, itatuma wataalamu wa udongo kufika katika eneo hilo na kuchukukua sampuli. Wataleta majibu mapema iwezekanavyo bila kukwamisha kilimo msimu unaofuata," alisema Mhandisi Ibrahim.



# Aagiza uhamasishaji watu kujiunga CHF

**Na Peter Mkwavila,**
CHAMWINO

MKUU wa Wilaya ya Chamwino mkoani Dodoma, Vumilia Nyamoga, amewataka watendaji wa wilaya hiyo kuwashawishi wananchi kujiunga na Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF) iliyoboreshwa.

Aliyasema hayo juzi wakati akizungumza kwenye kikao cha baraza la madiwani cha utekelezaji wa kipindi cha robo ya nne ya mwaka wa fedha 2018/2019.

Alisema wakihakikisha elimu hiyo inatolewa na kuandikisha wananchi wengi ambao watapata huduma na kuifikia nchi nzima.

Aidha, alisema kuwa malalamiko yatakayotolewa yatapatiwa majibu mahali popote.

"Wakishiriki kikamilifu itaondoa kingungumizi cha malalamiko kutoka kwa wananchi ya kutopata huduma hiyo ya mfuko wa afya ya jamii (CHF) iliyoboreshwa"alisema.

**"Ninawaomba madiwani pamoja na watendaji hakikisheni mnasimamia miradi ili halmashauri yetu mapato yake yaweze kuongezeka kwa kupitia vyanzo hivyo vya miradi"alisema.**

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Chamwino, Athumani Masasi, aliwataka madiwani kusimamia vyanzo vya mapato ikiwamo miradi ili pato liongezeke.

Alisema ili halmashauri hiyo iweze kupanda kiuchumi watendaji wanatakiwa kusimamia na kukamilisha miradi yote ili ihudumie wananchi kwa ajili ya maendeleo.

"Ninawaomba madiwani pamoja na watendaji hakikisheni mnasimamia miradi ili halmashauri yetu mapato yake yaweze kuongezeka kwa kupitia vyanzo hivyo vya miradi"alisema.

Mwenyekiti wa halmashauri hiyo, Samweli Kaweya, amewataka watumishi kuwa na ushirikiano ili waweze kutatua changamoto zinazowakabili wananchi kwa ajili ya maendeleo yao. Alisema ushirikiano huo ukiwapo halmashauri itakuwa imefanikiwa kwenye maendeleo yake ya kiuchumi.



Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino, Mkoa wa Dodoma, wakimsikiliza Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Athumani Masasi (hayuko pichani), alipokuwa akijibu hoja mbalimbali kwenye kikao cha robo mwaka wa fedha 2018/19 kilichofanyika, jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Balozi ahoji sababu za unyanyasaji kutokomeshwa

**Na Renatha Msungu,**
MPWAPWA

NAIBU Balozi na Mkuu wa Ushirikiano wa Maendeleo kutoka Ubalozi wa Ireland nchini, Broggh Carr, amehoji sababu za vitendo vya ukatili wa kijinsia kuendelea nchini.

Alisema hayo akizungumza na wadau wakati wa ziara ya asasi ya kiraia, utawala wa sheria nchini Ireland. Ziara hiyo ilifanywa kwa kutembelea Shirika la Jukwaa la Utu wa Mtoto (CDF) lililopo Wilaya ya Mpwapwa mkoani Dodoma ili kujionea shughuli inazozifanya sanjari na kufahamu mipango yake.

Naibu Balozi huyo alisema kuna haja ya kuendeleza mikakati iliyowekwa katika kutokomeza ukatili wa kijinsia nchini.

Hata hivyo, alishangazwa na vitendo vya ukatili wa kijinsia vikiendelea siku hadi siku na kuhoji sababu za kutotokomezwa ukatili huo.

Pamoja na kushangazwa alihoji nini kinafanyika kwa wale wanaotendewa ukatili huo.

"Kuna mambo ya kujiuliza nini sababu ya kuendelea kwa ukatili wa kijinsia nchini wakati kuna mikakati mingi ambayo imewekwa ili kuzuia ukatili? Na nini kinafanyika kwa wale wanaotendewa uovu huo kwa kuwa masuala ya ukatili yanaathiri jamii.

Alitaka kuwe na mikakati madhubuti ili kukabiliana na hali hiyo ambayo huenda inazidi kuota mizizi, alisema Carr.

Lengo la ziara hiyo katika halmashauri ya wilaya ya Mpwapwa ni pamoja na kuangalia utekelezaji wa kukabiliana na ukatili dhidi ya wanawake na watoto kama sehemu ya utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Kitaifa wa Kukabiliana na Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto(Mtakuwwa).

Mkuu wa Wilaya ya Mpwapwa, Jabir Shekimweri, alisema wilaya hiyo yenye kata 33 na vijiji 113 imekuwa na matukio ya unyanyasaji wa kijinsia kwa wanawake na watoto ambapo takwimu zinaonyesha kati ya Januari hadi Juni 2018 jumla ya kesi 275 za ukatili ziliripotiwa katika dawati la kijinsia.

Alisema mwaka 2018 wanafunzi wa sekondari 566 kati ya 10,224 waliacha shule huku 44 kati yao wakiwa na ujauzito.

Shekimweri alisema kati ya Aprili hadi Juni 2019 kesi 193 za ukatili dhidi ya wanawake na watoto ziliripotiwa kwenye vituo vya huduma za afya.

Mkuu huyo wa wilaya alisema kumekuwa na changamoto ya baadhi ya familia kutaka mashauri ya ukatili yasipelekwe mahakamani bali yamalizwe kifamilia jambo ambalo linapelekea matukio hayo kuendelea kuwapo. Aidha, alibainisha kuwa kuna mkakati wa kuanzisha vituo vya 'one stop center' ili kushughulikia waathirika wa matendo ya ukatili ikiwamo ubakaji.

Kwa upande wake Mkuu wa Utekelezaji Miradi wa CDF, Evance Rwamuhuru, alisema shirika hilo lilianza kazi wilayani humo mwaka 2017, ambapo wanafanya kazi katika Kata nne za Mpwapwa mjini, Kibakwe, Berege na Pwaga.

Alisema wamefanikiwa kuwajengea uwezo wasichana 324 walio shuleni na walio nje ya shule na kuongeza kuwa wana mradi wa kushirikisha wanaume na wavulana kuacha ukatili dhidi ya wanawake na watoto ili kutokomeza mimba za utotoni.

Alifafanua zaidi kuwa kunakuwa na ugumu kutokana na wazazi na walezi kutotoa ushirikiano kwa vyombo vya sheria na badala yake huamua kumalizana na waliowapa mimba watoto wao na kuendelea kuwapa kiburi wahusika.

Ujumbe uliotembelea ulijumuisha Jaji Aillen Donelley wa Mahakama kuu ya Ireland, Mary Rose Gearty, mwendesha mashtaka nchini Ireland na Kate Mulkerrins, Mkuu wa Idara ya sheria katika Jeshi la Polisi Ireland,ambao waliambatana na Mkurugenzi Mtendaji wa Chama cha Wanawake katika Sheria na Maendeleo Afrika tawi la Tanzania (WiLDAF), Anna Kulaya.

# Elimu jumuishi kufikia 1,000

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

MRADI wa Elimu Jumuishi jijini Dodoma, umepanga kufikia watoto wanaoishi na ulemavu 1,000 hadi ifikapo 2021 katika shule zilizopo wilaya za Dodoma na Chamwino.

Hayo yalielezwa juzi na Meneja Mradi wa Elimu Jumuishi jijini Dodoma kutoka Tanzania Foundation Cheshire, Menance Mhombwe, wakati wa semina ya kujadili jinsi ya uendeshaji elimu hiyo hapa nchini.

Mhombwe alisema moja ya lengo waliojiwekea katika mradi huo, ni kuhakikisha wanawafikia watoto hao ambao nao wanahitaji kupata huduma ya elimu kama ilivyo jamii nyingine.

Alisema hivi sasa ambao wanapata elimu hiyo kupitia mradi huo ni 625 kutoka shule 20 zilizopo katika Wilaya hizo mbili za jijini hapa.

"Tumejipanga kuhakikisha ifikapo 2021 tunafikia idadi hiyo katika utoaji wa huduma ya elimu jumuishi lengo ni kuona kila mmoja mwenye ulemavu anafikiwa na idadi hiyo," alisema Mhombwe.§

Alieleza kuwa elimu jumuishi kwa watoto wenye uhitaji huo ni muhimu kwa sababu itawasaidia kujua vitu vingi ikiwamo kupata msaada wakiwa pamoja na wanafunzi wenzao.

Alifafanua zaidi ya kuwa lengo lao ni kuona kila mtoto anapata haki ya msingi ya elimu inayokusudiwa kutolewa kwa jamii ujumla.

Mwenyekiti wa Bodi wa TCF, Steven Masangia, alisema elimu hiyo ni muhimu kwa vijana hawa ambao ni taifa la leo katika ujenzi wa uchumi wa viwanda.

Alisema elimu hiyo jumuishi ni muhimu na kuwataka wazazi kuacha kuwaficha watoto na badala yake watoe taarifa ili waweze kufikiwa na elimu hiyo ambayo itawasaidia kuendesha maisha yao.

"Hakuna sababu ya kuwaachicha watoto majumbani mnatakiwa kutoa ushirikiano pale wanapokuwa wanahitaji idadi," alisema Masangia.

Aliwaeleza kuwa watoto hao ni sawa na wengine kwa hiyo kupata elimu ni haki yao ya msingi.



# Mkutano wabunge Madola kuanza Jumatatu Z'bar

**Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Ali Muhamed Shein, keshokutwa Jumatatu, anatarajiwa kufungua mkutano wa 50 wa Chama cha Mabunge wa Jumuiya ya Madola Kanda ya Afrika (CPA) utakaofanyika mjini Zanzibar.

Akizungumza na wanahabari kuhusu maandalizi ya mkutano huo, Spika wa Baraza la Wawakilishi, Zubeir Ali Maulid, alisema kufanyika kwa mkutano huo Zanzibar ni fursa nzuri kwa Wazanzibari na Tanzania kujitangaza katika maeneo mbalimbali ya kiuchumi na kiuwekezaji.

Alisema, maeneo hayo ni pamoja na utalii, biashara, diplomasia na uwekezaji, ambazo ni sehemu muhimu za kiuchumi.

Alisema, fursa hiyo inatokana na ugeni huo wa mataifa zaidi ya 18 ambao wana ushawishi mkubwa katika masuala hayo ya kiuwekezaji, biashara na utalii katika nchi zao.

"Kuwapo kwa siku tano nchini kwetu ni wakati adhimu kwa ugeni huu kuona mandhari nzuri ya Zanzibar na Tanzania kwa ujumla kwani tuna vivutio mbalimbali vya utalii vilivyopo nchini na sera na vivutio vya biashara na uwekezaji," alisema Maulid.

**"Kuwapo kwa siku tano nchini kwetu ni wakati adhimu kwa ugeni huu kuona mandhari nzuri ya Zanzibar na Tanzania kwa ujumla kwani tuna vivutio mbalimbali vya utalii vilivyopo nchini na sera na vivutio vya biashara na uwekezaji," alisema Maulid.**

Spika huyo alieleza kuwa, wageni hao watakuwa mabalozi wazuri katika kutangaza utalii na kupeleka sifa ya visiwa vya Zanzibar ikiwemo mandhari mazuri.

Alisema kuwa, mkutano huo ni muhimu kwani utawaweka pamoja Maspika, Naibu Spika na wabunge zaidi ya 400 kutoka nchi mbalimbali za Afrika.

Mwenyekiti wa kamati tendaji wa wabunge wa Jumuiya ya Madola (CPA) kutoka Zanzibar, Simai Mohamed Said, alisema mkutano huo ni fursa nyingine ya kuitangaza Jamhuri ya Muungano pamoja na Zanzibar katika sekta ya utalii na uwekezaji.

"Hii ni fursa nyingine ya kupokea idadi kubwa ya wageni ambapo safari hii watatembelea Zanzibar na kujionea vivutio vilivyopo pamoja na ukarimu wa wananchi wetu"alisema.

Katika mkutano huo Tanzania ambayo ndiyo makao makuu ya (CPA) kanda ya Afrika itatumia fursa hiyo kuwashawishi wajumbe kuridhia kuwa sehemu ya kuwekeza katika ujenzi wa hoteli ya nyota tano katika makao makuu ya mji huko Dodoma.

Baadhi ya nchi zitakazoshiriki mkutano huo ni Zambia, Ghana, Malawi, Nigeria, Cameroon, Afrika Kusini, Uganda pamoja na wenyeji Tanzania.



Spika wa Bunge la Lesotho, Sephiri Enoch Motanyane (kulia), akiwasili katika Uwanja wa Ndege wa Zanzibar jana, na kupokewa na Maofisa Itifaki wa Bunge la Tanzania, kwa ajili ya kushiriki Mkutano wa 50 wa Mabunge ya Nchi za Jumuiya ya Madola (CPA), Kanda ya Afrika utakaofanyika tarehe 30 Agosti hadi tarehe 5 Septemba mwaka huu katika Hoteli ya Madinat Al Bahr Business and Spa. **PICHA: BUNGE**

# Serikali yaonya kupuuza mitaala

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

TAASISI ya Elimu ya Zanzibar, imezionya baadhi ya shule zisizofuata mtaala ulio idhinishwa na serikali hali inayopelekea kukosekana usawa na mfanano katika utoaji elimu.

Akiwasilisha taarifa ya taasisi hiyo katika mkutano wa Kamati ya Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi, Mkurugenzi wake, Suleiman Yahya Ame, alisema kufanya hivyo ni kinyume na maelekezo ya Sera ya Elimu ya mwaka 2006. Alisema katika kipindi cha robo ya kwanza wamefuatilia matumizi ya vitabu na mitaala kwa elimu ya maandalizi na msingi kwa shule za serikali na binafsi ambapo shule 80 zilifikiwa.

Alisema kati ya shule hizo 44 ni za serikali na 36 za binafsi na ilibainika kuwa katika shule binafsi baadhi ya walimu wakuu hawaandiki maombi kwa Wizara ya Elimu Zanzibar kuomba vitabu hata kama shule husika ina upungufu wa vitabu.

Aidha, alieleza kuwa taasisi katika kipindi hiki inaendelea kudurusu mtaala wa elimu ya maandalizi na msingi kwa kushirikiana na washauri elekezi pamoja na wadau mbalimbali ambapo mtaala huo pia utazingatia mahitaji ya wenye mahitaji maalum ili kujenga taifa bora.

Wakati huo huo kamati hiyo ya Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi limepokea ripoti ya Ofisi ya Mrajisi wa Elimu Zanzibar, iliyosomwa na Mrajis Siajabu Suleiman Pandu, ilielezea kuwa kuna mafanikio makubwa.

Alisema wamesajili shule za umma, binafsi na vyuo pamoja na kukusanya fedha nyingi kutokana na usajili huo.

Alisema lakini bado wanakabiliwa na matatizo mbalimbali yakiwamo ufinyu wa nafasi ya ofisi na usafiri.

## ILO yakunwa na mafanikio

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SHIRIKA la Kazi Duniani (ILO) limeeleza kufurahishwa na utekelezaji wa programu ya mafunzo kazi (apprenticeship) yaliyotolewa kwa vijana wa Zanzibar.

Mafunzo hayo kwa vijana wa Zanzibar yalikuwa kwenye ajira za hotelini na sekta ya utalii kwa ujumla.

Msimamizi Mkuu wa mradi wa mafunzo kazi kutoka shirika hilo Kanda ya Mashariki na Kusini mwa Afrika Laura Brewer, alieleza kuwa mafanikio hayo ni kielelezo kwamba serikali imedhamiria kwa dhati kulipatia ufumbuzi tatizo la uhaba wa ajira.

Aliahidi ILO itaendelea kushirikiana na serikali kwa kutoa mafunzo na misaada mingine inayohitajika ili vijana waweze kukubalika katika soko la ajira kwenye sekta ya utalii na nyinginezo.

Akizungumza na uongozi wa Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto huko Mwanakwerekwe, Brewer aliyekuja nchini kuona namna Zanzibar ilivyofanya vizuri kulinganisha na nchi nyingine kutokana na programu hiyo iliyoanza Agosti 2017.

Alisema ILO imetiwa moyo na ushirikiano ulioonyeshwa na wamiliki wa hoteli za kitalii kwa kukubali kuwapa mazoezi vijana wanaoshiriki mafunzo hayo.

Alimhakikishia Katibu Mkuu wa wizara hiyo Fatma Gharib Bilal, kuwa ILO inaunga mkono fikra ya serikali kuunda sera itakayorasimisha programu ya mafunzo kwa vijana, na kuongeza kuwa iko tayari kutoa msaada utakaohitajika kwa ajili hiyo.

Akitoa shukrani za serikali kwa ILO, Katibu Mkuu wa Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto, Fatma Gharib Bilal, alisema angalau mradi huo umepunguza malalamiko kwamba ajira nyingi za sekta ya utalii zinahodhiwa na wageni kwa kile kinachodaiwa kuwa Wazanzibari wengi wanakosa elimu ya kutosha.

Alieleza kuwa, awamu ya kwanza iliyoanza mwezi Agosti 2017, ilishirikisha vijana 75 waliopita katika usaili, 52 kati yao walimaliza kwa mafanikio makubwa, na wengine 36 tayari wameajiriwa kwenye hoteli mbalimbali zikiwamo walizofanyia mafunzo kwa vitendo, huku baadhi wakiamua kujiendeleza katika ngazi za juu na wengine kujiajiri wenyewe.

Aidha, alisema, baada ya Zanzibar kufanya vizuri katika awamu hiyo ya majaribio, ILO imevutiwa na kuamua mkupuo wa pili unaoendelea sasa kutoa nafasi 120 badala ya 100 za awali kabla ya kufanyiwa usaili na mchujo.

Katibu Mkuu alieleza kuwa, wamiliki wa hoteli zilizochukua vijana hao wameonesha kufurahishwa kwa kuwa wamevuna nguvu kazi mpya kutokana na uwezo wa kujifunza ulioonesha na wahitimu na kwa hivyo katika awamu ya pili wameamua kupokea vijana wengi zaidi.



Soma UK. 14

## DUDUBAYA

Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT
BURUDANI TELE
JUMAMOSI AGOSTI 31, 2019



# MILIONI 100

## PROFESA JAY KABIPU, P FUNK KAMPIGIA

UK.16

BASI SAWA



## Watakaomtafuta Dudubaya Mungu anawaona

MSANII nguli wa Bongo Fleva, Godfrey Tumaini, maarufu kama Dudubaya, amesema tukio la kuokoka kwake limemfanya kusahau mambo mengi mabaya na kwamba atasimamia haki katika kuendeleza kipaji chake.

Dudu baya ambaye hivi karibuni alijisalimisha kwa Mchungaji Boniface Mwamposya na kuokoka, ameeleza kwamba hadi kufikia hatua hiyo amekuwa na safari ndefu katika muziki wa Bongo Fleva na yeye ndiye alikuwa mmoja wa waanzilishi wake.

"Uamuzi wa kuokoka nimeufanya baada ya kutafakari katika maisha yangu yote, mimi ndiye niliweka ramani ya bongo fleva wakati ule studio zote zilikuwa na teknolojia duni lakini mafanikio yake yamekuwa machache. Nimeona nijisalimishe kwa Mungu ili niwe na msamaha na kuanza upya maisha yangu," amesema Dudubaya.



## Kumbe mashabiki wanawabadilisha wasanii

RAPA Nikki Wa Pili amesema wasanii wanaweka taarifa za bandia kutokana na kutaka kukuza biashara zao na kulenga mashabiki wa kumuunga mkono.

Akizungumza sababu ya baadhi ya mastaa kuongopa umri wao, amesema suala hilo linatokana na wengi kutumia mitandao ya kijamii na idadi kubwa ya watumiaji ni rika la kati na kushuka chini.

"Watu wanaangalia nani unawasiana naye na umri gani, nadhani hiyo ni sababu tosha kwa baadhi ya wasanii kudanganya ili kukuza soko lake na kutaka kukubalika na jamii inayomtazama kwa muda huo," amesema Nikki Wa Pili.



# THE MAFIC HAKUNA KULALA

MENEJA wa kundi la muziki la The Mafic, Ruksana, amesema pamoja na kumpoteza mwanamuziki wake Mbalamwezi, kazi ya kukuza muziki itabaki palepale.

Amesema wakati bado hujafika kuamua kama nafasi aliyoacha mwanamuziki huyo katika kifo chenye utata itazibwa au hapana kutokana na tukio hilo kiwasumbua vichwa.


"Pamoja na kupata msiba mzito, lakini kila kitu kitabaki paleplae na kazi zitaendelea. Kuhusu nani ataziba nafasi ya Mbalamwezi bado ni muda mfupi sana na sisi kama tuliokuwa tunafanya kazi naye tuna kumbukumbu nyingi kichwani, mapema sana kufanya jambo hilo," amesema Ruksana.

## INSTA-TWITTER





**Sichagui** kambi bia yoyote nakanyaga-**Pierre Liquid.**



**Jitahidi** sana usimuumize mtu kwa makusudi kwasababu kile unachomtendea kuna siku kitakurudia-**Nyamayao.**



## Wakazi kweli hata ukivaa ngozi unapata mkwanja?

MWANAMUZIKI wa HipHop Wakazi, ameeleza kwamba unadhifu wa mavazi sio sababu ya msanii kuwa kutengeneza pesa.

Akizungumza kupitia EATV na EA Radio, amesema kana unatengeneza kazi nzuri inayokubalika na watu wengi hata ukivaa nguo za ngozi kazi zao zitauzika na kukupa kipato kizuri.

“Mionekano ipo ya aina mbalimbali, kumbuka hata Mrisho Mpoto kuwa pekupeku ndiyo kuna muingizia pesa, kuna muda tusilazimishe kwamba muonekano ndiyo unakuingizia pesa kwa sababu kama Mwana HipHop unaweza kijitengenezea njia zako zingine na bado ukapata pesa”, amesema.




@burudanitele

>>> Usikose Jarida hili la Burudani Tele (BT) ndani ya Gazeti lako la Nipashe kila Jumamosi, pia lipo kwenye mtandao wa kijamii Twitter, tu' follow

## UNASEMAAA...



# SAUTI SOUL wao kama kumbikumbi

WANAMUZIKI wa kundi la Sauti Soul kutoka Kenya, wamesema kuvumiliana na kujitambua ni vigezo vyao vya kubaki kuwa imara kwa miaka mingi.

Wakiongea hivi Karibuni wasanii hao wamesema kwamba ndani ya kundi hilo kila mtu yupo sawa na mwingine na pale kunapotokea kutofautiana wanakaa chini kutafuta ufumbuzi.

“Kila mtu anajitambua, anamvumilia mwenziye kwani wote ni watu wazima tunajua umuhimu wa kuwa pamoja na ndio maana tunasema ukitaka kwenda haraka kuwa peke yako, lakini ukitaka mafanikio ya muda mrefu tembea na mwenzako,” amesema msanii mmoja.

## INSTA-TWITTER

Tuffolow/ Tu-tag
@burudanitele



**Ukipanda** uovu utavuna uovu, ukipanda mema juwa utavuna mema. Huwezi kupanda mchicha uvune dagaa. Tukumbuke kutenda mema dunia sio ya kwetu-Jenifer **Kyaka Odama.**



**Nafanya** vile akili inanituma ili mradi nisivunje sheria-**Mheshimiwa Temba.**



**Hatulalagi** njaa ila tunachelewa tu kula-**Shetta.**

# Kuumbe!

# MILIONI 100

## PROFESA JAY KABIPU, P FUNK KAMPIGIA





WIKI hii imekumbwa na joto kali baada ya wakongwe wawili katika tasnia ya muziki kujikuta wakiwagawa mashabiki wao baada ya wawili hao kutupiana maneno makali katika mitandao ya kijamii.

Wakongwe hao, Profesa Jay ambaye pia ni Mbunge wa Mikumi na mtayarishaji wa muziki P Funk 'Majani' wapo katika mgogoro mzito kutokana na tuhuma ya malipo ya pesa ya mrahaba wa muziki kutoka nchini Uganda.

Mgogoro ambao uliibuka baada ya serikali kutangaza ilimsaidia Profesa Jay kupata kiasi cha Sh. milioni 100 kutoka Uganda baada ya wimbo wake kutumiwa na msanii mmoja.

Baada ya tangazo hilo, Profesa Jay aliibuka na kusema Cosata haikusema ukweli kwani mtu aliyelipwa ni P Funk na si yeye.

Mbunge huyo alikwenda mtandaoni na kuandika ujumbe ulionekana kujaa mihemuko na kuhitimishwa mchafuko ambao unazidi kupamba moto.

"COSOTA Mmekuja kwenye kikao cha kamati ya Bunge na kusema uwongo kwamba mmenisimamia mimi PROFESSOR JAY nikalipwa sh.Milioni 100 kutoka UGANDA, ukweli ni kwamba sijalipwa hata senti tano na pesa zote amelipwa P Funk chini ya usimamizi wenu. Wekeni vizuri hiyo kumbukumbu yenu"

Ujumbe huo umeonekana kumkerasa sana P Funk na hapo ndipo naye alikwenda katika ukurasa wake wa Instagram na kumjibu kwa ukali.

Pamoja na kukiri kupokea kiasi hichi cha fedha, P Funk amejikuta akizungumza maneno yake ya akiba na kueleza hata heshima kwake imefikia tamati.

Ujumbe wa P Funk ulikuwa ukisema "Hizi ni siasa Profesa Jay au? Mbunge kweli roho inakuuma nikipewa haki yangu?

Prodyuza huyo alianza kwa kuuliza maswali na kasha aliendelea "Kazi nibuni mimi, kesi nibebe mimi bila msaada wowote , msongo wa mawazo nibebe mimi kwa miaka mitatu, hakuna ubunifu wala sauti yako iliyotumika. Unataka nini kama sio ulafi? Au leo hii wewe ndiye P Funk uliotengeza muziki? Punguza tamaa kaka kwani kwa miaka 19 umeweza kufaidika kutokana na muziki wangu.

Hata hivyo, mtayarishaji huyo anayeheshimiwa na wasanii wengi alihitimisha kwa kusema kwamba Mungu atampa haki zake zote ambazo aliwanufaisha wanamuziki na kwamba alipowafikisha panatosha.

"Nilipowafikisha panatosha kabisa, heshima yangu kwako imefia hapa leo," alimalizia P Funk.

Jumbe zote mbili zilizoandikwa na majemedari hao wa muziki zimeleta hisia hasi kwa mashabiki wao na wengi wao wanaona ugomvi huo unaweza kusambaa zaidi kama hatua ya kuwakutanisha haitafanyika.



# WANAMUZIKI WALIOFARIKI NA KUZIKWA KENYA

**Na Adam Fungamwango**

HISTORIA ya muziki wa Tanzania inaonyesha kuwa mwanamuziki maarufu nchini Tanzania, Mbaraka Mwinsheshe aliyekuwa akipigia bendi ya Moro Jazz na baadaye kuanzisha bendi ya Super Volcano, alifariki dunia nchini Kenya Januari 12 1979.

Huyu anaingia kwenye orodha ya wanamuziki wa Kitanzania waliofariki dunia nchini humo.

Hata hivyo, Mbaraka alirejeshwa nchini Tanzania na kuzikwa kijiji cha Mzenga, mkoani Pwani, ingawa kwa asilimia kubwa makazi yake yalikuwa mkoani Morogoro.

Leo tunawazungumzia wanamuziki wa Kitanzania waliokwenda nchini Kenya kutafuta maisha, lakini kwa bahati mbaya umauti uliwafika huko na mbaya zaidi hawakupata bahati ya kurejeshwa kwenye ardhi ya baba na babu zao, badala yake kuzikwa huko huko ughaibuni kwa sababu mbalimbali.

**George Peter Kinyonga**

Ni mwimbaji, mtunzi, na mpiga magitaa yote ya solo, rhythm na bass. George na kaka yake Willson Peter Kinyonga waliibukia Hale mkoani Tanga kwenye bendi ya Jamhuri Jazz Band mwishoni mwa miaka ya '60 na mwanzoni mwa miaka ha '70. Walijiengua na kwenda kuunda Arusha Jazz Band iliyoingia nchini Kenya na kubadilisha jina kujiita Simba Wanyika.

George, alitunga na kuimba nyimbo nyingi na kaka yake zilizokuwa maarufu sana kama 'Naepuka', 'Njoo Tushirikiane', 'Dunia Haina Wema' na nyingine nyingi.

Aina ya uimbaji wa George ndiyo uliomuathiri TX Moshi William ambaye kwa kiasi kikubwa aliiga uimbaji wake. Alifariki dunia mwaka 1992 na kuzikwa nchini Kenya.

**Willson Peter Kinyonga**

Ni mtunzi, mwimbaji, mpiga gitaa la solo na kiongozi wa bendi ya Simba Wanyika. Ustaa wake ulianza kwenye bendi ya Jamhuri Jazz band ya Tanga, kabla ya kuunda Arusha Jazz Band na wenzake wakaingia nchini Kenya.

Akiwa na ndugu yake George waliiletea heshima kubwa Tanzania kutokana na nyimbo zao zilizopendwa na kuvuma Afrika Mashariki yote. Nyimbo kama 'Sofia', 'Pamela', 'Polepole', 'Halima' na nyingine nyingi ziliifanya bendi hiyo kupendwa na wengi. Alifariki dunia mwaka 1995 na kuzikwa nchini Kenya.

**John Ngereza**

Wimbo wa 'Afro', ni maarufu sana hapa nchini, ukipigwa na bendi nyingi kwenye kumbi na baa mbalimbali. Lakini wengi hawajui mtunzi wa wimbo huu.

John Ngereza, ndiye mtunzi wa wimbo huu akiwa na Les Wanyika. Ni mmoja wa Watanzania waliokwenda nchini Kenya kutafuta maisha na alifanikiwa kujiunga na bendi hiyo akiwa na kina Issa Juma, Profesa Omari na wengine.

Ni mwanamuziki maarufu sana nchini Kenya akiwa pia amepitia bendi mbalimbali za huko.

Alifariki dunia mwaka 2002 na kuzikwa nchini Kenya.

**Profesa Omari Shaaban**

Ukizisikiliza nyimbo za Simba Wanyika na Les Wanyika, kuna wakati gita la 'rhythm' linaachiwa na linasikika peke yake, likisindikizwa na drums, huku kuna sauti ikisikika 'Profesaaa Omari'.

Mtu huyo alikuwa mpira gita hilo la kati na kuufanya muziki wa Simba Wanyika na Les Wanyika kukubalika sana nchini Kenya.

Pamoja na kwamba alifundishwa muziki na kina Willson na George mjini Tanga na kwenda naye Kenya, lakini huyu ndiye alikuwa kinara wa kushawishi baadhi ya wanamuziki wa Simba Wanyika kujiungua na kwenda kuunda Les Wanyika, wakiwaacha ndugu hao na bendi yao.

Alifariki mwaka 1998 na kuzikwa nchini Kenya.

**Twahir Mohamed**

Inasemekana Tanzania haijapata mpuliza saxaphone kama Twahir Mohamed Twahir. Huyu alikuwa na uwezo na pumzi ya kupiga chombo hicho kuanzia mwanzo wa wimbo hadi mwisho.

Ukitaka kuthibitisha hilo sikiliza wimbo wa 'Mimi Msafiri' wa Orchestra Safari Sound ya mtindo wa Masantula.

Alipigia bendi mbalimbali nchini Tanzania, lakini alikwenda nchini Kenya kwenye bendi ya Simba Wanyika kuziba pengo la Liza Elias, Mtanzania aliyeamua kurejea nchini na kujiunga na Mwenge Jazz Band wakati huo.

Alipigia bendi mbalimbali nchini Kenya ikiwemo Virunga ya Samba Mapangala, kabla ya kufariki dunia 2004 nchini Kenya na kuzikwa kwenye makaburi ya Kibera



The two brothers in Holland after recording *Pepea*, August 1991.

# Vijimambo

1. Hii ndio inaitwa 'nikinywa maji, nakuona kwenye glasi' - Agatha Mbale, Moro Town.
2. Ai weeewe, naoomba - Ebby Mbwambo, Tanga.
3. Hahahaaa, endelea kuomba tu mzee baba, atakupa tu - Maunda Alawi,
4. Duuh, kweli utoto kazi! Kidume kinategemea kabisa kimegewe mkate! - Beneali Moussa, Zenji.
5. Naomba, ukinipa na mie nikinunuliwa soda nakupa - Mauwa Minde, Kibada Kigamboni DSM.
6. Lazima huyo dogo atakua wa Bush Stars, anaiomba picha mkate! - Sultani Ubwa, Kibada DSM.
7. Endelea tu kuomba, huyo siyo mchoyo atakumegea tu - Moussa Beneali, Migombani Zenji.
8. Kama ulikuwa hujui tafsiri halisi ya neno 'zwazwa', basi ndio hiyo - Beneali Moussa, Migombani Zenji.
9. Naenda kukusemea kwa mama yako umeomba mkate kwa watu ->Julius Anthony, Usagara Tanga.
10. Acha uchoyo wewe, mwenzio anakuomba ndio unaingiza wote mdomo! - Mama Nah, Manzese DSM.
11. Mwache na uchoyo wake, na wewe ukinunua vitu vyako usimpe - Rehema Bwahoja, Buguruni DSM.
12. Dogo utachubuka 'makongoro' kwa kupiga magoti, hiyo picha tuu - Subira Bwahoja, DSM.
13. Jamani, si mngemuambia kama hiyo ni picha tu sio mtu kweli. Ona sasa anavyotia huruma - Dule DSM.
14. Yes, hiyo ndio dawa ya ombaomba. Kesho leteni roli lenye picha ya hela - Kijusi, Magomeni Mapipa DSM.
15. Daaah, mjukuu wa 'Matonya' anadhalilika hivi hivi kwa picha tu - Kijusi, Magomeni Mapipa DSM.
16. Huyo naye kubwa zima hajajua tu picha na mtu wa ukweli? Muacha achune magoti - Kole, Msata Pwani.
17. Hapo atalifuata gari mpaka wapi kwa kupiga magoti hivyo Magdalena Kachenja, Mabwepande DSM.
18. Tatizo dogo hajafunguka, anataka mkate au anataka uchumba - Alli Shaaban Mpanjira, Mbagala Kuu DSM.
19. Kweli walimu wanakazi. Huyo mpaka aje kujua hiyo ni picha tu si atakua Chuo Kikuu! - Pili Mpanjira DSM.
20. Mmmh, mie mgeni hapa, acha nipite tu! - Abass Ngulunga, Msasani Macho, DSM.
21. We mtoto utagongwa na magari buree. Huyo sio mtu kweli ni picha tu - Bernad Isuja, Makore Dodoma.

**SMS Bomba ya Leo:**

**Tatizo dogo hajafunguka, anataka mkate au anataka uchumba -Alli Shaaban Mpanjira, Mbagala Kuu DSM.**

## PICHA MPYA




**TUMA MESEJI - 0773 477311**




# Mama Mkwe
# Waruka jivu, wakanyaga moto

**Na Adam Fungamwango**

HII filamu inaitwa 'Mama Mkwe'. Inazungumzia matatizo yanayojitokeza kwenye jamii, hasa za Kiafrika.

Mara nyingi familia za Kiafrika zina utamaduni wa kuishi kijamaa.

Mume na mke wanaweza kuishi na ndugu za pande zote mbili nyumbani kwao, wakati mwingine hata wazazi wao.

Hii ina uzuri wake. Lakini pia upande wa pili kunaweza kutokea tatizo, kama mmoja wa watu hao au baadhi yao wataamua kwa makusudi kutengeneza mazingira ya wengine kuonekana wabaya.

Hili limejitokeza ndani ya filamu hii na kuzua matatizo makubwa.

Imechezwa na waimbaji wa muziki wa Injili, kina Jennifer Mgendi na Bahati Bukuku.

Wengine ni Senga, Mussa Banzi, Godliver Minangi, Christina Matai na wengine wengi.

Banzi ameoa mke ambaye ni Jennifer aliyecheza kama Amisa kwenye filamu hiyo.

Hapo nyumbani kwake pia anaishi na mama yake mzazi, Bi Esta na dada yake Stella.

Amisa ni mke mwenye huruma, upendo, mnyenyekevu, akiwa pia ni mcha Mungu.

Hata hivyo mkwewe Bi Esta na wifi yake Stella si watu wazuri.

Hawampendi na wanapanga njama za kumtengenezea uongo ili kuivunja ndoa hiyo.

Kitendo cha Banzi kuacha kuwapa pesa za matumizi mama na dada yake kama ilivyokuwa awali kabla ya kuoa, kimewafanya kumchukia dada wa watu pasipo sababu ya maana.

Sababu nyingine ni kwamba tangu aolewe, hajamzalia mumewe mtoto.

Wanaweka hirizi chini ya kitanda cha Banzi na mkewe na wakati anaingia tu, anapokewa na maneno kutoka kwa mama yake kuwa huenda mkewe amemuwekea kitu kisicho cha kawaida ndani.

Na ushahidi wa hilo ameupata kwa mganga wake aliyemwambia kuwa kijana wake amewekewa na mkewe kitu kisicho cha kawaida ndani ambacho kinafanana na uchawi, na lengo ni kumdhuru.

Baada ya kusaka kila kona, anakutana na hirizi chini ya kitanda.

Banzi anaanza kuondoa uaminifu kwa mkewe. Pamoja na kujitetea, lakini haisaidii kitu.

Stella, dada yake Banzi anamlipa kijana mmoja pesa kwa kazi moja tu. Kijana huyo anafika nyumbani hapo mbele ya Banzi, mkewe, mama na dada yake na kudai kuwa amemfuata mpenzi wake Amisa.

Akadai Amisa ni mpenzi wake tangu zamani na wamekuwa na uhusiano hata baada ya kuolewa. Hilo lilitosha kabisa mke kufungashiwa virago.

Ikawa ni sherehe kwa mkwewe na wifi yake Amisa. Banzi anapata mwanamke mwingine. Anaitwa Lady. Huyu ni tofauti kabisa na Amisa. Ni mtoto wa mjini. Wakati wakidhania mambo yataenda kama walivyopanga, ikawa kinyume chake. Lady hafanyi kazi yoyote nyumbani. Kutwa kujipodoa. Mama mkwe ndiyo akageuka kuwa 'hausigeli'. Kitendo hiki kilionekana kumchefua Stella.

Kibaya zaidi akajisingizia ujauzito asiokuwa nao. Jaribio lake la kutaka kumhonga nesi pesa ili amuibie mtoto hospitalini linashindikana. Kwa bahati mbaya sana wakati anaondoka, Stella naye anaingia kwenye hospitalini hiyo na nesi huyo anamhadithia kilichotokea, bila kutambua kuwa anayetoka ni wifi yake.

Siri inafichuka. Ugomvi mkubwa unazuka nyumbani wakati Banzi yupo safarini. Lady anatumia kutumia mwaya huo kumpigia simu kuwa mimba imeharibika baada ya kupigwa na wifi yake Stella.

Nyumba sasa haikaliki. Stella na mama yake wanaonekana vikaragosi mbele ya Lady. Wanaamua kwenda kwa mganga kwa lengo moja tu, kumdhuru mwanamke huyo. Wakati huo huo, Lady naye anakwenda kwa mganga huyo huyo kwa lengo hilo hilo.

Wakiwa nyumbani, Lady na mama mkwe wake, wanaanguka chini kwa kupigwa na kitu kinachodhaniwa kuwa ni jini la mganga.

Lady anafariki, mama yupo hoi. Stella ikabidi amuelezee kaka yake yote yaliyofichika. Ukweli unajulikana. Banzi na familia yake wanakwenda kwa Amisa kumuomba msamaha. Mama anapona baada ya kuombewa na mchungaji waliyemkuta ukweni. Lakini pia walimkuta Amisa akiwa na mtoto, kumbe alipofukuzwa, tayari alikuwa mjamzito.

Kasoro ndogo kwenye filamu hii ni eneo la kijana aliyekodiwa kwenda nyumbani kwa watu kudai ni mpenzi wa mke wa mtu.

Hapa uhalisia unakosekana, kwa sababu si jambo la kawaida kwenye mazingira halisi.

Mtunzi ingebidi atafute njia nyingine ya Banzi kudanganywa na kuamini kuwa mkewe si mwaminifu.



# HASHIKIKI

## TAYLOR SWIFT AOGELEA NOTI

ANAOGELEA kwenye fedha! Ndivyo maneno rahisi unavyoweza kumzungumzia mwanamuziki Taylor Swft baada ya kutangazwa kuwa ndiye msanii wa kike mwenye mkwanja mrefu duniani kwa mwaka 2019.

Kwa mujibu wa orodha mpya iliyotolewa na jarida maarufu la Forbes, msanii huyo amewatupa kwa mbali mwanamuziki mwenzake.

Taylor anakadiriwa kuwa na ukwasi wa fedha kiasi cha dola za Kimarekani Milioni 185 sawa na zaidi bilioni 400 za Kitanzania.

Utajiri huo umetajwa kuwa unatokana na ziara yake ya muziki 'Reputation Tour' ambayo ilimuingizia kiasi cha zaidi ya bilioni 600

Mwaka jana nafasi hiyo ilichukuliwa na mwimbaji Katy Perry ambaye alitajwa kuwa na kiasi cha bilioni 100.

Taylor ambaye hivi karibuni alikuwa na kashfa ya kuiba nyimbo, pengine kutajwa huko na jarida hilo kutampa afueni.

Wasanii waliomfuatia kwa utajiri ni Beyonce ambaye ni mke wa rapa Jay Z ambaye amefikia zaidi ya dola milioni 81 na Rihana dola milioni 62,

Mastaa wengine walitajwa kuwa ni Katy Perry (dola milini 57), Pink (milioni 57), Ariana Grande (milioni 48),

7. Jennifer Lopez (nuilioni 43), Lady Gaga (milioni 39, Celine Dion (milioni 37) na Shakira amejikuusanyia milioni 35.

# Seun Kuti mdomo utakuponza



MWANAMUZIKI Seun Kuti, amejitokeza na kuwakemea wanasiasa na kuahidi kula sahani moja kwa kitendo chao cha kumfanya kuishi kama mgeni katika nchi yake ya Nigeria.

Seun Kuti amesema ana matumaini siku moja wananchi wa nchi hiyo wataamka na kulinda maslahi yao.

Kulingana na mahojiano aliyofanya na Object TV anaumia kuona viongozi mbalimbali wanavyowaongoza wananchi kwa mkono wa chuma, hivyo naamini kuna siku hayo yatakwisha.



## Hee! Okoye huogopi polisi wewe?

MKALI wa muziki aliyekuwa mwimbaji wa kundi la Psquare, Paul Okoye, amewajia juu askari polisi wa nchi hiyo kwa kuwaita wajinga.

Katika ujumbe alioweka katika akaunti yake ya Instagram, amesema polisi wanailetea nchi hiyo aibu wakati wananchi wanahijitahidi kujivunia.

"Wanamuziki, wanamichezo, wanawake na vijana wajasiriamali wanaitangaza nchi yao duniani kote, lakini polisi wanaibomoea na kufanya mambo ya kijinga," amesema.

## D'Banj muombe Mungu akufute chozi

BAADA miezi 14 kupita tangu mtoto wake wa kiume kufariki, mwanamuziki wa Nigeria, Oladapo Daniel Oyebanjo maarufu kama D'banj, ametangaza ujio wa mtoto mwingine.

Kulingana na mahojiano aliyofanya nchini uingereza D'Banj, amesema hivi karibuni atakuwa baba tena baada ya mke wake kubeba ujauzito.

Mkali huyo amewashukuru mashabiki wake kwa kusimama upande wake na familia pale alipopata msiba huo mzito, lakini kwa sasa anatumaini kwa uwezo wa Mungu wanatarajia kumpokea mtoto huyo.





## Miley kweli kang'ang'ana

NYOTA wa muziki wa Marekani, Miley Cyrus amesema uvumi unaosambaa kwamba ameachana na mume wake Liam Hemsworth hauna ukweli wowote.

Awali ilitaarifiwa kwamba Miley Cyrus anatarajiwa kupewa talaka baada ya tuhuma ya kutoka kimapenzi na mwanamume mwingine.

Akitumia ukurasa wake wa Twitter, mrembo huyo amesema yeye na mume wake wapo poa na kwamba maneno yanayosambaa hayana ukweli na wao hawana muda wa kuyafuatilia.

## Mapenzi kwenda mbele BBNaija

MAPENZI kati ya washiriki wa shindano la Big Brother Nigeria, Rodd na Esther, yanazidi kushamiri na kusababisha mashabiki wao kupandwa na joto la kutaka kujua hatma yao.

Wiki hii Rodd ameonekana kupagawa zaidi pale Esther alipoamua kumpa busu la kimahaba na kuhitimisha urafiki wao ambao umeonekana kukua kila siku.

Esther ameonekana kumganda zaidi kijana huyo, huku Rodd naye akiwa katika ya kuzidiwa na hisia kali za kimahaba kiasi ambacho ilimbidi kumwambia Biggie kwamba anahisi kuzidiwa mapenzi.



**SAFU**



Na John Juma
0716217615

**MIONZI YA SHERIA**

# Ukirasimisha biashara ni rahisi kukopesheka

MSAMIATI wa kurasimisha biashara si neno geni zama hizi. Ni mambo yanayozungumzwa kila wakati. Kikubwa kinachoweza kukuletea tija iwapo utarasimisha kiwanja, nyumba na biashara ni wepesi wa kukopesheka.

Njia mojawapo ya kurasimisha ni pamoja na kufungua kampuni ambayo ni moja ya namna ya kurasimisha biashara unazofanya. Kusajili jina la biashara nayo ni namna nyingine ya kuirasimisha biashara. Safu hii leo inazungumzia zaidi njia ya pili ya kusajili jina la biashara kama utaratibu wa kuifanya kuwa rasmi. Na hii ni kwasababu utaratibu mwepesi, wa haraka, na wa gharama ndogo sana.

Mfano wa jina la biashara ni kama, Muheza Bazaar, King-David Investment, Michael-Kijaji Traders, Mzalendo Socio-Economic Activist Group (MSEAG), Kazi na Sala Group na Mkulima General Traders.

**JINA**

Jina la biashara msingi wake ni nini? Jina la biashara ni lile jina linalotumiwa na mtu kama utambulisho wa biashara yake inayofanywa katika mfumo ambao si kampuni. Kampuni zina majina lakini majina hayo hayawezi kuitwa ya biashara bali ni majina ya kampuni.

Jina la biashara ni kwa yule ambaye biashara yake imesajiliwa lakini sio kampuni.

Aidha, mwenye biashara ambayo haijasajiliwa lakini analo jina fulani analotumia kisheria huyo hana jina la biashara. Hilo jina si lake na mtu mwingine anaweza kulisajili na akamtaka huyu ambaye hajalisajili kuacha mara moja kulitumia .

Ili sheria ikutambue kuwa una jina la biashara ni pale tu unapokuwa umesajili jina hilo.

**MAMLAKA**

Usajili wa jina la biashara hufanyika kwa Wakala wa Msajili wa Biashara na Kampuni-Brela. ukifika hapo utawaeleza kuwa unataka kusajili jina la biashara watakupa fomu maalum utaijaza.

Lakini kabla ya hapo utatakiwa utume maombi maalum hapohapo Brela ukitaka kujua iwapo jina ulilochagua kuwa la biashara yupo mtu mwingine analitumia au la.

Hii ni kwasababu jina ni moja Tanzania nzima. Hakuwezi kuwa na majina mawili au zaidi yanayofanana huku yote yakiwa yamesajiliwa.

**ADA YA USAJILI**

Unaweza kujiuliza ada ni kiasi gani, Jibu ni kwamba usajili wa jina si gharama kubwa.

Mara ya mwisho mwaka 2015 ilikuwa Sh. 6,000, kwa hiyo ni kiasi kinachopatikana sana na hata kama kimepanda bila shaka hakiwezi kuzidi 20,000.

**TIN**

Kuwapo kwa namba ya mlipa ya kodi au Tin Number (TN) katika kurasimisha biashara kupata namba ya malipa kodi Tin Number ni hatua ya muhimu sana. Karibia kila ofisi ya TRA pote hata mikoani hutoa namba hizi.

Wanazo taratibu ikiwa ni pamoja na kuleta barua kutoka serikali za mitaa kwa anayehitaji kupata namba hiyo. Kwahiyo ni lazima pia upate namba hii.

**LESENI**

Ukiwa tayari umesajili jina na umepata nambari ya mlipa kodi basi hatua inayofuata ni kutafuta leseni ya biashara. Leseni hizi hupatikana manispaa. Kila manispaa ina utaratibu wa kutoa leseni . Viambatanisho utakavyotakiwa kuwa navyo ni pamoja na ushahidi kuwa unayo namba ya mlipa kodi.

**FAIDA ZA KURASIMISHA.**

Jambo hili lina faida mojawapo ni kuwa na sifa za kukopesheka katika taasisi za fedha. Lakini pia hata zile zinazotolewa na serikali kwenye halmashauri kwa ajili ya wajasiriamali unaweza kuomba na ukapewa. Si rahisi kupata fedha hizi kama haujarasimisha biashara kisheria.

Pili ni kinga ya biashara zako kwa kuwa unaweza kupata bima ya majanga kama moto na mafuriko unapokuwa umerasimisha unaweza kufidiwa lakini si rahisi kupata bima ya biashara ikiwa hujarasimisha.

Tatu unaondoka katika kufanya biashara kienyeji na kuanza kufanya biashara kisasa na katika mfumo rasmi bila kujali udogo wa biashara zako.



Na Reubeni Lumbagala

**KALAMU YA MWALIMU**

# Tunapohitimisha msimu wa maombi elimu ya juu

SIKU ya 15 Julai iliyopita, Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU) ilifungua pazia kwa waombaji kuomba nafasi mbalimbali katika vyuo vilivyopo nchini ili kuweza kujiunga kusomea kozi wazipendazo, ili kutimiza ndoto na malengo waliyojiwekea.

Kazi ya uombaji huo wa nafasi za vyuo vikuu linaendelea hadi Agosti 10, 2019 litakapohitimishwa kwa awamu ya kwanza. Hii ni fursa adhimu kwa vijana waliohitimu kidato ch sita mwezi Mei mwaka huu na wale wanaopenda kujiunga na elimu ya juu kuchangamkia fursa hiyo haraka.

Kutokana na unyeti wa kozi zinazotolewa na vyuo vikuu, ni muhimu kwa waombaji wa kozi hizo kufanya tafakuri pana kabla ya kuingia katika mfumo na kuanza kuomba kozi kwani kozi hizo ni safari ya kutimiza hatima zao kupitia elimu watakayoipata vyuoni.

Waombaji wa kozi za elimu ya juu wanapaswa kuzingatia yafuatayo kwa umakini mkubwa. Mosi, mwombaji atambue aina ya kazi anayopenda kufanya baada ya kuhitimu masomo yake.

Kwa kutambua aina ya kazi anayopenda kuifanya baada ya kuhitimu elimu ya juu, utakuwa mwongozo wake wa kutambua aina ya kozi ya kusomea.

Mathalani, ikiwa mwombaji anapenda kufanya kazi ya uhasibu. Kozi zitakazomfaa hapo mwombaji anajumuisha maendeleo kama shahada ya uhasibu, usimamizi wa fedha na biashara.

Pili, mwombaji aliunganishe kiwango cha ufaulu wake na sifa za kozi anayotaka kuomba kama zinaendana.

Ni vyema mwombaji akafahamu kiwango cha ufaulu kinachohitajika kwa waombaji wa kozi husika, ili alinganishe ufaulu wake kama unakidhi sifa zilizoainishwa. Ikiwa mwombaji atakuwa na ufaulu ambao ni chini na kiwango kinachohitajika katika kozi anayopenda kuomba, anapaswa kuacha kuchagua kozi hiyo na kuchagua nyingine inayoendana na ufaulu wake, ili apate sifa stahiki za kuchaguliwa.

Kwa mfano, kozi ya shahada ya kilimo, ikihitaji mwombaji aliye na ufaulu wa daraja la kwanza au la pili. Mwombaji mwenye ufaulu wa daraja la tatu, hapaswi kuomba kozi hiyo, kwani anakuwa amekosa sifa za kuchaguliwa kwa kutokukidhi kiwango cha ufaulu husika.

Ili kuepuka kukosa kabisa nafasi ya chuo, mwombaji mwenye daraja la tatu, anashauriwa kuomba kozi zinazohitaji ufaulu wa daraja la tatu ili kuchaguliwa na si kukosa kabisa nafasi ya chuo.

Tatu, mwombaji aombe kozi zenye uhusiano na mchepuo (combination) aliyosomea. Vyuoni zipo kozi nyingi zinazoendana na tahasusi za sayansi, sanaa, biashara na kilimo.

Tahasusi hizi zote zina kozi zinazoendana nazo kwa waombaji wa vyuo vikuu. Mathalani, mwombaji aliyesomea masomo ya sanaa, anaweza kusomea kozi kama vile, ualimu wa masomo ya sanaa; uandishi wa habari, sheria, utawala, maendeleo ya jamii, uhusiano wa kimataifa, sayansi ya siasa, au mazingira.

Aliyesomea sayansi anaweza kusomea kozi za uhandisi, famasia, udaktari, kilimo, mifugo, mimea. Kozi zinazoendana na masomo ya biashara, ni pamoja na uhasibu, masoko, uchumi na huduma za fedha.

Hivyo basi, itakuwa ajabu kwa mwanafunzi aliyesomea sayansi kuomba kozi za uandishi wa habari, maendeleo ya jamii, sheria nk, kwani kwa kufanya hivyo atakuwa amejikosesha nafasi yeye mwenyewe kwani mwombaji huyo alipaswa kuomba kozi zinazoendana na elimu ya sayansi aliyosomea kidato cha tano na sita au katika ngazi ya stashahada.

Nne, mwombaji aombe chuo chenye aina ya kozi aitakayo. Hili ni jambo la msingi sana kuzingatiwa na waombaji wote. Kabla mwombaji hajaomba nafasi ya kujiunga na elimu ya juu, ni vizuri afanye utafiti wa vyuo vinavyofundisha kozi azipendazo, ili atakapoingia mtandaoni kuomba nafasi za kujiunga katika vyuo mbalimbali, azingatie kuomba vyuo vyenye kutoa kozi zinazoendana na matakwa yake.

Kwa kushindwa kufanya hivyo, mwombaji anaweza kupoteza nafasi kwa kudhani kozi zake hazipatikani katika vyuo na hivyo kughairi kufanya maombi.

Tano, mwombaji anapaswa azingatie kupangilia kozi anazopenda kuzisoma kwa mtiririko mzuri. Katika kuomba kozi, mwombaji aanze na kozi anayoipenda zaidi kwa kuiweka namba moja ndipo kozi nyingine zifuate kwa mujibu wa matakwa yake.

Endapo mwombaji ataomba kozi bila kupangilia mtiririko, atajikuta akichaguliwa kozi ambayo si chague lake namba moja na hivyo kujikuta akisoma kozi ambayo si kipaumbele chake.

Kama mwombaji anapendelea kusomea kozi ya sheria au utawala, ahakikishe kozi ya sheria anaiweka namba moja ikifuatiwa na kozi ya utawala. Ikiwa mwombaji ana sifa zote za kukidhi kuchaguliwa kozi aliyoiweka namba moja, basi moja kwa moja yuko katika nafasi nzuiri ya atachaguliwa kusomea kozi hiyo.

Kwa haya machache, yanaweza kuwasaidia waombaji wa kozi mbalimbali za elimu ya juu. Uombaji wa vyuo unaendelea. Nawasihi waombaji waitumie fursa hiyo kabla ya tarehe 10, mwezi ujao litakapofungwa kwa awamu ya kwanza. Tafakari.

# ACCESS NJIA ILIYONUSURU MAELFU KUWA MBUMBUMBU



Mwenyekiti wa Kamati ya Shule ya Chilende Omari Mpilipili, (kulia), Abeid Mussa (katikati) shuhuda aliyeshiriki kuanzisha shule hiyo chini ya program ya ACCESS na Muhibu Bendara (kushoto) mjumbe wa kamati ya shule hiyo, wakizungumza na wanahabari (hawapo pichani) . Nyuma ni majengo ya Shule ya Chilende, ambayo awali ilikwa kituo cha ACCESS.

**Na Mwandishi Wetu**

KAMA kusingekuwa na shule za wananchi au vituo vya kujifunzia kwenye vijiji visivyokuwa na shule, takribani watoto 5,268 wangekuwa mbumbumbu wasijua kusoma, kuandika wala kuhesabu.

Aidha, pengine mabinti wangepata mimba na kuolewa utotoni na huenda baadhi wangepoteza maisha kutokana na kuzaa katika umri mdogo na wengine kuambukizwa VVU na Ukimwi.

Takwimu hizo ni kwa mujibu wa Shirika la ActionAid Tanzania, zinazozungumzia mradi wa ACCESS uliovihudumia baadhi ya vijiji vya mikoa ya Mtwara na Kigoma ambavyo havikuwa na shule wala namna ya kuwasaidia waliofikia umri wa kwenda shule kupata elimu.

Mratibu wa Shirika la ActionAid, anayesimamia Wilaya za Tandahimba na Newala mkoani Mtwara, Dinno Celestine, akizungumza wakati wa ziara za kutembelea miradi ya elimu inayosimamiwa na shirika hilo katika wilaya hizo anasema program ya kujenga vituo vya kujisomea au shule za wananchi zilizoitwa 'ACCESS' ulifanyika kati ya 2002 na 2010.

"Tatizo la ukosefu wa shule vijijini, umbali mrefu kati ya shule na makazi ya wanavijiji, wanyama wakali vilikwamisha watoto wengi kusoma. Ikabidi kushirikiana na wananchi kujenga vituo Tandahimba na Newala,"anasema Celestine.

### KILICHOFANYIKA

Celestine akiwa Shule ya Msingi Namedi wilayani Tandahimba, moja ya wanufaika wa mradi wa kuzisaidia jamii zisizokuwa na shule kupata elimu, anasema vilijengwa vituo vya kujisomea au shule za wananchi -ACCESS zilizosomesha watoto maskini.

ACCESS ni kifupi cha maneno 'Cost Effective Centres for Education' kwa mujibu wa maelezo yake ambao ni mradi wa kujenga vituo vya gharama nafuu vya kutolea elimu ambavyo vilihusisha wananchi na ActionAid.

Anasema katika mwaka 2005 vilikuwapo vituo vya ACCESS 50 ambavyo vilikuwa vimesajili wanafunzi 5,268 na zaidi ya asilimia 51 walikuwa mabinti na mwaka 2005 vituo 23 vilisajiliwa rasmi kuwa shule za msingi za serikali. Katika mkakati huo pia zilijengwa sekondari tatu.

"Anafafanua kuwa ACCESS ni mfumo uliokuwa unasaidia kuwapa elimu lakini si elimu mbadala, lengo ni kuweka vituo vya kusomea kwenye maeneo yasiyo na shule kabisa ili watoto wasome,"anasema Celestine.

Anabainisha kuwa tofauti na utaratibu rasmi, watoto hawakulazimika kuvaa sare, wala kuwa na darasa rasmi wala banda wakati mwingine la nyasi, lakini ni kituo cha kuwasomesha mambo muhimu kama kusoma, kuandika, kuhesabu kwa miaka minne na walielimika.

"Vituo vilikuwa ndani ya vijiji ili kuwafikia wanafamilia maskini wenye umri kati ya miaka 7 hadi 14. Tulitaka wasome bila gharama. Mabinti waende shule. Iliwezekana na watu waliamini wasichana wako salama na wanasoma kwenye kituo cha wananchi kilichoko kijijini kwenye makazi yao,"anasema Celestine.

### SHULE WANUFAIKA

Miongoni mwa shule zilizofaidika ni Namedi iliyoko wilayani Tandahimba, Mwalimu Mkuu Joseph John, anasema mwanzo wa Namedi ni shule ya ACCESS iliyojengwa mwaka 2002 na Action Aid na wanakijiji cha Namedi.

Anasema ilianza kama banda la nyasi na wanafunzi 40 wasichana 17 na wanaume 23 na kwa kuiimarisha mwaka 2006 Action Aid na wanavijiji walijenga madarasa mawili na ikasajiliwa rasmi kuwa katika mfumo wa shule za serikali na kuitwa Shule ya Msingi Namedi.

"Leo tuna wanafunzi 119 wasichana 56 na waliobakia ni wanaume. Tunafanya vizuri na mwaka 2017, tumekuwa shule ya tano katika ya 126 za wilaya ya Tandahimba wakati mwaka 2018 tumekuwa wa saba kati ya shule 126," anasema Mwalimu John.

Anaeleza kuwa shule za msingi zilikuwa chache na mbali na idadi kubwa ya watoto hawakuweza kutembea zaidi ya kilometa 10 (kwenda na kurudi) kwa siku.

Munaida ni shule nyingine ambayo awali ilikuwa kituo cha ACCESS, Mwalimu Mkuu Muhibu Muba Bakari, anasema ilianza mwaka 2002, wakati huo hakukuwa na shule hata moja.

"ActionAid walijenga kituo au shule ya wananchi baadaye wakaongeza madarasa mawili wakaendelea kuongeza jingine.

Anasema kijiji cha Mnaida hakikuwa na shule. Wanyama wakali hasa chui, simba na fisi walikuwa wamezagaa kwenye pori jirani na kijiji hicho.

Anasema program ya ACCESS ilikuwa mkombozi kwani watoto wadogo hawakuweza kwenda shule za vijiji jirani mfano Mivanga au Nambahu kusoma.

"Kuna umbali mrefu kuzifikia, hakukuwa na miundo mbinu , kulijaa mapori na wanyama wakali walitishia maisha." Kwa mujibu wa Bakari na kwamba kwa ujumla maeneo mengi ya Tandahimba vijana wengi walizaliwa kuanzia 1980 hadi 2000 wengi wanatatizwa na kusoma, kuandika na kuhesabu kutokana uhaba wa shule uliovikumba vijiji vingi.

Anasema, kwa mfano kutoka kijiji cha Namedi hadi kufikia shule iliyoko kijiji jirani cha Mivanga mwanafunzi angetembea kilometa takribani nane kwenda na kurudi.

Shule nyingine za ACCESS ambazo sasa ni shule rasmi za serikali ni Mbeya iliyoko katika kijiji cha Mbedede, nyingine ni Chilinde pamoja na Tumaini zote zilizoko Newala mkoni Mtwara.

Akizungumzia habari za ACCESS Mwalimu Sysnatus Mnali wa Shule ya Tumaini anasema hadi machi 2008 Kijiji cha Nangudiane hakukuwa na shule na watoto wengi hawakusoma.

Kadhalika Mwalimu Ahmed Chilumba wa Shule ya Chilende iliyoko kijijini Chilinde huko Newala anaongeza kuwa hadi 2010 kijiji hakikuwa na shule.

Anafafanua kuwa matatizo ya umbali mrefu hadi shuleni, maporini, wanyama wa kali yalikuwa kikwazo lakini Action Aid ilipojenga madarasa au vituo vya ACCCES ilisaidia kuboresha hali ya elimu katika vijiji ving.

### MAFANIKIO

Shule zote za ACCESS zilirasimishwa na serikali na kuingizwa katika mfumo rasmi wa elimu wa taifa na kutambulika rasmi uwa shule za msingi na kuziendeleza kwa kujenga madarasa, kuleta walimu, kuongeza huduma zilizopungua mfano visima vya maji na vyoo, anasema Celestine mratibu wa shirika hilo Tandahimba na Newala.

Kujenga madarasa vijijini kusikokuwa na shule yoyote hapo awali.Baada ya miaka miwili watoto wengi wa kaya masikini walimudu kusoma, kuandika na kuhesabu.

"ACCESS ilileta tofauti katika maisha ya wakazi wengi vijijini na maisha watoto yalibadilika wakapenda kusoma kwa vile shule ilifika nyumbani kwao na kuwapunguzia safari ndefu za kutembea na kuhofia kuumizwa na wanyama".

"Hata wasichana walielimika na wengi kuepushwa na mimba za utotoni," anakumbusha Mwalimu Sofia Mtangashari wa Namedi.

"Watoto wanaomaliza masomo yao katika vituo vya ACCESS waliendelea na kidato cha kwanza hadi cha nne na wengi wamefanya vizuri," anasema Khamisi Cheusi mnufaika wa ACCESS aliyesoma Namedi mwaka 2004 na kusoma hadi kidato cha nne katika Sekondari ya Ngongolo iliyoko wilayani Tandahimba.

### CHANGAMOTO

Kwa mujibu wa walimu na wajumbe wa kamati za shule changamoto kubwa ni uhaba wa walimu mathalani zote kuanzia Mnaida, Tumaini, Mbeya na Chilende hazina walimu.

Zote zina walimu wanne wanaohudumia wanafunzi takribani 200 kuanzia darasa la kwanza hadi la saba.

Hali hiyo inaonyesha kuwa walimu wote wakiingia darasani wanafunzi wa madarasa manne watakuwa bado hawana wa kuwafundisha, anasema Mwalimu Gama wa Shule ya Mbeya.

Uchache au ukosefu wa vyumba vya madarasa, vyoo, nyumba za walimu, ukosefu wa chakula shuleni ni mambo yanayolalamikiwa.

Kwa sababu wazazi na walezi wengi hawajasoma mwitikio wa elimu ni mdogo na mara nyingi kuna ubishi mkubwa katika kuchangia elimu, mfano kugharamia chakula. Wanasema walimu Chilumba wa Shule ya Chilende na Mnali wa Tumaini.

### MAPENDEKEZO

Viongozi hawa wanashauri watu wengi kuwekeza kusaidia elimu, wajenge madarasa, vyoo, visima vya maji.

Jukumu hili lihusishe watu binafsi, kampuni, viwanda , azaki ili kubadili hali ya elimu katika ukanda wa kusini, anasema Mwalimu Mnali.

"Watu wajitokeze ina maana kama si ActionAid kijiji na watu wasingekuwa na shule?" anahoji Mnali.

MAKALA

# SABABU ZINAZOKWAMISHA KESI ZA UKATILI WA KIJINSIA KORTINI Z'BAR

**Na Theodatus Muchunguzi**

SABABU mbalimbali zimebainishwa kuwa zinachangia kuongezeka kasi ya matukio ya ukatili wa kijinsia na kukwamisha mashtaka na kesi hizo mahakamani.

Mshikamano wa kijamii (muhali) na rushwa ni miongoni mwa sababu zinazotajwa sana na wadau kuwa kikwazo cha kuchelewesha au kukwamisha mashauri hayo kutomalizika mahakamani.

Pamoja na wadau mbalimbali kulalamikia muhali na aina nyingi za rushwa, utafiti uliofanyika hivi karibuni Zanzibar, umebainisha sababu nyingine nyingi zikiwamo na hizo.

Chama cha Wanahabari Wanawake Tanzania (Tamwa) Zanzibar kikitumia waandishi wa habari wachanga ambao ni marafiki (young media fellows-YMF), walifanya utafiti kwa kutathmini hali ya ukatili wa kijinsia Zanzibar katika wilaya mbili Kaskazini 'A' (Unguja) na Wilaya ya Mkoani (Pemba).

Lengo la utafiti huo lilikuwa ni kufanya ushawishi kwa vyombo vya habari kudhihirisha mchango wake muhimu wa kutokomeza udhalilishaji wa kijinsia kupitia mkakati wa utetezi na kuingilia kati kwa ajili ya kuboresha yaliyomo pamoja na kujielekeza katika mambo kadhaa kuhusiana na udhalilishaji wa kijinsia pamoja na kuwahimiza wadau wengine serikalini na asasi binafsi kushiriki kwa dhati katika utokomezaji wa ukatili wa kijinsia kupitia vyombo vya habari.

Mshauri wa masuala ya habari, Ali Sultan, aliwasilisha ripoti hiyo hivi karibuni mjini Zanzibar, anasema kesi za matukio mengi ya udhalilishaji kijinsia zinamalizikia ngazi ya familia au kuvurugwa kwa njia za rushwa kwa kushirikiana na polisi au mawakala wengine wa vyombo vya kusimamia sheria.

Kwa mujibu wa Sultan, lengo la njama hizo ni kuzilinda kesi hizo, hivyo kupunguza jitihada za wanaharakati katika mapambano.

Kwa mujibu wa ripori hiyo, matukio ya ubakaji yanayongoza katika udhalilishaji wa kijinsia katika wilaya hizo za Mkoani na Kaskazini A, kwa asilimia 80 kati ya matukio yote yaliyoripotiwa katika Dawati la Jinsia Polisi kwa mwaka 2017/2018.

Ripoti hiyo pia inautaja ushirikina umekuwa matukio mapya yanayohusiana na udhalilishaji wa kijinsia Zanzibar, huku Sultan akisema:

"Katika baadhi ya matukio, utafiti umebainisha kuwa kuna uhusiano wa moja kwa moja kati ya wahusika na waganga wa jadi kupitia madai ambayo yanahitaji utafiti zaidi kwa ajili ya kupata takwimu na uthibitisho wa suala hilo."

Utafiti huo unapendekeza umuhimu wa kulishughulikia tatizo la udhalilishaji wa kijinsia Zanzibar kutokana na matukio hayo kuripotiwa zaidi katika maeneo yote ya visiwa vya Unguja na Pemba.



Wananchi wa shehia ya Utaani iliyoko Wete Pemba, wakiangalia igizo la kikundi cha Thesode kilichopo Chonga Wilaya ya Chake Chake wakati wa mkutano wa kutoa elimu ya udhalilishaji iliyoandaliwa na Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto Pemba. **PICHA: MWANDISHI PEMBA.**

Utafiti huo ulienda sambamba na Mpango wa Taifa wa Zanzibar wa kutokomeza vitendo vya udhalilishaji wa Kijinsia dhidi ya Wanawake na Watoto (NPA-VAWC), 2017-2022, ambao unataka umakini katika kutokomeza vitendo hivyo.

Kwa mwaka 2018, jumla ya matukio 942 ya udhalilishaji wa kijinsia yaliripotiwa katika Dawati la Jinsia Polisi Police na Dawati la Watoto Zanzibar, jambo ambalo ni kupungua kwa kiasi kikubwa kutoka matukio 1,041 yaliyoripotiwa mwaka 2017.

Baadhi ya wadau waliochangia ripoti hiyo, walibainisha sababu zingine ambazo zinachelewesha au kukwamisha kesi hizo mahakamani.

Inaelezwa kwamba, kitendo cha baadhi ya watuhumiwa kesi za udhalilishaji kudanganya kuhusu umri ili waonekane kuwa wapo chini ya umri wa miaka 18, ni moja ya vikwazo kwa kesi za udhalilishaji wa kijinsia.

Hiyo ni kauli ya Hakimu wa Mahakama ya Mkoa wa Kaskazini Unguja, Makame Mshamba, ambaye anaeleza kuwa baadhi ya watuhumiwa wa kesi hizo wamekuwa wakighushi vyeti vya kuzaliwa na kudanganya umri kuwa hawajafikia miaka 18, umri ili wasiweze kutiwa hatiani.

Kwa mujibu wa sheria ya Zanzibar, umri wa kushtakiwa na kuhukumiwa kwenda jela ni kuanzia miaka 18, ambao ni umri wa mtu mzima.

Aliyasema hayo katika kikao cha kujadili taarifa ya utafiti wa Tamwa kuhusu udhalilishaji wa kijinsia ulioandaliwa na chama hicho na kuwashirikisha wadau mbalimbali.

Hakimu huyo anasema kwa mujibu wa sheria ya mtoto ya Zanzibar ya mwaka 2011, mtoto chini ya umri wa miaka 18 anakinzana na sheria, hivyo hapewi adhabu ya kifungo, badala yake hupelekwa katika kituo cha kurekebisha tabia (TAI).

Mshamba anasema kuwa watuhumiwa wa kesi za udhalilishaji wenye umri wa miaka 19 hadi 25 hutumia mwanya huo kwa kughushi vyeti vya kuzaliwa ili waonekane kuwa bado ni watoto.

Aidha, anasema kuwa kitendo cha baadhi ya madaktari kukataa kutoa ushahidi mahakamani ni moja ya vikwazo kwa kesi za udhalilishaji wa kijinsia kushindwa kusikilizwa kwa wakati.

Mshamba anasema madaktari wamekuwa wakisumbua, kutokana na kukataa kufika mahakamani wanapoitwa kwa ajili ya kutoa ushahidi kwa mtu alieathirika kwa matukio ya udhalilishaji wa kijinsia kusudan kubakwa au kulawitiwa.

Kwa mujibu wa Mshamba, hilo ni kosa kwa mtu anapoitwa mahakamani na kukataa wito ule, hivyo inachukuliwa ni sawa na kukwamisha juhudi za mahakama katika utekelezaji wa majukumu yake.

"Madaktari wanatusumbuwa sana katika uendeshaji wa kesi zetu kwa sababu wao wamefanya kazi ya uchunguzi kwa muathirika...wanaitwa waje wathibitishe kazi yao, lakini hawataki," anasema.

Alisema zipo baadhi ya kesi zimekwama kwa sababu ya kushindwa kupatikana ushahidi kutoka kwa madaktari walifanya kazi ya kupima mtu aliyedhalilishwa.

**"Katika baadhi ya matukio, utafiti umebainisha kuwa kuna uhusiano wa moja kwa moja kati ya wahusika na waganga wa jadi kupitia madai ambayo yanahitaji utafiti zaidi kwa ajili ya kupata takwimu na uthibitisho wa suala hilo."**

Kwa upande wake, Ofisa kutoka Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) Zanzibar, Rashida Ahmed, anaitetea ofisi yake dhidi ya lawama nyingi kuwa inachangia kukwamisha mashauri ya ukatili wa kijinsia.

Anasema baadhi ya kesi zinazopelekwa kutoka katika Jeshi la Polisi uchunguzi wake kwa kiasi kikubwa unakuwa haujakamilika, hivyo kuacha maswali mengi ya msingi yanayotakiwa kufanyiwa kazi.

"Tunapoletewa kesi za ukatili wa kijinsia kutoka Polisi baada ya kukamilika kwa uchunguzi wake... kwa kiasi kikubwa huwa hazijakamilika na ndiyo maana tunazifuatilia zaidi kwa kutaka kujua mambo ya ziada," anasema Rashida.

Rashida anaongeza kuwa ipo haja ya kuihusisha ofisi ya DPP katika kushughulikia kesi hizo kwa kuwa ndio mwavuli katika ufuatiliaji wa kesi, kuzipeleleza na kuzipeleka mahakamani. Meneja wa Sera na Utetezi Tamwa-Zanzibar, Hawra Shamte, anataja sababu kadhaa zinazokwamisha kesi mahakamani, akisema rushwa ya muhari ni kikwazo cha kuwa inawafanya wanajamii kutokuwataja wahusika wa matukio ya ukatili kwa kuwa ni ndugu au jamaa zao, hivyo kuamua kuzimaliza kifamilia.

Anafafanua kuwa hali hiyo inasababisha kuongezeka kwa ndoa za mkeka (wahusika kufungishwa ndoa za lazima na viongozi wa dini). "Mfano, mara nyingi wanaofanyiwa vitendo hivyo, wanakuwa wagumu kesi kutoa ushirikiano ili kesi zao kushughulikiwa kisheria kwa kusema huyu ni mpenzi wangu, siwezi kumuacha," anasema.

Anaongeza kuwa mamlaka husika za Polisi, Mahakama na Ofisi ya DPP hazifanyi kazi kama timu moja, hivyo mara nyingi kuonekana kama zinagongana.

Kwa mujibu wa taarifa fupi ya uchunguzi wa vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia iliyofanywa na Tamwa imebaini kwamba matukio hayo yamekuwa yakiongezeka ikiwamo ubakaji na ulawiti kwa watoto wa kiume na wanawake.

# Watoto kufa, wamama kubakwa ni adha ya uhaba wa maji Kisesa

**Na Elizabeth Faustine, MWANZA**

WANANCHI wa kata ya Kisesa na Bujora zilizoko katika wilaya ya Magu mkoani Mwanza, wanasimulizi nyingi za uhaba wa maji lakini kubwa wanacholalamikia ni vifo vya watoto vinavyoletwa na adha hiyo.

Japo hawana takwimu lakini wanasema ni mambo yanayotokea. Kuna watoto wanaofariki dunia kwa vile mama zao wameamka usiku wa manane na kuwaacha vitandani kwenda kusotea maji kata za jirani.

Ushuhuda huo anautoa Evaristina Mahela anapozungumza na Nipashe kuhusu kero hiyo, akilalamikia vifo vya watoto, anasema:

"Wakati mwingine mama anapoamka usiku kwenda kutafuta maji huku akiwaacha watoto na kibatari chumbani wengine huamka na kuanza kucheza matokeo yake mafuta na moto hukamata chandarua, godoro na mashuka na nyumba kulipuka."

"Mama anaamka usiku wa manane kusotea maji akirudi mali, nyumba na watoto wameungua. Hatimaye ni kilio na maafa lakini naye hayuko salama , njiani nako anabakwa, Kwa kweli hili naomba mliangalie, mabomba yameota kutu", anasema Mahela huku akilia.

Anasema wanatamani siku moja shida ya kusaka maji maporini tena kwa kilometa saba wanazotembea kwa zaidi ya saa sita ingeuke kuwa ndoto.

Kinamama hao wengi huanza safari usiku wa manane kuziendea kata za jirani za Nyanguge na Bukandwe zenye nafuu kiduchu.

Wakizungumza na Nipashe wananchi hao wanaeleza namna wanavyokabiliana na changamoto kadha wa kadha katika safari kutafuta maji, mfano Tereza Andrew anayesema, Kisesa maji yanatoka mara moja kwa mwezi na ndoo wanainunua kwa Sh. 500 hadi 1,000.

'Mara ya mwisho kuona maji yakitoka katika bomba langu ilikuwa mwezi Mei hivyo mpaka sasa ninachoona ni kutu." Anasema.

"Malalamiko yetu makubwa ni maji, tunaamka usiku wa manane, kina mama tulisomesha watoto kwa bustani za mboga, lakini leo hawaendi shule hatuna maji ya kilimo. Lakini pia wanakosa mahitaji hatuwezi kulima chochote tunahangaikia ndoo mbili za kunywa na kupikia"anasema Tereza.

Sara Masalu anaunga mkono akisema suala la maji kwao imekuwa kero kwani wanalazimika kuamka kuanzia saa 8:00 usiku na wakati mwingine wanayakosa.

"Ninaamka saa 8:00 usiku kwenda kutafuta maji, huku mtaani ndoo tunauziwa Sh. 1,000, kule tunanunua Sh 500. Nashangaa sisi watumiaji wa nyumbani tunayakosa lakini wauzaji mitaani wanayapata, Labda niwaulize mamlaka ya maji , huko ziwani nako wanayanunua," anahoji Sara anayeishi Kisesa.

**MAJIRANI WAKERWA**

Baadhi ya wananchi wa kata ya Bukandwe mahali ambapo wakazi wa Kisesa na Bujora wanachukulia maji wameeleza kero wanazopata kutokana na mwingiliano na foleni ya maji kisimani.



Teresa Andrew, mkazi wa Kisesa (aliyeshika kipaza sauti), akieleza changamoto wanazokabiliana nazo kutokana na ukosefu wa maji katika kata za Kisesa na Bujora, kwenye mkutano wa hadhara uliohudhuriwa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Profesa Mkumbo. (hayupo pichani): **PICHA: ELIZABETH FAUSTINE.**

Rhode Rayson, anasema maji yaliyopo kwenye kisima wanapochota hayawatoshi wenyeji lakini wanapokuja hao wa mbali foleni inazidi kuwa ndefu na hutumia muda mwingi kwenye maji.

Diwani wa kata ya Bukandwe Michael Minzi anasema alichimba kisima cha maji chenye uwezo kutoa lita 4,500 kwa saa kwa ajili ya kuwahudumia wananchi wa kata yake hivyo wanapoongezeka majirani uhaba unazidi kuwa mkubwa.

Minzi anasema kauli ya kizuri kula na jirani inawaponza, hiyo shida ya maji inakuzwa na ushirikiano na majirani wa Kisesa na Bujora.

**VIPI MWAUWASA?**

Chombo chenye jukumu la kuwapa maji wakazi wa Bujora na Kisesa, ni Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira jiji Mwanza (Mwauwasa), na Mkurugenzi wake Antony Sanga, akizungumza katika mkutano baina ya mamlaka hiyo na wanahabari mkoani Mwanza anasema tatizo ni gharama za uendeshaji.

Anapohojiwa katika mkutano ulioandaliwa na Klabu ya Waandishi wa Habari Mwanza, (MPC) anasema kinachokwamisha maji kuwafikia watumiaji ni gharama kubwa za uaendeshaji.

Anaeleza kuwa kuna baadhi ya maeneo yamekuwa na changamoto ya upatikanaji wa huduma ya maji, na wamekusudia kuboresha kwa kujenga miradi mipya yenye kuongeza mtandao wa usambazaji na kuyafikia maeneo hayo.

Anasema mamlaka hiyo inajiendesha kwa kutumia vyanzo vya ndani vya mapato.

"Hatubadilishi bei ya maji kwa ajili ya maslahi ya watumishi, tumelenga kuboresha huduma na miundombinu ya maji pamoja na kutatua changamoto za upatikanaji wa maji kwenye maeneo mengi hususani yale ya milimani na pembezoni," anasema Sanga.

Anaeleza kuwa mara ya mwisho Mamlaka ya Udhibithi wa Nishati na Maji (EWURA) iliidhinisha mabadiliko ya bei za maji kwa Mwauwasa takribani miaka minne iliyopita na kwa kipindi chote wameendelea kutumia bei zile zile licha ya kuwapo mabadiliko ya gharama za uendeshaji.

"Yote haya hufanya gharama kuwa kubwa zaidi hali iliyosababisha mamlaka yetu kushindwa kutekeleza mipango yake ya kuwafikishia huduma ya maji kikamilifu." Anasema Sanga.

Anataja baadhi ya viunga vinavyohudumiwa kuwa ni Kisesa, Bujora, Buhongwa, Kiseke na , Nyasaka Islamic, Nyasaka Riverside na Ibanda.

Anasema, Mwauwasa ndiyo inayowajibika kufanya matengenezo na ukarabati wa mabomba yale ya mamlaka hiyo pamoja na ya wateja yanayosababisha mivujo ya maji kabla ya mita ili kudhibithi upotevu wa maji bila kutozwa gharama.

**'MAJII' KUWA SALAMU**

Kwa namna ya kipekee wananchi walitoa kilio chao kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji Profesa Kitila Mkumbo, kwa kujibu salamu alizowapa kwa kuitikia majii.

Hayo yalitokea alipokuwa katika mkutano wa hadhara uliofanyika katika uwanja wa Mkapa Kisesa jijini Mwanza hivi karibuni na hiki ndicho kilichojiri.

Profesa Kitila :"Rafiki yangu mheshimiwa Kiswaga, mheshimiwa Mkuu wa Wilaya , waheshimiwa viongozi wote wa Magu, mabibi na mabwana habari za jioni.

"Majii" Ndivyo wananchi wakaitikia kwa sauti kubwa na Kitila akaendelea kusema Kisesa oyee akajibiwa 'majii'.

Baada ya kusikia kilio hicho alitumia hadhara hiyo kueleza mikakati ya serikali kunusuru hali hiyo ikiwamo kujenga miradi mitatu ya Sh, bilioni 16 katika miji mitatu kwa wilaya ya Magu, Misungwi, na Lamadi.

Aliwaambia kuwa katika taratibu za kiuongozi si jambo la kawaida Katibu Mkuu wa Wizara kufika katika mkutano wa hadhara lakini kwa sababu maji ni jambo nyeti , Katibu Mkuu wa CCM alipotembelea Magu aliagiza mbele ya hadhara na vyombo vya habari afike hapo mara moja kutatua tatizo hilo.

Aliahidi hatua kuchukuliwa ili kutatua changamoto ya maji Kisesa ni kuongeza mtandao wa maji utakaoendana na mahitaji ya sasa na miaka ijayo.

Profesa Kitila anakiri kuwa kero ya maji katika kata ya Kisesa na nyingine jirani ya Wilaya ya Magu ni kubwa na ndiyo maana serikali inatekeleza miradi mitatu ya Sh. bilioni 16 kwa Wilaya ya Magu, Misungwi na Lamadi

"Nyamohongolo nimepita nimeona wameanza kutandaza mabomba, hivyo nawaagiza Mwauwasa kuhakikisha mradi huu unakamilika kwa siku 90 kuanzia Agosti 15 hadi Novemba 15 mwaka huu, ili wananchi wa Kisesa na Bujora waweze kupata maji lakini pia wanawake waondokane na adha walizokuwa wanazipata," anasema Prof Mkumbo.

"Ni kweli mnahitaji matangi kwa ajili ya kutunzia na kuteremsha maji hivyo pia nimeagiza mradi wa ujenzi tangi kubwa uanze na ukamilike ndani ya miezi sita, hivyo miradi yote ikikamilika wananchi wanatakiwa kuuziwa maji kwa Sh. 50 kwa ndoo, tukirudi hapa mwezi Novemba na Desemba wapige ngoma za kutushukuru", anasema Profesa Mkumbo.

Aidha, anasema, suluhisho la kudumu la kumaliza changamoto ya maji ni mradi ambao unaogharamiwa na Benki ya Maendeleo ya Ulaya na Ufaransa kwa Sh bilioni 70 na utatekelezwa katika maeneo manne ya jijini hapa ikiwemo Kisesa,Usagara, Buswelu na Buhongwa.

Sera ya maji ya mwaka 2012 inaeleza mtu yeyote kupata huduma ya maji ndani ya mita 400 anazoishi, kadhalika CCM imetangaza ndani ya ilani yake jukumu la 'kumtua mama ndoo kichwani' ikiwa na maana kumfanya huru asisotee maji.

HABARI KIMATAIFA

# Mgonjwa wa tatu ebola afa Uganda

**KAMPALA,** Uganda

Msichana huyo alitengwa na kuhamishwa katika kituo cha kuwashughulikia wagonjwa wa ebola.

MAOFISA wa afya nchini Uganda wametangaza kifo cha binti mwenye miaka 9 kutoka Congo aliyethibitishwa kuwa na virusi vya ebola, aliyefariki Alhamisi wiki hii akipokea matibabu.

Walieleza kwamba alifariki wakati mazungumzo yakiendelea kuhusu kumrudisha Congo kwa matibabu zaidi. Mama wa msichana huyo aliyewasili na binti yake Uganda kupitia mpaka wa nchi hiyo na Congo wa Mponde - ametengwa na atarudisha nchini kwake kwa uchunguzi zaidi.

Mama na mwana huyo wanaripotiwa kuwa waliingia Uganda walikofika kutafuta matibabu.

Wizara ya Afya Uganda ilithibitisha kisa hicho kipya cha ugonjwa wa ebola katika mji wa magharibi wa Kasese.

Msichana huyo alipatikana akiwa na homa wakati wa ukaguzi wa ebola kwenye Mpaka wa Mpondwe.

Sampuli ya damu iliyotumwa kufanyiwa ukaguzi juzi ilithibitisha kwamba anaugua maradhi hayo.

Dalili za awali huenda ni pamoja na homa ya ghafla, kudhoofika haraka, maumivu ya misuli na kuumwa na koo.

Kiwango kinapozidi mtu anaweza kuanza kutapika, kuharisha na mara nyingine kuvuja damu ndani na nje ya mwili.

Msichana huyo alitengwa na kuhamishwa katika kituo cha kuwashughulikia wagonjwa wa ebola.

Uganda imeidhinisha na kuendeleza kwa ufanisi vituo vya ukaguzi katika mpaka wake na Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo katika jitihada ya kuuzuia mlipuko uliosababisha vifo vya karibu watu 2,000 katika mwaka uliopita. Mnamo Juni mwaka huu kuliripotiwa vifo vya watu wawili.

Mwanamume raia wa Uganda na mkewe wa Congo waliwapoteza watoto wawili wa kiume baada ya kurudi kutoka safari katika Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo walikokwenda kuwaona jamaa zao.

Ebola ni ugonjwa unaoambukizwa na virusi ambapo mwenye maambukizi hupata dalili za homa, uchovu, maumivu ya viungo na koo.

Pia kutapika, kuharisha na kutoka damu sehemu zenye matundu nje na ndani. Huambukizwa kwa njia ya kugusana, majimaji za mwili. **BBC**

## Japan yaonya kuitwisha Afrika madeni kiholela

**TOKYO,** Japan

WAZIRI Mkuu wa Japan, Shinzo Abe, ameonya dhidi ya kuzibebesha madeni makubwa nchi za Afrika, katika hali ambayo inaonekana kuwa kidole kinaelekezwa kwa China.

Waziri Mkuu wa Japan ameonya kwamba wawekezaji katika bara la Afrika hawanabudi kutahadhari kuzibebesha mzigo mkubwa wa madeni nchi za bara hilo.

Onyo hilo la Waziri Mkuu Shinzo Abe, limeonekana kuielekea zaidi China ambayo sera yake ya ujenzi wa miundombinu ya reli na barabara imekuwa ikikosolewa kwamba inaziangamiza nchi masikini kwa kuzibebesha madeni makubwa.

Akizungumza na waandishi habari baada ya kumalizika mkutano wenye dhamira ya kuendeleza ustawi wa Bara la Afrika nje ya mji wa Tokyo, Abe, alisisitiza kwamba nchi za kundi la mataifa yenye uchumi kubwa za G20 ikiwamo China zimejitolea katika mpango wa kuyadhibiti madeni na kwa hivyo ili kuzisaidia nchi za Afrika suala la mzigo wa madeni hayo linapaswa kuzingatiwa na kudhibitiwa yasipite kiwango. **DW**

## Wakimbizi Burundi wakimbilia Congo

**BUJUMBURA,** Burundi

KATIKA siku za hivi karibuni, inaelezwa kuwa kambi za muda za wakimbizi katika maeneo ya Sange na Kavimvira, mashariki mwa Congo zimeendelea kupokea wakimbizi kutoka Burundi.

Zaidi ya watu 100 wanaripotiwa kuvuka mpaka kwa siku na kuorodheshwa katika kambi hizo. Hali hiyo ilianza wiki mbili zilizopita, kwa mujibu wa Gazeti la Burundi la Iwacu. Wakati wanaendelea kusubiri msaada, wakimbizi hao wanaishi katika mazingira mabaya, baadhi wanaonekana mitaani wakiomba omba wasamaria wema.

Katika kambi ya muda ya wakimbizi ya Sange, iliyoko kilomita 15 kutoka Mto Rusizi, kwenye mpaka wa Burundi na DRC, watu wengi wamekuwa wakitoroka makazi yao upande wa wilaya ya Buganda katika Mkoa wa Cibitoke, magharibi mwa Burundi, wakijielekeza katika kambi hiyo, inayopatikana katika Jimbo la Uvira. **FRI**




Waziri Mkuu wa Japan, Shinzo Abe (kushoto) na Rais wa China, Xi Jinping kwenye mkutano wa G20 2019. **PICHA: MTANDAO**

## Aliyejifungulia jela atinga mahakamani

**DENVER,** Marekani



Diana Sanchez, akiwa kitandani peke yake muda mfupi kabla ya kujifungua kwenye gereza la Colorado bila msaada, Agosti mwaka jana. **PICHA: MTANDAO.**

MJAMZITO aliyejifungulia kwenye gereza huko Denver, Colorado nchini Marekani amemshitaki mkuu wa polisi wa mji huo baada ya kujifungua mwenyewe jela bila msaada wa wahudumu wa afya.

Diana Sanchez, anadai kuwa alilazimishwa kujifungua mtoto wake mwaka jana katika benchi lililokuwa na ubaridi ambalo lilikuwa karibu na choo ndani ya jela hilo.

Mwanamke huyo alidai kuwa wahudumu wa gereza hilo walijua kuwa alikuwa anakaribia kujifungua lakini hawakumtilia maanani.

Mkuu wa Idara ya Polisi ya Denver aliiambia BBC kuwa inafanya uchunguzi ili kubaini wafanyakazi waliokuwapo zamu siku hiyo na sababu ya kushindwa kutimiza wajibu wao. Sanchez mwenye umri wa miaka 26 alihukumiwa kwa kosa la wizi wa kitambulisho na mwanamke huyo alikuwa ameandikiwa siku ya kurudi kujifungua kuwa Julai 4, 2018.

Na muda ulipowadia , Sanchez alitoa taarifa kwa ofisa wa afya kuhusu miadi yake ya hospitali wakati huo alikuwa na mimba ya zaidi ya miezi nane.

Mlalamikaji huyo alisema kwamba Julai 31, aliripoti kueleza tena juu ya hali yake na muda wa kujifungua kukaribia.

Aliombz kuzungumza na muuguzi pamoja na mlinzi wa zamu, zaidi ya mara nane asubuhi, "nilikwenda kutoa taarifa kuwa uchungu umeanza na hakuna aliyejali".

Kesi hiyo inayodai kuwa mfungwa alijifungua mwenyewe katika gereza kwa saa tano bila msaada wowote .

Alidai kuwa baadae nesi alikuja kumpima baada ya chupa kupasuka na kumpatia pedi tu, hakufanya jambo lolote jingine na hata kuita gari ya dharura .

"Siku ya kujifungua ilipaswa kuwa yenye furaha zaidi lakini ilibakia kuwa siku yenye hofu, maumivu na udhalilishaji uliopelekea kupata kiwewe cha mimba".

Msemaji wa kituo hicho cha polisi aliiambia BBC kuwa gereza lao lina huduma zote za afya na wanafanya kazi kitaaluma , kuna vifaa vyote vya huduma ya afya katika jela hiyo.

"Tunaelewa hali wanayopitia wajawazito wote walioko jela pamoja na Sanchez mwenyewe, ndiyo maana tuna kitengo maalum cha afya ambacho kinafanya kazi kwa weledi," alisema mhudumu huyo.

Lakini, kuhakikisha kuwa tukio kama hilo halijirudii, mkuu wa kitengo amebadilisha utaratibu kuwa mtu yeyote mwenye ujauzito gerezani akifikia muda wa kujifungua, atapelekwa hospitali badala ya kuhudumiwa hapo.

Madai hayo yamepelekea maofisa walioopelekea uzembe huo kutoka mwanzo kuwajibishwa. **VOA**

# HADITHI

WASWAHILI wana msemo wao unaosema kuwa ufukara ni jereha la ulimwengu. Wakiwa na maana, mtu fukara mara nyingi hukutana na mitihani mikubwa duniani, ambayo mingi husababishwa na baadhi ya binadamu wengine wenye vipato kwa kuwaona hawana thamani na hawahitajiki kuwa na kitu chochote cha thamani.

Kijana anayetoka kwenye familia duni Kadili, anatokea kupendwa na msichana mrembo anayetoka kwenye familia ya kitajiri, Edina. Lakini kitendo hicho kinamsababishia kijana huyo matatizo makubwa ambayo hajawahi kuyapata katika maisha yake, kiasi cha maisha yake kuwa hatarini. Fuatilia mkasa huu wa aina yake.

# JUMBA JEKUNDU- **16**

**Mtunzi anapatikana (0716 350534)**

**Na Adam Fungamwango**




"Unajua wewe mbishi sana." Ilikuwa ni kauli ya kwanza aliyoisikia kwa mtu mwingine aliyeingia kwenye selo hiyo kwa ajili ya kumtoa ndani, lakini haijulikani anapopelekwa.

Hakuwa yule baunsa aliyekuwa akimuuliza maswali na kupiga kwa mkanda wa suruali. Na wala si yule jamaa kibonge aliyemtembeza kwenye bustani na makaburi ndani ya jumba lile.

Kwanza huyu alikuwa kijana zaidi kuliko wenzake. Lakini hakuwa na mwili mkubwa. Kadili alifuatana na kijana yule mpaka kwenye chumba kimoja ambacho ni kama stoo vile. Hata hivyo kulikuwa na viti viwili vya chuma.

"Kaa hapa, nakuja." Ilikuwa ni kauli ya kijana yule aliyeonekana pia ni mpole na hakumchukulia Kadili kama mhalifu.

Dakika tano zilipita, aliingia msichana mmoja mwembamba mrefu aliyebeba sinia lililokuwa na chakula. Hakikuwa kingi sana, lakini kilinukia kiasi cha kumfanya mate kumvuja Kadili, ukichukulia kuwa alikuwa na njaa kwa muda mrefu.

Chakula kiliwekwa kwenye kiti kingine. Hakuongea kitu chochote zaidi ya macho yake kumtazama sana Kadili na yalikuwa yakiongea kuwa 'hiki ni chakula chako'.

Ulikuwa ni wali na nyama iliyopikwa vizuri. Pembeni kulikuwa na mboga za majani, matunda, maziwa na maji ya kunywa.

Kadili alianza kula kwa pupa kutokana na njaa aliyokuwa nayo bila hata kumuangalia msichana yule aliyekuwa akiondoka huku akimtazama Kadili kwa makini na mshangao.

Ndipo alipogundua kuwa hakuwa amekula tangu jana yake mchana. Muda huo ilikuwa ni jioni majira ya saa 10 hivi kwa jinsi alivyoliona jua alipotolewa selo na kijana yule.

Kitu pekee alichokumbuka ni kwamba wakati anachukuliwa nyumbani alikuwa anakula ugali na hata hivyo aliondoka akiwa na bado hajamaliza.

Alilazwa selo hadi asubuhi na tayari ilikuwa imefika jioni. Chakula hakikuchua raundi kikawa kimekwisha. Licha ya kwamba alikula kwa pupa kutokana na njaa, lakini pia ni kitamu kilichopikwa na kungwa na mtu anayeijua vema kazi yake.

Shibe ilianza kumfanya aanze kuwaza. Alishangaa kuona pamoja na mateso makali na vitisho vya kuuawa, lakini watu hawa wamemletea chakula cha kifalme. Chakula ambaye hata yeye mwenyewe hakumbuki aliwahi kula wapi mara ya mwisho.

"Nia yao ni nini?" Alijiuliza. Alikumbuka hadithi za baadhi ya watu mitaani kuwa watu waliohokumiwa kunyongwa, kabla ya kuuawa, maisha huishi maisha kama wafalme. Wanakula vizuri na hawafanyishwi kazi ngumu.

"Ina maana huu msosi mzuri ndiyo wamenipa kusudi baadaye waniue?" Kichwa chake kilizidi kumuuma kwa kujiuliza maswali yasiyojibika.

**************************************

Ilikuwa kama anaangalia sinema isiyoeleweka. Sinema yenye sehemu za kutisha, kuhuzinisha, kushangaza na zingine zikiwa za kutia matumaini.

Sehemu ya chakula kidogo ilimtia matumaini. Lakini hii ya sasa ilimshangaza. Ni baada ya yule kijana aliyemtoa selo na kumpeleka kwenye chumba cha chakula, kurejea tena kumchukua na kupeleka ndani kabisa ya jumba lile kubwa jekundu.

Alikuwa kwenye ukumbi mkubwa sana. Ulikuwa umenakshiwa vizuri kwa mapambo mbalimbali, kiasi cha akili ya harakaharaka kufikiria kuwa ukubwa wa ukumbi na mapambo yake huyaona kwenye picha na sinema za majumba ya wafalme, au kanisani.

Juu kulikuwa na mapambo yaliyomeremeta yakininginia, sambamba na taa kubwa lilizokuwa zimewashwa na kung'aa kama mwezi na nyota angali. Feni za pangaboi zaidi ya tano nazo zilikuwa zinaning'inia kutoka juu, lakini pia zikifanya kazi ambayo ilitakiwa izifanye zikiwa hapo.

Ilionekana kana kwamba kuna kikao hivi kimeandaliwa, kutokana na jinsi viti vilivyopangwa.

Alipelekwa kukaa kwenye kiti kimoja, ambacho mita 30 hivi mkabala kulikuwa na kiti kimoja kikubwa ambacho ni kama vile ambavyo hukaliwa na wafalme. Kilinakshiwa mapambo na vito, kiasi cha kuonekana mtu atakayekuja kukaa hapo ni zaidi ya mgeni wa heshima.

Mbele ya kiti hicho cha enzi kulikuwa na meza kubwa iliyokuwa imetandikwa kitambaa kikubwa cha rangi ya bluu na nakshi nyingine pembeni kama vile maua ya rangi mbalimbali, kiasi cha kupendezesha mandhari ya hapo.

Baada ya kuamriwa kukaa kwenye kiti hicho, kijana yule aliondoka na kwenda kwenye moja kati ya milango mingi ya nyumba hiyo, akatoweka.

Kadili alibaki peke yake akishangaa uzuri wa mandhari ya ukumbi huo, pamoja na jumba hilo jekundu.

Alikiri moyoni kubwa yoyote atakayekuwa anamiliki jumba hilo atakuwa mmoja wa matajiri wakubwa nchini.

Mpaka wakati huo hakujua kusudio zima la watu wale. Ila alichogundua ni kwamba chanzo cha kuletwa pale kilikuwa ni mrembo Edina.

Ghalfa mlango mmoja ukafungiliwa. Walioingia ndani walikuwa ni mabausa watatu. Wawili kati yao ni wale waliokwenda kumchukua nyumbani kwake. Mmoja ni yule aliyekuwa akimpa adhabu na hata kumpiga na mkanda wa suruali mle selo.

Kama vile haitoshi, waliingia watu wengi watano, ambao Kadili hakuwahi kuwaona, wawili wakiwa ni wasichana.

Dakika 10 baadaye ukumbi ulikuwa na kiasi cha watu wapatao 15 hivi ambao wote wanaonekana wanaishi mle mle ndani au kufanya kazi.

Ilipita tena kama dakika tano hivi, sauti kali kama ya king'ora ikasikika. Wote wakasimama kasoro Kadili. Ni kwa sababu hakuelewa chochote kinachoendelea.

Aliyeingia ni mwanamke mwenye umri unaokadiriwa miaka 45 hivi. Alikuwa amevaa kama malkia halisi. Alitembea kwa madaha na maringo, nyuma kukiwa na watu wawili wasio na miili mikubwa wakiwa wanamlinda.

Ingawa hawakuonekana kama mabaunsa, lakini walionekana ni wakakamavu na wenye uwezo wa kufanya kitu chochote kile kumlinda tajiri yao. Walikuwa wametinga suti za bluu.

Uso wake angavu ulionyesha kabisa kuwa ni mwanamke mwenye madaraka au pesa. Wala haihitaji elimu ya chuo kikuu kujua kuwa ndiye mmiliki wa jumba na vitu vyote mle, au mke wa mwenye mali.

Kama ilivyotegemewa, alikaa kwenye kiti cha enzi na kuinamisha kichwa kidogo kama kushukuru, akainua.

Akaangalia pembeni kushoto na kulia kama kuihabarisha hadhira kuwa tayari ameshachukua nafasi yake.

Akaangalia mbele na uso wake ukamuelekezea moja kwa moja Kadili. Kwa aibu Kadili akaangalia chini.

Hadi wakati huo alikuwa hajabadilisha nguo. Ilishaloa na kukauka mara mbili. Kwa mbali alisikia harufu ya jasho lake na nguo zake mwenyewe kutokana na kukaa masaa zaidi ya 24 bila kubadilisha wala kuoga.

Akakunja sura na kutikisa kichwa kwa namna ya dharau. "Ndiyo haka kajitu kenyewe kanakotusumbua?"

"Ndiyo mkuu." Alijibu mmoja wa watu wake waliokuwa wanamsikiliza.

"Wewe kinyago, eti ndiyo unataka kumuoa Edina?" Swali hilo la dharau si tu lilimkwaza Kadili kutokana na kuangaliwa kwa dharau na kila mtu humo ndani, lakini pia lilimshangaza kwa sababu ni jipya kichwani kwake.

Hakuwaza, wala kumwambia hata siku moja Edina kuwa anataka kumuoa. Hajawahi kuwa na hata uhusiano wa kimapenzi na msichana huyo zaidi ya kucheza naye muziki tu.

Kadili sasa alionekana kujutia kitendo chake cha kukubali kucheza muziki na msichana huyo, kwani yute wanayomkuta kwa sasa ni sababu hiyo tu.

"Hapana, si kweli." Alijibu kama vile yuko mahakamani akikanusha tuhuma anazikabiliwa nazo.

"We Edina, njoo huku, mchumba 'ako kaja kutoa barua ya uchumba, njoo ushuhudie tafrija bibi harusi mtarajiwa."

Ilikuwa ni sauti ya mwanamke hiyo iliyojaa mzaha, kejeli, nyodo na dharau.

Mlango ulifunguliwa. Aliyetoka humo hakuna mgeni machoni mwa Kadili. Ni Edina. Hakuna amejipamba kama alivyokuwa akikutana naye Bluu Star.

Alivaa gauni mmoja fupi kiasi cha kuonyesha mapaja yake laini wazi. Alikuwa ameshikwa mkono na mmoja wa mabaunsa ambaye aliyeonekana kumtoa huko alikokuwa.

Sura yake haikuwa na tabasamu. Naye kama ilivyo Kadili hakuwa akimuangalia mtu yoyote ndani. Ni mtu pekee ambaye hakutaka kukaa kwenye kitu, bali aliamua kukaa chini, huku akionekana amenuna kupita kiasi.

**Alivaa gauni mmoja fupi kiasi cha kuonyesha mapaja yake laini wazi. Alikuwa ameshikwa mkono na mmoja wa mabaunsa ambaye aliyeonekana kumtoa huko alikokuwa.**

**Itaendelelea Jumamosi**

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

### VIWANJA / MASHAMBA

**SHAMBA NYUMBA INAUZWA**
Shamba ekari 13 lililopo Vikuruti barabara iendayo Bagamoyo lina matunda, maji ya dawasco na Kisima Kirefu. Piga simu: 0767 237404, 0715 237 404 na 0767 856900.

### NAFASI ZA KAZI

Anahitajika - Mhasibu na sales Lady
Sifa – Awe Mwanamke
Elimu – Diploma

Ofisi yetu ipo Posta – Dar es Salaam
Kwa Mawasiliano :- 0715 – 885 533


## NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz,
au piga simu: 0767 223311


### KUPOTEA KWA VYETI



Edward Nzwila anatangaza kupotea kwa vyeti vifuatavyo cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S2115-0019** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la taifa mwaka 2014 katika shule ya Sekondari Walla, cheti cha certificate chenye namba **LGTI/DTC/DRAIN/2016/024** kilichotolewa na Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo mwaka 2017, cheti cha Diploma chenye namba **LGTI/DTC/DRAIN/2016/024** kilichotolewa na Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo mwaka 2018.

**Polisi Taarifa: DOD/RB/169992/2019**

### KUPOTEA KWA VYETI



**Justa Ngaiza** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba S.0320-015 kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 1991 katika shule ya Sekondari Kigoma, cheti cha kidato cha sita chenye index namba S0202-0514 kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 1994 katika Shule ya Wasichana Sekondari Bwiru.

Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

Polisi Taarifa: DAR/UR/RB/256334/2019

### KUPOTEA KWA CHETI



James Octavian Temu anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba S1060-0107 kilichotolewa na Baraza la Mithihani la taifa mwaka 2007 katika Shule ya Sekondari St. Mary's Hish School. Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.
Polisi Taarifa:
DAR/OST/RB/247001/2019

### KUPOTEA KWA VYETI



Mwijage Wenceslaus anatangaza kupotea kwa vyeti vifuatavyo cheti cha kidato nne, chenye index namba S1049-0124 kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2011 katika shule ya Sekondari St.Thomas Aquinas, cheti cha Certifiacate chenye namba CCM /5114/305/DT kilichotolewa na chuo Cha Kampala International University mwaka 2016, cheti cha Diploma chenye namba NS.1049/0124/2011 kilichotolewa na chuo cha Paradigms Collage of Health Science mwaka 2018 na cheti cha kuzaliwa.
Yeyote atakaevion atoetaarifa kituo chochote cha Polisi.
Polisi taarifa: LIN/LIW/244593/2019

215395802

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA WILAYA**
**KINONDONI**
**SHAURI IA MIRATHI NA 26 YA 2019**
**Maombi ya barua ya usimamizi wa mirathi ya marehemu**
**SUNDAY HONEST MUGANYIZI BAGENDA**
**DHIDI YA**
**RAYMOND**
**BAGENDA.........................................WAOMBAJI**
**/MUOMBAJI**

**TAARIFA YA KAWAIDA**

Watu wote wanaodai kuwa na Haki ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua za usimamizi wa mirathi kwa waombaji hapo

Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 30 Mwezi wa 09 Mwaka 2019.

Hati hii imetolewa Alhamisi tarehe 15 Mwezi 08 Mwaka 2019.

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA WILAYA
KINONDONI

115397302

### KUPOTEA KWA KADI

**Mathew Emilius Nganyanyuka** anatangaza kupotea kwa kadi ya Pikipiki yenye usajili wa namba MC 651 AVA aina ya BOXER yenye engine namba PFZWFC79709.

Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

Polisi Taarifa:
**OB/RB/19009/2017**

115397902

### KUPOTEA KWA KADI

**ASHRAFU SABIHI CHIBWANA**
amepotelewa na kadi ya pikipiki aina ya HAOJUE yenye namba za usajili MC 587 CGS.

Yeyote atakaeiona anaombwa atoe taarifa kituo chochote cha polisi

taarifa ya polisi :
MOR/MOR/RB/251610/2019.

215398102

### TANGAZO

1. Kampuni ya **MM integrated Steel Wills Ltd** inawatangazia wananchi kuwa siku ya Jumapili tarehe **01/09/2019** itapitisha gari lenye vipimo tofauti kutoka **Dar es Salaam kwenda Mboga (Lugoba)**, gari lenye namba za usajili **T 265 BQW/ T997 BSV.**

2. Gari lina vipimo vifuatavyo
   Urefu -16.0
   Upana -2.5
   Kimo -4.8

3. Njia itakayotumika ni barabara ya Bagamoyo hadi Msata-Mboga.

**Tunaomba radhi kwa usumbufu wowote utakaojitokeza.**


## NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI
BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA
Tutumie E-mail:
advertise@guardian.co.tz,
au piga simu: 0767 223311

**Kwa Habari Motomoto**
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie 0767 223 311

Nipashe MWANGA WA JAMII

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# RONALDO KULA CHAKULA CHA USIKU NA MESSI



**MONACO,** Ufaransa

CRISTIANO Ronaldo alitania kwamba, ana matumaini siku moja anaweza kukaa chini na kula chakula cha usiku na mpinzani wake, Lionel Messi wakati wawili hao walipokaa pamoja kwenye droo ya upangaji wa makundi ya Ligi ya mabingwa Ulaya mjini Monaco, juzi Alhamisi.

Ronaldo ametumia muda wake mwingi wa uchezaji soka akishindana na Messi kwa kuwania tuzo kubwa duniani, wakati raia huyo wa Ureno alipocheza kwa kipindi cha miaka tisa kwenye Ligi Kuu ya Hispania, La Liga.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 34 kwa sasa anacheza kule Juventus akiwa na nia ya kubeba taji la Ligi ya mabingwa Ulaya, lakini alibainisha mjini Monaco kwamba, 'amemis' kucheza nchini Hispania kwani Messi 'alimsukuma' kuwa bora.

"Nilihamasika kwa sababu tumekuwa pamoja kwenye jukwaa hili kwa kipindi cha miaka 15 yeye na mimi," alisema Ronaldo.

"Sijui kama hilo limewahi kutokea kwenye soka kamwe, watu walewale wawili kuwa kwenye jukwaa moja kwa miaka hiyo, siyo rahisi.

Wachezaji wote wawili wameshinda tuzo ya Ballon d'Or mara tano na wakajikuta tena wametajwa kuwania tuzo ya mchezaji bora wa mwaka wa Ulaya, na wakashindwa kwa beki wa Liverpool, Virgil van Dijk.

Messi ni mdogo kwa miaka miwili zaidi ya mchezaji huyo wa zamani wa Real Madrid, lakini wote wanaelekea mwishoni mwa uchezaji wao, huku Ronaldo anaamini kwamba, watabakia kwenye vitabu vya historia kwa muda wa miaka mingi kwa kile walichokifanya kwenye soka.

"Bila shaka ninamis kucheza Hispania, tulipambana kwa miaka 15, kitu ambacho kilikuwa kizuri kwetu," aliongeza kusema mchezaji huyo wa kimataifa wa Ureno.

# Sanchez: Asanteni Manchester United




**MILAN,** Italia

ALEXIS Sanchez alituma ujumbe kwa kuwatakia kila la heri wachezaji wenzake wa zamani wa Manchester United baada ya kukamilisha uhamisho wa kutua Inter Milan.

Mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 30, ambaye alitumia misimu mitatu kwenye Ligi Kuu ya Italia, Serie A, akiwa na Udinese kuanzia mwaka 2008 hadi 2011, alijiunga na Nerazzurri kwa mkopo.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Chile alimaliza miezi yake 18 aliyokaa kwenye dimba la Old Trafford ambako alifunga mabao matano katika mechi 45 akitokea Arsenal.

Aliposti baadhi ya picha kwenye ukurasa wake wa mtandao wa Instagram akiwa na wachezaji wenzake wa United, Sanchez aliandika: "Kila la heri kwa kipindi cha msimu uliobakia."

Sasa atacheza kwa pamoja na mshambuliaji mwenzake wa United, Romelu Lukaku ambaye aliondoka klabuni hapo kipindi cha majira ya joto kwa pauni milioni 73.

# Kocha Enrique afiwa na binti yake

**BARCELONA,** Hispania

BINTI wa miaka tisa wa kocha wa zamani wa Barcelona, Luis Enrique amefariki dunia baada ya miezi mitano tangu agundulike kuwa na saratani ya mifupa.

Enrique mwenye umri wa miaka 49, alitangaza kifo cha binti yake huyo, Xana baada ya kuposti ujumbe wa huzuni kwenye ukurasa wake wa Twitter, akimuelezea binti hiyo kama 'nyota atakayeilinda familia'.

Xana alipigania maisha yake baada ya kugundulika na saratani ya mifupa kwa kipindi cha miezi mitano, alieleza kocha huyo raia wa Hispania.

Xana alikuwa mtoto mdogo zaidi kwa Enrique kati ya watoto wao watatu na mke wake, Elena Cullell.

Wanandoa hao wana mtoto wa kwanza wa kiume mwenye umri wa miaka 19, Pacho na binti mwenye umri wa miaka 18 na Sira.

Enrique, ambaye pia aliiwahi kuinoa timu ya taifa ya Hispania, aliwashukuru wote waliomtumia ujumbe wa masikitiko kwa kufiwa na binti yake huyo.

Katika ukurasa wake wa Twitter aliandika: "Binti yetu, Xana amefariki duniani mchana huu (juzi) akiwa na umri wa miaka 9, baada ya kupambana na ugonjwa wa saratani ya mifupa kwa miezi mitano. Tunawashukuru wote kwa mchango wenu katika kipindi hiki kigumu."



HABARI MICHEZO

# Emery: Ozil haondoki Arsenal

**LONDON,** England

UNAI Emery amedokeza kwamba wachezaji zaidi wataondoka Arsenal kabla ya kufungwa kwa pazia la dirisha la usajili la Ulaya, lakini akaondoa uwezekano wa Mesut Ozil kuondoka.

Ozil amekuwa akisumbuliwa na majeruhi tangu Emery achukue mikoba ya Arsene Wenger mwaka jana, akianza katika mechi 20 kati ya 38 za Arsenal za Ligi Kuu msimu wa 2018-19.

Kiungo huyo hadi sasa bado hajacheza mchezo wowote msimu huu tangu alipokumbwa na mkasa wa kuvamiwa na genge la waharifu wakitaka kumpora gari akiwa na mchezaji mwenzake, Sead Kolasinac.

Hakuwapo kwenye mchezo wa wikendi iliyopita ambapo Arsenal walipokea kichapo cha mabao 3-1 kutoka kwa Liverpool, licha ya kufanya mazoezi na kikosi hicho, lakini Emery amemfungulia mlango wa kurudi katika mchezo wa kesho Jumapili dhidi ya Tottenham.

"Wiki hii alifanya mazoezi vizuri na anaendelea vizuri," alisema Emery Alhamisi katika mkutano wake na waandishi wa habari.

"Anakaribia kurudi uwanjani kwa mchezo wa Jumapili, nafikiri hivyo."

Timu nyingi nje ya England zina hadi Jumatatu kuweza kumakilisha usajili wa wachezaji na Ozil ni mmoja wa wachezaji wa Arsenal ambaye amekuwa akihusishwa na mpango wa kuondoka klabuni hapo.

Emery hafikirii kumuuza Ozil, lakini Nacho Monreal anaweza kwa njiani kuelekea Real Sociedad.

"Hatuwezi kusajili mchezaji mwingine, lakini kuna uwezekano wa mchezaji mmoja kuondoka ndani ya siku nne zijazo," alisema.





# BARCA, PSG WAMALIZANA KWA NEYMAR

**MILAN,** Italia

KLABU za Inter Milan na Manchester United zimeafikiana kuhusu usajili wa mshambuliaji, Romelu Lukaku.

Inter sasa itatoa kitita cha pauni milioni 74, dau ambalo Man United walikuwa wakilitaka toka awali.

Barcelona, PSG wamalizana kwa Neymar

PARIS, Ufaransa

KLABU za Barcelona na Paris St-Germain "zimefikia makubaliano juu ya thamani ya Neymar", amesema mwandishi wa BBC Radio 5 Live, Guillem Balague.

Klabu zote mbili zimekubaliana thamani ya mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil kuwa ni euro milioni 200, lakini pia Barca imetoa ofa ya kuwatoa beki wake, Jean-Clair Todibo na kiungo Ivan Rakitic, pamoja na mshambuliaji, Ousmane Dembele ambaye atacheza pale kwa mkopo wa muda mrefu.

Ofa ya Barcelona ya kuwatoa wachezaji watatu imekuja ili waweze kulipa kwa mafungu kiasi hicho cha fedha.

Hata hivyo, kwa wakati huu wachezaji wote watatu wamekataa uhamisho huo.

Maofisa wa Klabu hizo mbili walikutana Jumanne jijini Paris nchini Ufaransa kwa ajili ya kukamilisha dili hilo.

Mshambuliaji Neymar mwenye umri wa miaka 27, alijiunga na PSG kutoka Barcelona mwaka 2017 kwa ada iliyoweka rekodi ya euro milioni 222.

Katika mkutano na waandishi wa habari Alhamisi, kocha wa PSG, Thomas Tuchel alisema Neymar hatahusishwa katika mchezo wa Ligue 1 dhidi ya Metz uliopigwa jana Ijumaa.

Baada ya klabu hizo kufikia makubaliano, sasa inaonekana wazi kwamba mchezaji huyo atatua pale Nou Camp kabla ya kufungwa kwa pazia la dirisha la usajili Jumatatu saa 5:00 usiku.

# Klopp: Tuzo ya Van Dijk ni ya wachezaji

**MONACO,** Ufaransa

JURGEN Klopp amemsifia mshindi wa tuzo ya mwanasoka bora wa kiume wa mwaka wa Ulaya, Virgil van Dijk na kwamba ni zawadi kwa wachezaji wote wa Liverpool.

Van Dijk alifurahia msimu mzuri wa 2018-19, akiisaidia Liverpool kutwaa ubingwa wa Ligi ya mabingwa Ulaya na kuwa nahodha wa Uholanzi aliyeifikisha fainali ya Ligi ya mataifa ya Uefa.

Beki huyo wa zamani wa Southampton aliwashinda wachezaji, Cristiano Ronaldo na Lionel Messi na kutwaa tuzo mjini Monaco Alhamisi.

Klopp haraka akapaza sauti kwa mafanikio binafsi ya Van Dijk na akasema asingeweza kutwaa tuzo hiyo bila ya kikosi cha Liverpool.

"Hongera kwake! Hakika ni kubwa. Nilitaka kumpigia simu haraka, lakini alikwenda jukwaani. Nina furaha kubwa juu yake," alisema Klopp akiiambia tovuti ya Liverpool.

"Nina furaha kwa upande wetu pia kwa sababu anajua kwamba bila vijana wanaomzunguka, hangeweza kushinda tuzo hii.


"Ni zawadi kwetu sote lakini tulimtuma mtu mkubwa kwenda kuichukua. Kwa hakika ni mara chache kwa beki. Ndio, wote tunapenda mabao, tunataka kufunga kwa ajili yao na kuwaona wao, lakini watu wengi wamehamasika zaidi kuhusu nafasi yake ya beki.

"Virg ni beki wa aina yake, kwa asilimia 100 yeye ni mmoja wa beki bora duniani, kwa uhakika kabisa anastahili tuzo hii.

"Kwa sasa tunafurahia matunda mazuri ya kutwaa ubingwa wa Ligi ya mabingwa Ulaya msimu uliopita."



# DO... ZA SOKA MAG... YA ULAYA




# AUBA, LACAZETTE, PEPE KUANZA VS SPURS- EMERY

## Nadhani wanaweza kuanza pamoja na wanaweza kucheza pia wakati wa mechi kama...

**LONDON,** England

KOCHA wa Arsenal, Unai Emery amesema Pierre-Emerick Aubameyang, Alexandre Lacazette na Nicolas Pepe atawachezesha pamoja dhidi ya Tottenham katika mechi ya 'dabi' ya Kaskazini mwa London.

**Watatu hao bado hawajaanza pamoja kwenye mechi ya Ligi Kuu England tangu Arsenal ilipomsajili kwa dau la rekodi Pepe na kuwa mchezaji ghali namba tatu katika klabu hiyo, wakati mshambuliaji huyo wa kimataifa wa Ivory Coast alipotua hapo Emirates akitokea kwa miamba ya Ligue 1, Lille.**

Lacazette amekuwa akisumbuliwa na kifundo cha mguu na aliachwa katika kikosi cha Ufaransa Alhamisi, lakini Aubameyang ameanza msimu mpya kwa kiwango cha juu akitupia mabao mawili katika mechi tatu alizocheza.

Safu ya ushambuliaji ya Arsenal kwa sasa inaelezwa kuwa imara kama zingine za Ligi Kuu England, na Emery sasa anataka kuzingatia kwa kuichagua mechi dhidi ya Spurs kwa kuwachezesha Aubameyang, Lacazette na Pepe kwa pamoja.

"Ndiyo lakini kuwa mpole," Emery aliwaambia wanahabari, juzi Alhamisi wakati alipoulizwa kama watatu hao watakuwa sehemu ya kikosi chake cha kwanza kitakachoanza. "Uamuzi wangu katika kila kipindi ni kufikiri kuhusu namna tulivyo.

"Kwa mfano na Lacazette, alikuwa na matatizo ya kifundo cha mguu. Wiki hii ni wiki bora kati ya tatu zilizopita. Amekuwa bora na anajisikia vizuri na kifundo chake cha mguu, ni chanya kabisa.

"Na Pepe, alichelewa kuja hapa kuliko wengine, lakini anajisikia vizuri katika kila mechi. Aubameyang ni muhimu sana kwetu, alifunga mabao mawili katika mechi zake mbili za mwanzo, alijaribu vizuri mara mbili ama tatu dhidi ya Liverpool.

"Kitu muhimu sana kwangu ni kupata nafasi na baada ya wachezaji kama Aubameyang, Lacazette, Pepe, Micki [Henrikh Mkhitaryan], Reiss [Nelson], [Dani] Ceballos na Mesut [Ozil] tunaweza kufunga na wachezaji tofauti.

"Nadhani wanaweza kuanza pamoja na wanaweza kucheza pia wakati wa mechi kama wote watatu, itategemea ni namna gani tutaamua mpango wa mechi yetu. Bali nina matumaini makubwa na hali hiyo, lakini si hao wachezaji watatu, pia Nelson, Mkhitaryan, [Joe] Willock, Ozil.

"Tunahitaji kuwa tayari kufanya maamuzi mazuri, lakini juu ya yote kuwa na mbadala tofauti kwa wachezaji wetu."

"Kwetu sisi kucheza mechi kama wiki iliyopita dhidi ya Liverpool na wiki hii dhidi ya Tottenham, timu mbili ambazo zimecheza fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya ni kushangaza," Emery.

## ZISIKUPITE

### POGBA HATAONGEZA MKATABA

KIUNGO wa Manchester United, Paul Pogba, 26, hataongeza mkataba mpya kutoka huu wa sasa na anataka kujiunga na Real Madrid haraka iwezekanavyo. ***(Marca - in Spanish)***

### ERIKSEN MBADALA WA NEYMAR

PARIS St-Germain inamtaka kiungo wa Tottenham, Mdenmark Christian Eriksen, 27, kama mbadala wa mshambuliaji wa kimataifa wa Brazil Neymar, ambaye anakaribia kurudi Barcelona. ***(Le Parisien - in French)***

### TUCHEL AMWANGUKIA DEMBELE

KOCHA wa Paris St-Germain, Thomas Tuchel, amempigia simu mshambuliaji wa Barcelona, Ousmane Dembele, 22, kumshawishi kujiunga na klabu hiyo kama mbadala wa dili la Neymar. ***(Le Parisien via Mirror)***

### VERTONGHEN AWINDWA

BAYER Leverkusen inataka kumsajili beki wa kati wa Tottenham, Mbelgiji Jan Vertonghen, 32, kabla ya dirisha la usajili Ulaya kufungwa Jumatatu. ***(Kicker in German)***

### DARMIAN ANUKIA KUTUA PARMA

BEKI wa pembeni wa Manchester United, Matteo Darmian, anafanya mazungumzo kurudi Serie A kujiunga na Parma. ***(La Gazzetta dello Sport via Football Italia)***

### SMALLING AJIENDEA ROMA

BEKI wa Manchester United, Chris Smalling, 29, amesafiri kuelekea Italia kukamilisha mkataba wa mkopo wa muda mrefu wa kujiunga na Roma, na klabu yake inajiandaa kupokea ada kiasi cha pauni milioni 2.7. ***(Mirror)***

### EMERY AMFUNGUKIA NACHO

KOCHA wa Arsenal, Unai Emery amesema beki wa pemebeni Mhispania Nacho Monreal, 33, ambaye amekuwa akihusishwa na Real Sociedad, anaweza kuondoka kabla ya dirisha la usajili Ulaya kufungwa. ***(Mirror)***

### POCHETTINO AMPOTEZEA AURIE

BEKI wa Tottenham, Mauricio Pochettino, hajutii kutokuwa na beki Muivory Coast Serge Aurier, 26, katika mechi ya 'dabi' ya Kaskazini mwa London dhidi ya Arsenal wakati huu akiwa yupo tayari kuondoka kabla ya dirisha la usajili Ulaya kufungwa Jumatatu. ***(Evening Standard)***

### UNITED YAMWANIKA DYBAL

MANCHESTER United imekimbia dili la kuinasa saini ya mshambuliaji wa Juventus, Paulo Dybala, 25, majira haya ya joto kutokana na mshahara mkubwa aliohitaji Muagentina huyo ambaye alitaka kulipwa pauni milioni 18 kwa mwaka. ***(Mail)***

### PIQUE: MAGUIRE ATAIBEBA UTD

BEKI wa Barcelona, Gerard Pique, anatumai Harry Maguire anaweza kuisaidia klabu yake ya zamani, Manchester United kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu England. ***(Express)***

### SANCHEZ ATUMA SMS UNITED

MSHAMBULIAJI wa kimataifa wa Chile, Alexis Sanchez, 30, alituma ujumbe kwenye Instagram kwa wachezaji wenzake wa Manchester Utd kabla ya kutua Inter Milan kwa mkopo. ***(Manchester Evening News)***

## HABARI MICHEZO

### MSIMAMO LIGI KUU BARA

| | P | W | D | L | F | A | PTS |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. Simba | 1 | 1 | 0 | 0 | 3 | 1 | 3 |
| 2. Lipuli | 1 | 1 | 0 | 0 | 3 | 1 | 3 |
| 3. Kagera Sugar | 1 | 1 | 0 | 0 | 2 | 0 | 3 |
| 4. Namungo | 1 | 1 | 0 | 0 | 2 | 1 | 3 |
| 5. Azam | 1 | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 3 |
| 6. Ruvu Shooting | 1 | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 3 |
| 7. Polisi Tanzania | 1 | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 3 |
| 8. Mwadui | 1 | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 3 |
| 9. Mbao | 1 | 0 | 1 | 0 | 1 | 1 | 1 |
| 10. Alliance | 1 | 0 | 1 | 0 | 1 | 1 | 1 |
| 11. Mbeya City | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| 12. TZ Prisons | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| 13. Ndanda | 1 | 0 | 0 | 1 | 1 | 2 | 0 |
| 14. Yanga | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 |
| 15. Coastal Union | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 |
| 16. Singida United | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 |
| 17. Kinondoni MC | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 |
| 18. Mtibwa Sugar | 1 | 0 | 0 | 1 | 1 | 3 | 0 |
| 19. JKT Tanzania | 1 | 0 | 0 | 1 | 1 | 3 | 0 |
| 20. Biashara United | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 2 | 0 |

# ARSENAL KWA WAJERUMANI, UNITED MCHEKEA EUROPA

**MONACO, Ufaransa**

MANCHESTER United itakabiliwa na kusafiri umbali wa maili 6,000 kwenda Kazakhstan kucheza dhidi ya Astana kwenye mechi ya Europa League.

**Washindi hao wa Europa League mwaka 2017, pia wataivaa Partizan Belgrade na AZ Alkmaar, wakati Wolves itakayocheza Europa League kwa mara ya kwanza tangu mwaka 1980, ikikabiliana na Besiktas, Braga na Slovan Bratislava.**

Arsenal, ambayo ilipoteza dhidi ya Chelsea katika fainali ya msimu uliopita, imepangwa kundi moja na Wajerumani Eintracht Frankfurt, Standard Liege na Vitoria.

Celtic itaivaa Lazio, wakati Rangers ikiwa katika kundi gumu na Porto.

Katika droo iliyopangwa jana; Kundi A linaundwa na Sevilla, Apoel Nicosia, Qarabag na F91 Dudelange wakati Kundi B likiwa na Dynamo Kiev, FC Copenhagen, Malmo na Lugano, kwa upande wa Kundi C zimo Basel, Krasnodar, Getafe na Trabzonspor.

Kundi D likijumuisha Sporting Lisbon, PSV Eindhoven, Rosenborg na Lask, huku Kundi E likiundwa na Lazio, Celtic, Rennes na Cluj, kwa upande wa Kundi F kuna Arsenal, Eintracht Frankfurt, Standard Liege na Vitoria wakati Kundi G likiwa na Porto, Young Boys, Feyenoord na Rangers.

CSKA Moscow ipo Kundi H pamoja na Ludogorets, Espanyol na Ferencvaros huku Kundi I likiwa na Wolsfburg, Gent, Saint-Etienne na Olexandriya, kwa upande wa Kundi J linaundwa na Roma, Borussia Monchengladbach, Istanbul Basaksehir na Wolfsberger AC

Kundi K kuna Besiktas, Braga, Slovan Bratislava na Wolves huku Kundi L ndipo walipo Manchester United, FC Astana, Partizan Belgrade na AJ Alkmaar.

Fainali ya michuano itapigwa mjini Gdansk, Poland Mei 27, mwakani.




Mshambuliaji wa Simba, Meddie Kagere (katikati), akipongezwa na wachezaji wenzake kwa kuifungia timu yake bao la pili wakati wakishinda 3-1 dhidi ya JKT Tanzania, kwenye mechi ya Ligi Kuu ya Vodacom iliyopigwa Uwanja wa Uhuru juzi. Kulia ni Clautos Chama akimpongeza Mzamiru Yassin aliyetoa pasi ya mwisho kwa mfungaji. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Mavugo amfuata Msuva

**Na Mwandishi Wetu**

STRAIKA wa zamani wa Simba SC na Napsa Stars ya Zambia, Mrundi Laudit Mavugo, amejiunga na Klabu ya Difaa El Jadida ya Morocco anayocheza mshambuliaji Mtanzania Saimon Msuva.

Imeelezwa kuwa dili hilo tayari limekamika na Mavugo sasa atakuwa sehemu ya kikosi cha wachezaji wa timu hiyo kwa msimu huu.

Mavugo ambaye alichezea Simba kwa misimu miwili 2016/17 na 2017/18, kabla ya kuondoka kutokana na kuchoka kusugulishwa benchi, amejiunga na Difaa El Jadida akitokea Napsa Stars ya Zambia.

Kwa misimu miwili aliyoichezea Simba aliifungia mabao 10, licha ya kusajiliwa kwa mbwembwe huku wengi wakiamini angetisha kwa kucheza na nyavu.

Msimu wa kwanza aliifungia Simba mabao manne kabla ya kuhitimisha na mabao sita msimu wa pili na kutupiwa virago vyake.

# KMKM, Malindi dimbani Ngao ya Jamii kesho

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

MIAMBA ya soka visiwani Zanzibar KMKM na Malindi itashuka katika dimba la Amaan kuwania Ngao ya Jamii ambayo ni maalum kwa ajili ya kukaribisha msimu mpya wa Ligi Kuu visiwani hapa.

Mechi hiyo huwakutanisha mabingwa wa Ligi Kuu Zanzibar, ambao ni KMKM na bingwa Kombe wa FA, Malindi.

Awali mechi hiyo ilipangwa kufanyika Agosti 24, mwaka huu kwa mujibu wa Kalenda ya Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), lakini ikasogezwa mbele kutokana na timu hizo kukabiliwa na mechi za marudiano za Ligi ya Mabingwa kwa KMKM na Kombe la Shirikisho Afrika kwa timu ya Malindi.

Akizungumza na waandishi wa habari, Mjumbe wa kamati ya Mashindano ya ZFF kwa niaba ya Katibu wa kamati hiyo, Hawa Abdallah, alisema mchezo huo wa Ngao ya Jamii unatarajiwa kupigwa katika dimba la Amaan majira ya saa kumi alasiri na kupambwa na burudani mbalimbali.

Alisema mechi hiyo itatanguliwa na mchezo wa timu ndogo za chini ya umri wa miaka 21 kwa timu hizo za KMKM na Malindi.

Aidha, alisema katika mchezo huo, ZFF shirikisho la Soka Zanzibar imeona ipo haja ya kubuni ngao ambayo itaendana na uhalisia wa visiwa vya Zanzibar ikilinganishwa na ngao zilizokuwa zikitolewa miaka ya nyuma.

Hata hivyo, ZFF imewaomba mashabiki wa Soka visiwani Zanzibar kujitokeza kwa wingi kushuhudia mechi hiyo ambayo imepangwa kuchezwa kwa sura tofauti ili iweze kuwavutia mashabiki wa timu hizo na hata wadau wa soka kwa ujumla.

# Michezo

Jumamosi Agosti 31, 2019
Nipashe




Auba, Lacazette, Pepe kuanza vs Spurs- Emery

UKURASA 30

MWAKA WETU...



Beki wa Liverpool, Virgil van Dijk (kushoto), akiwa na tuzo yake ya Mchezaji Bora wa Mwaka wa Uefa sambamba na mlinda mlango wa timu hiyo, Mbrazil Alisson, aliyetwaa tuzo ya Kipa Bora wa Mwaka baada ya kutangazwa kushinda kinyang'anyiro hicho usiku wa kuamkia jana katika hafla iliyofanyika Monaco, Ufaransa. **PICHA: MTANDAO**

## Klopp: Tuzo Van Dijk ya wote

**MONACO,** Ufaransa

JURGEN Klopp amemsifia mshindi wa tuzo ya mwanasoka bora wa kiume wa mwaka wa Ulaya, Virgil van Dijk na kwamba ni zawadi kwa wachezaji wote wa Liverpool.

HABARI UK 29

## Ronaldo, Messi kula chakula cha usiku pamoja

**MONACO,** Ufaransa

CRISTIANO Ronaldo alitania kwamba, ana matumaini siku moja anaweza kukaa chini na kula chakula cha usiku na mpinzani wake, Lionel Messi wakati wawili hao walipokaa pamoja kwenye...



HABARI UK 28

# ‘Kuna swali kwa Wabrazil?’

## ●●● Akunwa na kiwango walichokionyesha Uhuru, mashabiki wasema Wawa atapotea, Kotei...

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya mashabiki kwa muda mrefu kumtaka Kocha Mkuu wa Simba, Mbelgiji Patrick Aussems kuwachezesha wachezaji wa Kibrazil waliosajiliwa na klabu hiyo msimu huu, huku watani zao Yanga wakiwatania kuwa wamesajili ‘magarasha’ hatimaye kocha huyo amekata kiu hiyo na kuwauliza “kuna swali tena?”.

**Simba imesajili wachezaji watatu kutoka Brazil, beki Tairone Santos da Silva aliyeanguka wino wa miaka miwili kuitumikia klabu hiyo, mshambuliaji Wilker Henrique da Silva na kiungo kiraka Gerson Fraga Viera.**

Katika mechi ya juzi ya Ligi Kuu ya Vodacom dhidi ya JKT Tanzania iliyopigwa Uwanja wa Uhuru, Da Silva alikuwa majeruhi, lakini Tairone na Fraga walianza na kuonyesha kiwango cha hali ya juu ambacho kilimkuna Aussems pamoja na mashabiki wa Simba.

Akizungumza baada ya mechi hiyo, Aussems alisema: “Kila mara nimekuwa nikulizwa kuhusu Wabrazil, Wabrazil, Wabrazil... sasa mmewaona, kuna swali tena?”

Aussems alieleza kufurahishwa na kiwango kilichoonyeshwa na wachezaji Tairone ambaye kama si umakini wa beki wa JKT Tanzania, Mohamed Fakhi kuokoa mpira wa kichwa uliounganishwa kimyani na Mbrazil huyo, angeiandikia Simba bao.

“Wamecheza vizuri na Tairone angeweza kufunga bao, ila kwa ujumla sikufurahishwa na namna timu nzima ya Simba ilivyocheza kwani ilicheza ‘kitoto’ na ingeweza kupata mabao hata matano.

“Unajua Simba ni timu kubwa sana hapa nchini, kiwango ilichokionyesha hakikuniridhisha kabisa katika mchezo wa leo (juzi),” alisema Mbelgiji huyo.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti uwanjani hapo, mashabiki wa Simba walionyesha kukunwa na uwezo wa Tairone huku wakimtaka Aussems kuendelea kutoa nafasi kwa mchezaji huyo ambaye wanaamini ni zaidi ya Pascal Wawa hata beki aliyeondoka, Juuko Murshid.

Aidha, kwa upande wa Fraga walisema kwa namna anavyokaba na kutoa pasi za mwisho wana uhakika sasa wanaweza kumsahau kiungo wao kipenzi, James Kotei aliyemaliza mkataba na kukataa kuongeza.

“Huyu beki (Tairone) ni fundi sana wa ‘kubloku’ na ametulia sana hana papara, lakini pia akipanda ana madhara sana kwa mabeki wa timu pinzani, kwanza anajua kuanzisha mashambulizi, ni aina ya beki mwenye sifa zote,” alisema shabiki aliyejitambulisha kwa jina la Benson Jackson.

Hamisi Athumani, shabiki mwingine aliyetoa tathimini yake kuhusu Wabrazil hao, alisema: “Tazama Simba ilikuwa na tatizo la mabeki wanaoruka kucheza mipira ya juu, na huyu Tairone amekidhi haja hiyo kwani anatumia vema urefu wake na anakaba nafasi.” Shabiki mwingine aliyejitambulisha kwa jina la John Kondo, alimwelezea Fraga kumudu vema ukabaji kwa nidhamu katika dimba la kati huku akisema ni muda tu unahitajika kuweza kuzoeana vema na wenzake kabla ya Simba kumsahau kabisa Kotei.

“Wanaowabeza Wabrazil hawa sasa watafunga midomo yao, hawa jamaa wana mpira mkubwa lazima hilo tulikubali, tuache utani usiokuwa na maana,” alisema.

Simba inatarajia kurudi tena dimbani mara baada ya mapumziko ya mechi za kimataifa, ambapo itaikaribisha Mtibwa Sugar iliyotoka kupoteza mechi ya ufunguzi kwa mabao 3-1 dhidi ya Lipuli FC.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002